الصَّارِمُ البَتَّارِ فِي التَّصَدِّي لِلسَّحَرَةِ الأَشْرَارِ

TAFSIRI YA

as-S̲ârimul-Battâr
Fit-Tas̲addî Lis-Sah̲aratil-Ashrâr

UPANGA MKALI WA KUPAMBANA NA WACHAWI WAOVU

Mwandishi:
Wah̲îd 'Abdus-Salâm Bâlî

Mfasiri:
Uthmân Muh̲ammad Alî

Chapa mpya 2014

دار الحكمة للتأليف والترجمة
al-Hikma For Authorship & Translation.
P.O. Box 81691, Mombasa 80100, Kenya. East Africa.
Mobile: (+254) 0722-597959
E-mail: alhikmah1992@yahoo.com

Tafsiri ya "*as-Sârimul-Battâr Fit-Tasaddî Lis-Saharatil-Ashrâr*" (Upanga Mkali wa Kupambana na Wachawi Waovu)

Mfasiri: 'Uthmân Muhammad 'Alî

KITABU HIKI, PIA KINAPATIKANA:

مكتبة المدينة

Maktabatul-Madinah
Singida, Tanzania
(+255) 0769044988
Ubavuni mwa Markaz Noor (Islamic)

مكتبة القصواء

Maktabatul-Qaswâ
Kondoa, Tanzania.

KWA JINA LA ALLÂH MWENYE KUREHEMU WEMA NA WABAYA DUNIANI, MWENYE KUREHEMU WEMA WATUPU AKHERA

بسم الله الرحمن الرحيم

NENO LA MFASIRI

Kila jinsi ya Sifa njema ni ya Allâh. Rehma na amani zimwendee Mtume wetu Muhammad, Aila yake na Maswahaba wote.
Waba'd;

Hii ndio chapa mpya ya ***as-Sârimul-Battâr, fit-Tasaddî lis-Saharatil-Ashrâr* (Upanga Mkali wa Kupambana na Wachawi Waovu),** ambapo chapa ya kwanza, ilitoka mwaka wa 1428 Hijriyyah; mwafaka na 2007 Miladiyyah, wasomaji wakafaidika vya kutosha; kwa sababu ni kitabu cha aina yake kufafanua kwa kina mambo ya uchawi, na katika vitabu vya Kiswahili, hakuna kitabu kilichoandikwa kwa mtindo huu kama alivyoandika Sheikh Wahîd 'Abdus-Salâm, Allâh Amjazi kila la kheri. Fauka ya hapo, mwandishi mwenyewe alikuwa akiwatibu wenye tatizo hili, kwa hivyo kazi aliyoifanya, ina tajriba.

Namshukuru Allâh kwa kuwa watu wengi wamefungukiwa na mengi kuhusiana na mambo haya ya kimazingira. Si Waislamu pekee, hata wasiokuwa Waislamu pia, nao wametaalamika, kwa sababu tatizo hili, lawakumba wote.

Vile vile nimepokea barua nyingi ambazo watu wanashukuru kwa juhudi hii ndogo, na wengine wakitarajia vitabu vingine zaidi. Allâh Atuwezeshe kufanya mengi zaidi.

Miongoni mwazo, ni barua iliyotoka kwa Dr. Masudi Mohamed, wa Congo (Zaire), aliyekipata kitabu hiki bila ya kutarajia, akaniambia: "Nilikisoma njiani kitabu hiki nilipokuwa nikirudi nyumbani DRCongo, nikawa nina Imani kuwa Allâh Aliijibu Dua yangu ya kupata kinga kutoka Kwake dhidi ya matatizo mengi ya husuda na uchawi. Nimepigana navyo muda wa miaka mingi kwa Nguvu Yake Allâh." Akasema pia: "Sasa nitaanza matibabu binafsi ya kijicho; nina Imani Allâh Ataniponya." Akaendelea: "Kitabu hiki ni tofauti na vitabu

vingine; sababu mwandishi humkabidhi Allâh Uwezo kwa yote." Hatimaye akamalizia kwa kuniombea dua njema: "Mungu Akuzidishie kheri duniani na Akhira kwa kazi hii, na akinge kitabu hiki na vita vya makuhani na wachawi ili kiendelee kupatia Waumini tiba kwa njia ya Allâh Karim."(1)

Kitabu hiki, ni miongoni mwa vitabu vilivyoenea sana katika ulimwengu wa Tiba ya Qur'âni. Watu walikuwa wakitaabika na masaibu yanayowasibu wakati wanapopatwa na tatizo la sihiri (uchawi). Ilibidi mtu anaposihiriwa, amwendee mchawi ili amwague! Ukimwuliza "Mbona wafanya hivyo?" Atakwambia: "Nipe tiba mbadala itakayonizuwia nisiende huko."

Lakini Allâh kwa rehma Yake juu ya waja Wake, akamtoa Mwanachuoni mkubwa aliyejitoa muhanga kujaza pengo hili. Akaanza kulishughulikia tatizo hili, akawatibu watu kwa moyo wa ikhlasi. Ameleta mafanikio ya kuridhisha na watu wakapata kuepukana na njia za upotofu.

Tatizo la watu kusihiriana na kurogana, limeongezeka hasa wakati huu wa *maendeleo*. Mtu amwonapo jirani akipata mafanikio, moyo wake huanza kutweta na kuchemka kwa husuda na kwenda kwa waganga na wachawi ili mwenzie aharibikiwe, hata kama hatofaidika kwa chochote katika uharibifu huo! Au utamuona mwanamke anayetaka *kummiliki* mumewe, akienda kwa waganga hao ili wawafanyie vitu vya kuwamiliki waume zao. Hapo utamuona mwanamume kwa mkewe ni kama kondoo, hupelekwa popote naye akafwata. Hufikia wakati, yule mume akawa hamtambui yeyote katika jamii, si mama wala dada, bali hao huwa ndio maadui wake na mahasidi wanaotaka kumvunjia nyumba!

Wakati hayo yanatendeka, mwanamke huyu huwa yumo furahani kuona kuwa yake yametimia, bali hujionea fahari mbele ya wengine kwa kitendo hiki. Hebu niambie, mama aliyembeba mwanawe miezi 9 tumboni kwa taabu na mateso, akamlea kwa kila aina ya taklifu, yuwaketi na njaa ili yeye ale, yuwavaa nguo za viraka ili mwanawe ang'are. Leo huwaje mama huyu akawa ndiye hasidi wa ndoa yao? Kwa hivyo, mambo kama haya ukiyatazama kwa makini, utaona nyuma yake pana mchezo mbaya wa sihiri na kurogana.

---

(1) Nimerekebisha kidogo na kuifupisha barua.

Baadhi ya sehemu; kama vile Mombasa, Lamu, Zanzibar na kwingineko, wachawi na waganga, huitwa *waalimu* ili mtu asione vibaya kumwendea *Maalim*; kwa sababu mtu akisema yuwaenda kwa mganga au mchawi, mbali na watu, hata nafsi yake pia humsuta. Lakini asemapo yuwaenda kwa *Mwalimu* au *Fundi*, nafsi yake itamruhusu; mithili ya aliyemchinja panya na akamuunga vizuri kwa bizari na masala, na akajiambia kuwa, hiyo ni nyama ya sungura. Kidogo italeta takhfifu moyoni; japo ukweli, hiyo ni nyama ya panya!

Kumbuka, matatizo mengine, hayatokani na uchawi wala urogi, bali yamechangiwa na mambo mengi ikiwemo vyombo vya habari, ambavyo kila kuchapo, humpa mwanamke kipaumbele, na kuonyesha kuwa mwanamke anadhulumiwa tu, wala hana kheri apatayo! Lakini vyombo hivi, ni vipofu kuona mema wanayotendewa wanawake hao, hawaoni mapesa wanayopewa, mali wanayotunukiwa, gharama za kila siku na ulinzi wanaopewa na mengine mengi. Na hivi vipindi vya televisheni na masinema yasoneema, aghlabu havina mafunzo ela kumtia ufidhuli mwanamke, akajiona kama kichwa-mchunga; kitahamaki unaulizwa mswali kama mtoto, na kukuona ni mtu usiyejua maana na thamani ya mwanamke! Bali na wengine, hufanya makubwa zaidi ya hayo, lakini kinachoonekana, ni "mwanamke kunyanyasika"![1] Basi ndugu, uonapo hayo, usisingizie uchawi.

Sihiri (uchawi) huwa na nguvu iwapo aliyesihiriwa hana kinga ya kusoma nyuradi alizofundisha Mtume صلى الله عليه وآله وسلم.

Unaweza ukauliza: Sihiri ni nini? Na je ni kweli? Ulamaa (Wanazuoni) wamesema nini juu ya jambo hili? Majini wapo kweli? Mchawi humleta vipi jini? Muna aina ngapi za sihiri? Dalili za sihiri na mchawi ni zipi? Wachawi hutumia mbinu gani ili kufanikisha mambo yao ya kishetani? Kijicho na husuda ni nini? Mtu hufungwaje? Na je mtu atawezaje kujinasua na yote hayo?

---

[1] Na hivi sasa kumezuka kundi la wanawake *wasomi,* ambao wana kazi na fedha za kutosha, lakini mwelekeo wao, ni kutotaka maisha ya ndoa; kwa sababu ni maisha ya kunyanyasika! Kwa akili zao hizi, kwenda kufanya machafu na kujidunisha, huko si kunyanyasika, bali ndio kuifikia ndoto waliyoiota ya kuwa na *future* nzuri! Ndio falsafa na mtindo unaokwenda na wakati! Allâh Atuongoze, na Atupe fahamu ya kutambua vigumu. Alokufa, Mungu Amrahamu!

Majibu ya maswali hayo na zaidi yake, yapatikana kwa upana katika kitabu hiki.

Namuomba Allâh, Atufadhili kwa Radhi na Mapenzi Yake, Atudumishe katika kumtii Yeye na mengineyo yenye kufurahisha, wala Asitupokonye tunu na hidaya Alizotupa. Namuomba Atunufaishe sote ajmaina na kila atakayekisoma kitabu hiki au kukichapisha. Namuomba Allâh Atupe vipawa vikubwa, Azitwahirishe nyoyo na viungo vyetu kutokana na maasi yote, Atujaalie tuwe ni wenye kumuachia Yeye mambo yetu, kumtegemea Yeye Pekee na kumpa mgongo asiyekuwa Yeye katika kila dakika na nukta.

Nimejihifadhi kwa Allâh, nimemwegemea Allâh, Alitakalo Allâh ndilo liwalo, hakuna hila ya kuepuka mabaya wala nguvu ya kufanyia utiifu ispokuwa ni kwa Msaada wa Allâh. Allâh Ananitosha, na Ndiye Mstahiki wa kutegemewa. Sifa njema na neema zote ni Zake, Kwake Pekee naomba taufiki na kuhifadhiwa.

Rehma na amani zimwendee Mtume Wake Muhammad, Aila yake na Maswahaba wote.

'Uthmân Muhammad Alî
***Muharram*, 24, 1435 Hijriyyah**
27/11/2013
Mombasa, Kenya.

MATAMSHI YA HERUFI

Herufi za madda (zinazovutwa) huwekewa kofia (ˆ) juu yake, mfano:
â = aa. Mfano: *All**â**humma* (*All**aa**humma*).
î = ii. Mfano: *Inn**î*** (*Inn**ii***).
û = uu. Mfano: *Innah**û*** (*Innah**uu***).
Neno likianza kwa A bila ya kutiwa (‘) juu yake, au herufi hiyo ya A ikawekewa mstari (-) kabla yake, hutamkwa kwa sauti ya *hamza*. Mfano: *as-**a**luka*.
H = ح mfano: *Al**h**amdu* (ina mstari chini).
S = ص mfano: ***s**alâtî* (ina mstari chini).
Dh = ض mfano: *a**dh**âllîn* (ina mstari chini).
T = ط mfano: ***t**alaba* (ina mstari chini).
Dhw = ظ mfano: *a**dhw**lima*.
Ishara ya (‘) kabla ya herufi, ni (ع), mfano: ***‘a**laihim*, *a**‘û**dhu* na ***‘i**nda*.
Herufi yenye shadda (inayokazwa) huandikwa mara mbili, mfano: *Rabbi*, *inna* n.k.

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

KWA JINA LA ALLÂH MWENYE KUREHEMU WEMA NA WABAYA DUNIANI, MWENYE KUREHEMU WEMA WATUPU AKHERA

UTANGULIZI
Chapa Ya Kumi

Namhimidi Allâh Aliyemtuma Mtume Wake kwa uongofu na Dini ya haki ili Aipe ushindi juu ya dini zote hata makafiri wakichukia. Akajaalia baada yake, Wanazuoni wenye amali, Maimamu mujtahidina, Mafaqihi waliohifadhi Sharia, Mu<u>h</u>addithina walioibeba <u>H</u>adîth na walinganizi wenye kualika katika uongofu na kuepusha ubatilifu. Hawa wote ndio walioibeba Dini hii na ndio mawarithi wa Mitume.

يَا سَيِّدَ الرُّسْلِ طِبْ نَفْسًا بِطَائِفَةٍ ❊ بَاعُوا إِلَى اللهِ أَرْوَاحًا وَأَبْدَانَا

Ewe bwana wa Mitume, tulia moyo wako kwa watu waliomwuzia Allâh roho na viwiliwili vyao.

قَادُو السَّفِيْنَ فَمَا ضَلُّوْا وَلاَ وَقَفُوْا ❊ وَكَيْفَ لاَ وَقَدِ اخْتَارُوْكَ رُبَّانَا

Wameiongoza safina, hawakupotea wala hawakusimama. Vipi isiwe hivyo na ilihali wamekuchagua wewe uwe ndiye rubani?

أَعْطَوْا ضَرِيْبَتَهُمْ لِلدِّيْنِ مِنْ دَمِهِمْ ❊ وَالنَّاسُ تَزْعُمُ نَصْرَ الدِّيْنِ مَجَّانًا

Kodi yao ya damu wameipa Dini, na watu wanadai kuinusuru Dini bure.

عَاشُوْا عَلَى الْحُبِّ أَفْوَاهًا وَأَفْئِدَةً ❊ بَاتُوْا عَلَى الْبُؤْسِ وَالنَّعْمَاءِ إِخْوَانًا

Waliishi juu ya mapenzi kwa ndimi na nyoyo, wameishi katika umasikini na neema wakiwa ndugu.

اللهُ يَعْرِفُهُمْ أَنْصَارَ سُنَّتِهِ ❊ وَالنَّاسُ تَعْرِفُهُمْ لِلْخَيْرِ أَعْوَانَا

Allâh Anawajua kuwa ndio Ansari wa Sunnah yake, na watu wanawajua kuwa ni wasaidizi wa mambo ya kheri.

Nashuhudia kuwa hakuna Anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa ni Yeye Pekee, Hana mshirika, Ufalme na shukrani zote ni Zake, Naye ni Muweza wa kila jambo. Na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja Wake na ni Mtume Wake. Amefikisha ujumbe, ameifikisha amana, ameunasihi umma, Allâh Ameondoa kero kwa sababu yake (Mtume صلى الله عليه وآله وسلم), Akaongoza watu kwa sababu yake, Akaongoza kutoka katika upotofu kwa sababu yake. Ewe Mola, Tujaalie ni wenye kumfuata, wenye kuiandama Sunnah yake, wenye kuishika Dini yake na ni wenye kutembea katika njia yake.

Ewe Mola, kama tulivyomuamini nasi hatukumuona, basi Usitunyime kumuona Peponi. Ewe Mola, kama tulivyoifuata Sunnah yake basi Tunyweshe hodhi yake kinywaji kizuri, tusipate kusikia kiu baadaye milele.

Ewe Mola, Jaalia amali yangu hii, iwe ni halisi kwa ajili Yako tu, wala si kwa mwingine, Uninufaishe kwayo siku ambayo hayatafalia chochote mali wala watoto, ispokuwa atakayemwendea Allâh kwa moyo uliosalimika.

Ama baada ya haya; tangu kitoke kitabu *Wiqâyatul-Insân, Minaljinni Wash-shaitân* (Kinga ya Mwanaadamu Dhidi ya Jini na shetani), na nilikuwa nimeahidi katika mwisho wake kuwa nitataoa kitabu "*as-Sârimul-Battâr Fit-Tasaddî Lis-Saharatil-Ashrâr"* (Upanga Mkali wa Kupambana na Wachawi Waovu). Tangu wakati huo, barua hunimiminikia kwa wingi mno kutoka mataifa ya Kiislamu zikinihimiza kukitoa kitabu hiki. Kwa kweli nilikuwa nimeshughulishwa na baadhi ya mambo muhimu ya kiilimu; kama vile kufundisha somo la *Fiqhul-Muqâran* (Fiqhi Linganishi) kwa wanafunzi; nalo somo hili linahitaji juhudi kubwa ya kukusanya kauli, dalili na njia za dalili zenyewe, na inahitaji juhudi kubwa zaidi katika kutilia nguvu na kuzidurusu vema dalili na hoja ili kuijua njia sahihi na ambayo si sahihi. Basi nikawa nikiuwona uwanda huu – yaani kuifundisha Fiqhi kwa njia hii niliyoitaja

– ni aula zaidi kutolewa wakati hasa katika zama za mwamko wenye baraka unaoshuhudia mashababu wengi wakiielekea ilimu. Kwa sababu kila mwamko usiokwenda juu ya ujuzi, basi upo kwenye maangamivu; na kila ukamataji Dini usiojengeka katika ufahamu (Fiqhi), basi upo karibu zaidi na upotevu.

Na kwa taathira ya barua zilizonifikia kutoka sehemu mbalimbali, na msisitizo wa makampuni ya uchapishaji, nimekata sehemu katika wakati wangu, ndipo nikaandika kitabu hiki na nikakifupisha sana. Nikakifanya ni kama mada ya maudhui mbalimbali, na ni kama asili katika furui (tanzu). Sikuweza kujikatia wakati – bali na wakati wa wanafunzi – zaidi ya hapo. Ndipo kikaja kitabu hiki kilichosambazwa nakala zaidi ya elfu thalathini (30,000) katika miezi michache tu ya mwanzo. Nikadhani kuwa nimetekeleza wajibu na nimeisambaza ilimu. Lakini nilipigwa na butwaa kwa barua nyingi kutoka Misri, Saudia, mataifa ya ghuba, nchi za Sham (Syria, Palestina, Lebanon na Jordan), Libya, Tunisia, Aljeria, Morocco na nchi nyingine za Kiislamu, barua zilizobeba malalamiko, uchungu na hali za kustaajabisha, na pia wakinibashiria kuwa wao wametumia tiba hii ya ki-Sharia iliotajwa katika Qur'âni, Allâh Akawaponya. *Alhamdulillâhi Rabbil'âlamîn!* Wala sitoisahau ile barua niliyoipokea kutoka Morocco. Kwa ufupi, barua hiyo inaeleza kuwa shababu mmoja yeye na mama yake walikuwa wakifanya vijinyuzi (vya shirki). Yule shababu akakisoma – kiasi fulani – kitabu hiki cha *as-Sârim*. Akajua kwamba wao walikuwa katika upotevu, akamdokezea mama yake. Nao walikuwa mashuhuri kwa kazi hiyo, ikawa uzito wao kuiacha. Wakaamua wahamie sehemu nyingine, wakaiacha kazi hiyo na wakatubia kwa Allâh Mtukufu. *Alhamdulillâh!*

Nikapata barua zinazoeleza kuwa, kitabu hiki kimewakomoa wachawi, hasa wale wanaodai kuwa wao hutibu kwa Qur'âni na ilihali wao kwa hakika ni wachawi na wanamazingaombwe. Watu walipoisoma fasili isemayo *Alama za kumjua mchawi*, walikuwa wakiwajua mara tu wanapowaona. Twamshukuru Allâh mwanzo na mwisho.

Zikaja barua nyingine zikikosoa baadhi ya sehemu fulani katika kitabu. Kifua changu kikawa baridi na nikawaombea dua, nikazifwata nasaha

zao katika mambo mengi. Na bado nasubiri barua nyinginezo za aina hii; kwa sababu hilo ni katika "kusaidiana katika wema na uchamungu", na amali ya Mwanaadamu haikosi dosari. Ewe Mola, Muongoze anayetuongoza na Umuilimishe anayetuilimisha.

- ***Uzindushi*:**

Kwanza, kila nilichokiondoa katika chapa hii na ilihali kilikuwepo kwenye chapa zilizotangulia, itakuwa nimekibatilisha.

Pili, hesabu nilizozitaja katika chapa iliyopita, nimeziondoa na nimezirudi.

Tatu, katika siku za hivi karibuni, vimedhihiri vijitabu vidogo na vikubwa vikiwemo vyenye manufaa na ambavyo havina kitu, bali kuna ambavyo vimebeba sumu kali. Kwa mfano, katika baadhi ya vijitabu hivi, nimeona njia ya kumtibu aliyesihiriwa, mwandishi wake ameeleza: "Utaandika Aya kadha chini ya kitovu kisha umjamii mkeo, basi sihiri itafunguka, kisha utaifuta kabla ya kuingia chooni"!!

Ala! Kwani mwandishi huyu hajui kama kufanya hivyo ni kuitweza na kuidhalilisha Qur'âni? Nikamkalifisha mmoja katika wanafunzi wetu awasiliane na mwandishi na ambainishie hatari ya jambo lenyewe na kwamba haifai kufanya hivyo kwa vyovyote iwavyo. Naye akamuahidi kuwa atayaondoa maneno hayo. Lakini imepita zaidi ya mwaka na hakuna chochote alichofanya. Allâh Ndiye tunayemuomba msaada!

Basi ni juu ya kila Muislamu kutahadhari vitabu hivyo japo waandishi wake watadai kutotoka nje ya Qur'âni na Hadîth maadamu hawajahakiki.

Nne, nawanasihi mashababu wanaotibu, kuwa wakomee katika tiba za Sharia tu na wasibobee sana ili wasije wakaingia katika mipaka ya haramu; **"Kama mchungaji anayechunga kando ya mipaka (ya wengine), anaweza akaingia maeneo ya wengine."**

Tano, nimeambiwa kuwa baadhi ya wanaotibu, wanarahisisha katika kutibu wanawake, kama vile kumruhusu mwanamke aingie huku amejipodoa, au anasahilisha katika kutopatikana maharimu, hivyo anamtibu mwanamke bila maharimu au pamoja na kundi la wanawake. Basi ni juu ya anayetibu amche Mola wake, aihifadhi nafsi yake na amchunge Muumba wake.

Sita, nimeambiwa vilevile kuwa baadhi ya wanaotibu, wamefanya hii ndio kazi (ya kujipatia riziki), wanasharutisha malipo maalumu wakitoa dalili kwa Hadîth iliopokewa na Abû Sa‘îd ﵁ niliyoitaja katika kitabu hiki, pamoja na kuwa Hadîth iliyotajwa haina dalili katika hilo, ispokuwa ndani yake muna muamala kama huo, kwa ambavyo kijiji cha Mabedui walikataa kuwakirimu (Maswahaba); kwa ajili hiyo Abû Sa‘îd alikataa kuwazungua ela kwa kitu. Halafu, nao walimsharutisha Abû Sa‘îd mgonjwa apone kabisa, hawakumpa kitu ela baada ya yule mgonjwa kupona akawa kanakwamba amefunguliwa kamba. [Tazama: Bukhârî (2276), Muslim (2201), Tirmidhy (2063) na Ibnu Mâjah (2156)].

Saba, mgonjwa asidanganyike kwa mavazi na manjonjo, bali amtafute tabibu wa Qur’âni aliye mchamungu.

Nane, yamlazimu maharimu wa mwanamke asimuache aingie peke yake kwa tabibu hata kama tabibu huyo ni mchamungu kiasi gani; kwa sababu jambo hilo ni haramu halifai. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alikataza kuketi faragha na mwanamke ajinabi.

Mwisho; twapenda kutanabahisha kuwa upeo wa malengo yetu ni haki, makusudio yetu ni kubainisha, matarajio yetu ni Radhi za Allâh, njia yetu ni Qur’âni na Hadîth kama walivyofahamu Wanazuoni wema waliotangulia. Yeyote atakayekuta katika kitabu hiki kinachokhalifu nilioyataja, yamlazimu kutunasihi;

﴿وَاللهُ فِي عَوْنِ الْعَبْدِ مَا كَانَ الْعَبْدُ فِي عَوْنِ أَخِيهِ﴾.

“Allâh Yu katika kumsaidia mja maadamu mja huyo yu katika kumsaidia nduguye.”

Ewe Mola, Tuepushie dosari, Utusahilishie kufanya amali na Utuongoze njia ya amani. Umrehemu, Umpe amani na Umbarikie (Nabii) Muhammad, Aila yake, Maswahaba zake na wenye kuwafwata wao kwa wema.

Wakatabahu:
Wahîd bin 'Abdus-Salâm Bâlî.
Mansha-atu 'Abbâs 4/Shabani/1417Hijriyya.

بسم الله الرحمن الرحيم

KWA JINA LA ALLÂH MWENYE KUREHEMU WEMA NA WABAYA DUNIANI, MWENYE KUREHEMU WEMA WATUPU AKHERA

UTANGULIZI WA CHAPA YA KWANZA

إِنَّ الْحَمْدَ لِلهِ، نَحْمَدُهُ وَنَسْتَعِينُهُ، وَنَسْتَهْدِيهِ وَنَسْتَغْفِرُهُ، وَنَعُوذُ بِاللهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا وَمِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا، مَنْ يَهْدِهِ اللهُ فَلا مُضِلَّ لَهُ، وَمَنْ يُضْلِلْ فَلا هَادِيَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيكَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ، وَرَسُولُهُ.

Shukrani Anastahiki Allâh, twamhimidi, twamuomba msaada, twamuomba uongofu na twamuomba maghfira. Twajilinda kwa Allâh dhidi ya shari ya nafsi zetu na ubaya wa dhambi zetu. Anayeongozwa na Allâh hakuna wa kumpoteza, na anayepotezwa Naye, hakuna wa kumuongoza. Nashuhudia kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa ni Yeye Peke Yake, Hana mshirika, na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja Wake na ni Mtume Wake.

Ama baada ya haya; bila shaka maneno ya kweli kabisa ni Kitabu cha Allâh Mtukufu, bora ya njia, ni njia aliyopita Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم , na shari ya mambo ni yaliozuliwa, kila kilichozuliwa ni bid‘a (uzushi), kila bid‘a ni upotevu na kila upotevu ni motoni.

Maudhui ya sihiri (uchawi), ni miongoni mwa maudhui muhimu mno ambayo yapasa kwa Ulamaa wakabiliane nayo kwa utafiti, uchambuzi na uandishi. Kwa sababu ni jambo linalojiingiza lenyewe katika hali halisi katika jamii; kwani wafanyaji sihiri hutenda usiku na mchana katika kufisidi kwa mkabala wa vijishilingi wanavyovipata kwa

madhaifu wa kinafsi na waovu wa watu wenye chuki dhidi ya wenzao na wakifurahi huku wakiwaona wakipata taabu na wakiadhibiwa kutokana na athari za sihiri.

Ndiposa ikawa ni wajibu wa Ulamaa kuwabainishia watu hatari na madhara ya sihiri. Bali muhimu mno ni kuwapa tiba ya ki-Sharia ili wasiende kwa wachawi waovu[1] ili wawabatilishie sihiri walizofanyiwa, au wayatibu maradhi yao.

Sasa, naweka mikononi mwa wasomaji kitabu hiki "*as-Sârimul-Battâr Fit-Tasaddî Lis-Saharatil-Ashrâr*" (Upanga Mkali wa Kupambana na Wachawi Waovu) nilichowaahidi mwisho wa kitabu *Wiqâyatul-Insân, Minal-Jinni Wash-shaitân* (Kinga ya Mwanaadamu Dhidi ya Jini na shetani), kwa zaidi ya miaka minne. Hili ni zoezi dogo na jitihada ndogo, nimemkusudia shababu Muislamu ajifunze njia za ki-Sharia katika kubatilisha sihiri (uchawi), kuwatibu waliosihiriwa na kutibu hasadi (husuda) na kijicho ili watu wasiwahitajie wachawi na wanamazingaombwe wanaozibomoa Imani za watu na wakizifisidi ibada zao. Kitabu hiki, nimekigawa katika fasili nane:

- **FASILI YA KWANZA: (Taarifa ya sihiri).**

Nimezungumzia:
1. Sihiri, kilugha.
2. Sihiri kiistilahi.
3. Baadhi ya njia za wachawi wanazotumia kujikaribisha kwa shetani.

- **FASILI YA PILI: (Sihiri kwa mujibu wa Qur'âni na Hadîth).**

Nimezungumzia:
1. Dalili za Qur'âni na Hadîth juu ya kuwepo majini.
2. Dalili za Qur'âni na Hadîth juu ya kuwepo sihiri.
3. Maneno ya Ulamaa juu ya sihiri.

---

[1] Pengine utashangaa, kwani kuna wachawi wasiokuwa waovu? Hapana, lakini kusema *waovu*, ni kusisitiza sifa yao chafu.

- **FASILI YA TATU: (Vigawanyo vya sihiri).**

Nimezungumzia:

1. Vigawanyo vya sihiri kwa ar-Râzy.
2. Vigawanyo vya sihiri kwa ar-Râghib.
3. Uhakiki na uwazi wa vigawanyo vya sihiri.

- **FASILI YA NNE: (Mchawi anavyomleta jini)**

Katika fasili hii, nimezungumzia njia nane ambazo wachawi waovu wanazitumia kumleta jini, pamoja na kutoitaja njia yenyewe ili msomaji asije akaitumia.

- **FASILI YA TANO: (Hukumu ya sihiri katika Sharia ya Uislamu).**

Nimezungumzia:

1. Hukumu ya kujifunza sihiri katika Uislamu.
2. Hukumu ya mchawi katika Uislamu.
3. Hukumu ya mchawi wa *Ahlul-Kitâb* (Mayahudi na Manaswara).
4. Je, inafaa kuifungua sihiri kwa sihiri?
5. Tofauti baina ya sihiri, mwujiza na karama.

- **FASILI YA SITA: (Kuibatilisha sihiri).**

Nimezungumzia:

1. Sihiri ya kufarikisha: dalili zake, namna ya kuibatilisha na namna ya kuitibu.
2. Sihiri ya mapenzi: dalili zake, namna ya kuibatilisha na namna ya kuitibu.
3. Sihiri ya kuzuga: dalili zake, namna ya kuibatilisha na namna ya kuitibu.
4. Sihiri ya wazimu: dalili zake, namna ya kuibatilisha na namna ya kuitibu.
5. Sihiri ya upumbavu: dalili zake na namna ya kuitibu.
6. Sihiri ya sauti (kelele): dalili zake na namna ya kuitibu.
7. Sihiri ya magonjwa: dalili zake, na namna ya kuitibu.

8. Sihiri ya kutokwa damu (*istihâdha*)[1]: dalili zake, namna ya kuibatilisha na namna ya kuitibu.
9. Sihiri ya kuvunja ndoa: dalili zake, namna ya kuibatilisha na namna ya kuitibu.

- **FASILI YA SABA: (Tiba ya aliyefungwa asiweze kumjamii mkewe).**

Nimezungumzia:
1. Sampuli za kufungwa.
2. Kutibu kufungwa kwa tiba ya Qur'ân, Sunna na nyuradi za ki-Sharia.
3. Tofauti baina ya kufungwa na udhaifu wa nguvu za kiume.
4. Kutibu aina fulani za utasa.
5. Kinga ya maarusi (wanandoa) dhidi ya sihiri.
6. Namna ya kutibu kufungwa.

- **FASILI YA NANE: (Tiba ya kijicho).**

Nimezungumzia:
1. Dalili za Qur'âni na Sunnah juu ya athari ya kijicho.
2. Hakika ya kijicho.
3. Tiba ya kijicho.
4. Namna ya kutibu kijicho.

Namuomba Allâh Amnufaishe kwa kitabu hiki aliyekiandika, msomaji, na mchapishaji. Yeye Ndiye Mwenye kuachiwa hilo na ni Muweza juu yake. Nami namuomba ndugu atakayenufaika kwa kitabu hiki, asiache kuniombea dua akiwa mbali.

Nawatanabahisha kuwa, kila mnachokipata katika kitabu hiki ambacho kitakhalifu Qur'âni na Sunnah, basi muachane nacho na mufwate Qur'âni na Sunnah. Allâh Amrehemu yule atakayeona kosa akanifikishia iwapo nipo hai, au akalitengeneza iwapo nimekufa.

---

[1] *Istihâdha:* ni damu imtokayo mwanamke katika kipindi kisichokuwa cha hedhi.

Nami niko mbali na kila kilichokhalifu Qur'âni na Sunnah. Sikusudii ispokuwa kutengeneza kiasi ninachoweza, taufiqi yangu iko kwa Allâh, Kwake nimeegemea na Kwake narejea.

Wakatabahu mja fakiri kwa Allâh:
Wahîd bin 'Abdussalâm Bâlî.
Katika Raudha Tukufu ya Msikiti wa Mtume
14/Ramadhani/ 1411 Hijriyya.

FASILI YA KWANZA
TAARIFA YA SIHIRI (UCHAWI)

- Sihiri, kilugha.
- Sihiri kiistilahi ya Sharia.
- Baadhi ya njia za wachawi wanazotumia kujikaribisha kwa shetani.

FASILI YA KWANZA
TAARIFA YA SIHIRI (UCHAWI)

❖ ***Sihiri kilugha:***

* al-Laith amesema: "Sihiri ni amali inayokaribiwa kwayo shetani na kwa msaada wake."

* al-Azhary amesema: "Asili ya sihiri ni kukigeuza kitu katika hakika yake hadi sehemu nyingine." [*Tahdhîbul-Lughah* (4/290)].
* Ibnu Mandhwûr amesema: "Kana kwamba mchawi alipoonyesha batili katika sura ya kweli na akakisawirisha kitu kwa namna isiyo hakika, atakuwa amekisihiri kitu, yaani amekigeuza." [*Lisânul-'Arab* (4/348)].

* Shamir amepokea kutoka kwa Ibnu 'Âisha akisema: "Waarabu wameita sihiri kuwa ni sihiri; kwa sababu huondoa uzima hadi kwenye maradhi." [*Maqâyîsul-Lughah* (ukurasa wa 507)].

* Ibnu Fâris amesema kuhusiana na sihiri: "Watu (wa lugha) wamesema: ni kuidhihirisha batili katika sura ya haki." [*Maqâyîsul-Lughah* (س ح ر) na *al-Misbâh* (267)].

* Katika *al-Mu'jamul-Wasît* imeandikwa: "Sihiri ni kukidhihirisha kitu katika maonyesho yake mazuri ili ifitini (ivutie)." [*Mahîtulmahît* (399)].

❖ ***Sihiri katika istilahi ya Sharia*:**

Fakhruddîn ar-Râzy amesema: "Sihiri katika istilahi ya Sharia, imehusika na kila jambo ambalo sababu yake imefichika na linasawirisha kwa namna isiyo hakika yake, na huwa ikipitika kwa namna ya kuficha na kuhadaa." [*al-Misbâhul-Munîr* (268)].

* Ibnu Qudâma al-Maqdisy amesema: "(Sihiri ni) kifundo, zunguo na maneno yanayosemwa au kuandikwa, au afanye jambo litakaloathiri katika mwili wa aliyesihiriwa au moyoni mwake au akilini mwake bila ya kumshika. Nayo ina hakika, kuna yenye kuuwa, yenye kutia maradhi, inayomzuwia mwanamume asiweze kumjamii mkewe. Muna na inayomtenganisha mtu na mkewe na inayomchukiza mmojawapo kwa mwenzie, au kutia mapenzi baina ya wawili." [*al-Mughnî* (10/104)].

* Ibnul-Qayyim amesema: “(Sihiri ni) mchanganyo wa athari za mapepo wachafu na athari ya nguvu ya kimaumbile.” [*Zâdul-Ma‘âd* (4/126)].

❖ *Taarifa ya sihiri*:

Sihiri ni maafikiano baina ya mchawi na shetani juu ya kwamba mchawi atende baadhi ya mambo ambayo ni haramu au ya ushirikina katika mkabala wa shetani kumsaidia yeye na kumtii katika analolitaka.

❖ *Baadhi ya njia ambazo wachawi huzitumia kujikurubisha kwa shetani*:

Katika wachawi, muna ambaye huvaa Msahafu (Qur’âni) katika nyayo zake akiingia nao chooni. Muna wanaoandika Aya za Qur’âni kwa uchafu. Muna wanaoziandika Aya hizo kwa damu ya hedhi. Muna wanaoziandika Aya za Qur’âni chini ya unyayo. Muna wanaoandika *Sûratul-Fâtiha* kinyumenyume. Muna wanaoswali bila udhu. Muna wanaoketi na janaba muda wote. Muna wanaomchinjia shetani; hivyo huwa hawataji Jina la Allâh wanapochinja, na kisha humtupa mahala alipowaelekeza shetani.(1) [Tazama: *Wiqâyatul-insân* ukurasa wa 45]. Muna wanaoziomba nyota na wakizisujudia badala ya Allâh. Muna wanaowanajisi mama zao au binti zao. Muna wanaoandika talasimu kwa maneno yasio ya Kiarabu yenye maana ya kikafiri.

Hapa ndipo tunapoona kuwa jini hamsaidii mchawi wala hamtumikii ela kwa kubadilishana (*nipe nikupe!*), na mchawi kila anapokuwa ana ukafiri zaidi, shetani naye humtii zaidi na huharakisha kumtekelezea alitakalo. Mchawi anapokusuru kuyafanya alioamriwa na shetani katika mambo ya kikafiri, naye shetani hukataa kumhudumikia na anaasi amri yake.

Kwa hivyo, mchawi na shetani ni wendani waliokutana katika kumuasi Allâh.

---

(1) Ukiona mganga au *mwalimu* amechinja mbuzi au mnyama kisha akamtupa kama vile baharini, basi usiulize, hiyo ni amali ya kujikurubisha kwa shetani.

Unapoutazama uso wa mchawi, utadhihirikiwa na ukweli huu niliokwambia, utaona giza la ukafiri limetanda usoni mwake kanakwamba ni wingu jeusi.

Utakapomjua mchawi kwa ukaribu zaidi, utamkuta anaishi katika mateso ya kinafsi pamoja na mkewe na wanawe, bali pamoja na nafsi yake yeye mwenyewe. Hawezi kulala kwa umakinifu na moyo uliotulia, bali mara kwa mara huwa akifazaika usingizini; ongezea hapo, mashetani mara nyingi huwa wakiwaletea adha wanawe na mkewe na hutia ugomvi na utesi baina yao.

Allâh Mtukufu Amesadiki Aliposema:

﴿وَمَنْ أَعْرَضَ عَنْ ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنْكًا﴾.

"Atakayejiepusha na mawaidha Yangu, kwa yakini atapata maisha yenye dhiki …"[1] [20: 124].

*****

[1] Aya ikamalizikia: **"… na Siku ya Qiyama Tutamfufua hali ya kuwa kipofu."** Aya mbili mbele yake zikasema: **"Aseme: "Mola wangu! Mbona umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona?" (Allâh) Atamwambia: "Ndivyo hivyo; zilikufikia Aya Zetu, ukazisahau; vile vile leo unasahauliwa!"**

FASILI YA PILI
SIHIRI KWA MUJIBU WA QUR'ÂNI NA HADÎTH

- Dalili za Qur'âni na Hadîth juu ya kuwepo majini na mashetani.
- Dalili za Qur'âni na Hadîth juu ya kuwepo sihiri.
- Maneno ya Ulamaa kuhusu sihiri.

FASILI YA PILI
SIHIRI KWA MUJIBU WA QUR'ÂNI NA HADÎTH

❖ ***Dalili za kuwepo majini na mashetani.*** [Tazama: *Wiqâyatul-insân*].

Mafungamano ni ya nguvu baina ya jini na mchawi. Bali majini na mashetani ndio msingi na mhimili wa uchawi. Baadhi ya watu wamekanusha kuwepo majini na halafu wakakanusha kutokezea sihiri. Kwa hivyo nitaorodhesha dalili za kuwepo majini na mashetani kwa ufupi.

Kwanza, dalili za Qur'âni:

1. Allâh Amesema:

﴿وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ﴾

"(Wakumbushe) Tulipokuleteа kundi la majini (kuja kwako) kusikiliza Qur'âni." [46: 29].

2. Allâh Amesema:

﴿يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ وَالإِنْسِ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِنْكُمْ يَقُصُّونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِي وَيُنْذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَذَا﴾.

"(Siku ya Qiyama wataambiwa): enyi makundi ya majini na Wanaadamu! Je, Mitume hawakuwafikia miongoni mwenu kuwabainishia Aya Zangu na kuwaonyesha mkusanyo wa Siku yenu hii ya leo?" [6: 130].

3. Allâh Amesema:

﴿يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ وَالإِنْسِ إِنِ اسْتَطَعْتُمْ أَنْ تَنْفُذُوا مِنْ أَقْطَارِ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ فَانْفُذُوا لاَ تَنْفُذُونَ إِلاَّ بِسُلْطَانٍ﴾.

"Enyi jamii ya majini na watu! Kama mtaweza kupenya katika mbingu na ardhi, basi penyeni. Hamtapenya ela kwa nguvu (Zangu)." [55: 33].

4. Allâh Amesema:

﴿قُلْ أُوحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفَرٌ مِنَ الْجِنِّ فَقَالُوا إِنَّا سَمِعْنَا قُرْآنًا عَجَبًا﴾.

"Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikia (Qur'âni) likasema: "Hakika tumesikia Qur'âni ya

ajabu!” [72: 1].

5. Allâh Amesema:

“Kulikuwa na wanaume miongoni mwa Wanaadamu wakijikinga kwa wanaume miongoni mwa majini; kwa hivyo wakawazidishia madhambi.” [72: 6].

﴿وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِنَ الإِنْسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا﴾.

6. Allâh Amesema:

“Hakika shetani anataka kuwatilia uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kuwazuilia kumkumbuka Allâh na (kuwazuilia) kuswali. Basi je mtaacha (mabaya hayo)?” [5: 91].

﴿إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللهِ وَعَنِ الصَّلاَةِ فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ﴾.

7. Allâh Amesema:

“Enyi mlioamini! Msifuate nyayo za shetani; atakayefuata nyayo za shetani (atapotea); kwani yeye huamrisha machafu na maovu.” [24: 21].

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لاَ تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ وَمَنْ يَتَّبِعْ خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ﴾.

Dalili katika Qur’âni ni nyingi zinajulikana, ikutoshe kuwa katika Qur’âni muna Sura kamili inayozungumzia majini, bali ikutoshe kuwa neno *jinni* limetajwa katika Qur’âni mara 22, neno *majini* limetajwa mara saba, neno *shetani* limetajwa mara 68 na neno *mashetani* limetajwa mara saba. Na pia, ni kwamba Aya zilizotaja majini na mashetani ni nyingi.

Pili: dalili katika Hadîth:

1. ‘Abdullâh bin Mas‘ûd ﵁ amesimulia:

“Tulikuwa pamoja na Mtume صلى الله عليه وآله وسلم usiku mmoja. Mara tukamkosa, tukamtafuta katika

كُنَّا مَعَ رَسُولِ اللهِ ذَاتَ لَيْلَةٍ فَفَقَدْنَاهُ

majangwa na mabonde. Tukasema: "Ametekwa au ameuliwa!" Tukalala usiku mbaya waliowahi kulala watu. Kulipopambazuka, tukamuona akija akitokea upande wa Hirâ. Tukamwambia: "*Yâ Rasûlallâh*, tumekukosa na tumekutafuta wala hatukukupata, tukalala usiku mbaya waliowahi kulala watu." Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akasema: **"Nilijiwa na mwitaji wa majini, nikaenda naye nikawasomea Qur'âni."** Tukaenda naye akatuonyesha athari zao na athari za mioto yao. Wakamuomba akiba. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akawaambia: **"Nyinyi muna kila mfupa uliotajiwa Jina la Allâh juu yake utakaoangukia mikononi mwenu wenye nyama, na kila samadi ni chakula cha wanyama wenu."** Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akatwambia: **"Basi msitambe (msichambe) kwavyo, kwani ni vyakula vya wenzenu."** [Muslim (4/170)].

فَالْتَمَسْنَاهُ فِي الْأَوْدِيَةِ وَالشِّعَابِ. فَقُلْنَا: اسْتُطِيرَ أَوِ اغْتِيلَ. قَالَ: فَبِتْنَا بِشَرِّ لَيْلَةٍ بَاتَ بِهَا قَوْمٌ فَلَمَّا أَصْبَحْنَا إِذَا هُوَ جَاءٍ مِنْ قِبَلِ حِرَاءٍ. قَالَ: فَقُلْنَا يَا رَسُولَ اللهِ فَقَدْنَاكَ فَطَلَبْنَاكَ فَلَمْ نَجِدْكَ فَبِتْنَا بِشَرِّ لَيْلَةٍ بَاتَ بِهَا قَوْمٌ. فَقَالَ: ﴿**أَتَانِي دَاعِي الْجِنِّ فَذَهَبْتُ مَعَهُ فَقَرَأْتُ عَلَيْهِمُ الْقُرْآنَ**﴾. قَالَ: فَانْطَلَقَ بِنَا فَأَرَانَا آثَارَهُمْ وَآثَارَ نِيرَانِهِمْ وَسَأَلُوهُ الزَّادَ فَقَالَ: ﴿**لَكُمْ كُلُّ عَظْمٍ ذُكِرَ اسْمُ اللهِ عَلَيْهِ يَقَعُ فِي أَيْدِيكُمْ أَوْفَرَ مَا يَكُونُ لَحْمًا وَكُلُّ بَعْرَةٍ عَلَفٌ لِدَوَابِّكُمْ**﴾. فَقَالَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ﴿**فَلَا تَسْتَنْجُوا بِهِمَا فَإِنَّهُمَا طَعَامُ إِخْوَانِكُمْ**﴾.

2. Abû Sa'îd al-Khudry ﵁ amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم aliniambia:

"Nakuona wapenda mbuzi na jangwani. Basi utapokuwa katika mbuzi wako au jangwani kwako na ukaadhini kwa ajili ya Swala, inua sauti yako unapoadhini; kwani hatoisikia sauti ya

﴿**إِنِّي أَرَاكَ تُحِبُّ الغَنَمَ وَالبَادِيَةَ، فَإِذَا كُنْتَ فِي غَنَمِكَ، أَوْ بَادِيَتِكَ، فَأَذَّنْتَ بِالصَّلاَةِ فَارْفَعْ صَوْتَكَ بِالنِّدَاءِ، فَإِنَّهُ لاَ يَسْمَعُ**

mwadhini jini wala Mwanaadamu wala chochote kile ispokuwa kitamshuhudia Siku ya Qiyama.” [Mâlik (1/68), Bukhârî (6/346 *Fat-hi*), an-Nasâ-î (2/12) na Ibnu Mâjah (1/239)].

مَدَى صَوْتِ الْمُؤَذِّنِ، جِنٌّ وَلاَ إِنْسٌ وَلاَ شَيْءٌ، **إِلَّا شَهِدَ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ﴾**.

3. ‘Abdullâh bin ‘Abbâs رضي الله عنهما amesimulia:

“Mtume صلى الله عليه وآله وسلم aliondoka pamoja na Maswahaba zake wakielekea soko la ‘Ukâdh, na kulikuwa kumeshazuiwa baina ya mashetani na habari za mbinguni, na wamerushiwa vimondo, mashetani wakawarejelea jamaa zao, wakawauliza: “Munani?” Wakawambia: “Tumezuiwa baina yetu na habari za mbinguni na tukarushiwa vimondo.” Wakawaambia: “Hamkuzuiwa baina yenu na habari za mbinguni ela kuna kitu kimetokea. Safirini mashariki ya ardhi na magharibi yake na mutazame ni kipi hicho kilichozuia baina yenu na habari ya mbinguni.” Wakaondoka wale walioelekea upande wa Tihâma mpaka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم naye yupo Nakhla wakielekea katika soko la ‘Ukâdh, naye akiwaswalisha Maswahaba zake Swala ya alfajiri. Walipoisikia Qur’âni, waliisikiliza na wakasema: “Wallahi jambo hili ndilo lililozuia baina yenu na habari za mbinguni.”

انْطَلَقَ النَّبِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي طَائِفَةٍ مِنْ أَصْحَابِهِ عَامِدِينَ إِلَى سُوقِ عُكَاظٍ، وَقَدْ حِيلَ بَيْنَ الشَّيَاطِينِ وَبَيْنَ خَبَرِ السَّمَاءِ، وَأُرْسِلَتْ عَلَيْهِمُ الشُّهُبُ، فَرَجَعَتِ الشَّيَاطِينُ إِلَى قَوْمِهِمْ، فَقَالُوا: مَا لَكُمْ؟ فَقَالُوا: حِيلَ بَيْنَنَا وَبَيْنَ خَبَرِ السَّمَاءِ، وَأُرْسِلَتْ عَلَيْنَا الشُّهُبُ، قَالُوا: مَا حَالَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ خَبَرِ السَّمَاءِ إِلَّا شَيْءٌ حَدَثَ، فَاضْرِبُوا مَشَارِقَ الأَرْضِ وَمَغَارِبَهَا، فَانْظُرُوا مَا هَذَا الَّذِي حَالَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ خَبَرِ السَّمَاءِ، فَانْصَرَفَ أُولَئِكَ الَّذِينَ تَوَجَّهُوا نَحْوَ تِهَامَةَ إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَهُوَ بِنَخْلَةَ عَامِدِينَ إِلَى سُوقِ عُكَاظٍ، وَهُوَ يُصَلِّي بِأَصْحَابِهِ صَلاَةَ

Waliporejea kwa jamaa zao waliwaambia: "Enyi jamaa zetu, **"tumeisikia Qur'âni ya ajabu, inaongoza katika uongofu, kwa hivyo tumeiamini, wala hatutomshirikisha Mola wetu na yeyote."** [72: 1,2]. Allâh Akamteremshia Mtume Wake Aya hii: **"Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la __majini__ lilisikia (Qur'âni**)**…"**[1] [72: 1]. Na alifunuliwa kauli ya __majini__."

الفَجْرِ، فَلَمَّا سَمِعُوا القُرْآنَ اسْتَمَعُوا لَهُ، فَقَالُوا: هَذَا وَاللهِ الَّذِي حَالَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ خَبَرِ السَّمَاءِ، فَهُنَالِكَ حِينَ رَجَعُوا إِلَى قَوْمِهِمْ، وَقَالُوا: يَا قَوْمَنَا: ﴿**إِنَّا سَمِعْنَا قُرْآنًا عَجَبًا، يَهْدِي إِلَى الرُّشْدِ، فَآمَنَّا بِهِ وَلَنْ نُشْرِكَ بِرَبِّنَا أَحَدًا**﴾. [الجن: ٢]، فَأَنْزَلَ اللهُ عَلَى نَبِيِّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ﴿**قُلْ أُوحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفَرٌ مِنَ الجِنِّ**﴾. [الجن: ١] وَإِنَّمَا أُوحِيَ إِلَيْهِ قَوْلُ الجِنِّ.

4. 'Âisha رضي الله عنها amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

"Malaika wameumbwa kwa nuru, __majini__ wameumbwa kwa ulimi wa moto, na Adam ameumbwa namna mulivyosifiwa." [Ahmad (6/153,18), Muslim (18/123 *Nawawy*)].

﴿**خُلِقَتِ المَلَائِكَةُ مِنْ نُورٍ، وَخُلِقَ الجَانُّ مِنْ مَارِجٍ من نَارٍ، وَخُلِقَ آدَمُ مِمَّا وُصِفَ لَكُمْ**﴾.

5. __S__afiyyah binti __H__uyayyi رضي الله عنها amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

---

[1] Aya zote mbili zasema: **"Sema: "Imefunuliwa kwangu ya kuwa; kundi moja la majini lilisikiliza, na likasema: "Hakika tumeisikia Qur'âni ya ajabu! Inaongoza kwenye uongofu, kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha Mola wetu na yeyote."**

﴿إِنَّ الشَّيْطَانَ يَجْرِي مِنَ ابْنِ آدَمَ مَجْرَى الدَّمِ﴾.

"shetani hupita kwa Mwanaadamu mapitio ya damu." [Bukhârî (4/282 *Fat-hi*), Muslim (14/155 *Nawawy*)].

6. 'Abdullâh bin 'Umar رضي الله عنهما amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿إِذَا أَكَلَ أَحَدُكُمْ فَلْيَأْكُلْ بِيَمِينِهِ، وَإِذَا شَرِبَ فَلْيَشْرَبْ بِيَمِينِهِ، فَإِنَّ الشَّيْطَانَ يَأْكُلُ بِشِمَالِهِ، وَيَشْرَبُ بِشِمَالِهِ﴾.

"Anapokula mmoja wenu, ale kwa mkono wake wa kulia, na anapokunywa anywe kwa mkono wake wa kulia, hakika shetani anakula kwa mkono wake wa kushoto na anakunywa kwa mkono wake wa kushoto." [Muslim (13/191 *Nawawy*)].

7. Abû Huraira ﷺ amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿مَا مِنْ مَوْلُودٍ يُولَدُ إِلاَّ نَخَسَهُ الشَّيْطَانُ فَيَسْتَهِلُّ صَارِخاً مِنْ نَخْسَةِ الشَّيْطَانِ إِلاَّ ابْنُ مَرْيَمَ وَأُمُّهُ﴾.

"Yeyote anayezaliwa hudukuliwa na shetani, akapiga ukelele kutokana na mdukuo wa shetani, ispokuwa Mwana wa Maryam (Nabii Isa) na mama yake." [Bukhârî (8/212 *Fat-hi*) na Muslim (15/120 *Nawawy*)].

8. 'Abdullâh bin Mas'ûd ﷺ amesimulia: "Mbele ya Mtume صلى الله عليه وآله وسلم kulitajwa mtu aliyelala usiku mpaka akapambazukiwa. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akasema:

﴿ذَاكَ رَجُلٌ بَالَ الشَّيْطَانُ فِي أُذُنَيْهِ﴾.

"Huyo ni mtu ambaye, shetani amemkojolea masikioni mwake." [Bukhârî (3/28 *Fat-hi*) na Muslim (6/64 *Nawawy*)].

9. Abû Qatâda ﷺ amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿الرُّؤْيَا مِنَ اللهِ، وَالْحُلْمُ مِنَ الشَّيْطَانِ،

"Ndoto njema yatoka kwa Allâh, na njozi yatoka kwa shetani. Basi

﴿فَإِذَا رَأَى أَحَدُكُمْ شَيْئًا يَكْرَهُهُ فَلْيَنْفِثْ حِينَ يَسْتَيْقِظُ ثَلاَثَ مَرَّاتٍ، وَيَتَعَوَّذْ مِنْ شَرِّهَا، فَإِنَّهَا لاَ تَضُرُّهُ﴾.

atakayeona kitu kinachomchukiza, anapoamka ateme upande wake wa kushoto mara tatu na ajilinde dhidi yake (njozi hiyo); kwani haitamdhuru." [Bukhârî (12/283 *Fat-hi*) na Muslim (15/16 *Nawawy*)].

10. Abû Sa'îd al-Khudry ﵁ amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿إِذَا تَثَاءَبَ أَحَدُكُمْ فَلْيُمْسِكْ بِيَدِهِ عَلَى فِيهِ ؛ فَإِنَّ الشَّيْطَانَ يَدْخُلُ﴾.

"Mmoja wenu atakapoenda mwayo, azuwie kwa mkono wake kinywani mwake; kwani shetani huingia (asipoziba)." [Muslim (18/122 *Nawawy*)] na Dârimy (1/321)].

Hadîth katika mlango huu, zipo nyingi, lakini hizo zatosha kwa anayetafuta haki.

Hapa tunabainikiwa kwamba majini na mashetani, ni hakika wala hakuna shaka yoyote. Hakuna atakayeleta mjadala katika hilo ispokuwa mtu anidi anayeshindana na haki, anayefwata hawaa zake pasipo uongofu utokao kwa Allâh.[1]

*****

(1) Kwa anayetaka maudhui haya kwa upana zaidi, atazame kitabu *Wiqâyatul-insân, minaljinni wash-shaiṯân* (Kinga ya Mwanaadamu Dhidi ya Jini na shetani).

1. ***Kwanza:dalili ya Qur'âni Tukufu*:**

2. Allâh Amesema:

﴿وَاتَّبَعُوا مَا تَتْلُو الشَّيَاطِينُ عَلَى مُلْكِ سُلَيْمَانَ وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أُنْزِلَ عَلَى الْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ هَارُوتَ وَمَارُوتَ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولاَ إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلاَ تَكْفُرْ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ وَمَا هُمْ بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلاَّ بِإِذْنِ اللهِ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمْ وَلاَ يَنْفَعُهُمْ وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الآخِرَةِ مِنْ خَلاَقٍ وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْا بِهِ أَنْفُسَهُمْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ﴾.

"Wakayaandama yale waliyoyazua mashetani dhidi ya ufalme wa Sulaimân, Sulaimân hakukufuru, bali mashetani ndio waliokufuru wakiwafundisha watu uchawi, na wakiwafundisha yale yalioteremshwa kwa Malaika wawili; Haruta na Maruta (katika mji wa) Babili, walikuwa hawamfundishi yeyote mpaka wamwambie: "Sisi ni mtihani, kwa hivyo usikufuru." Wakawa wakijifunza kwa Malaika hao mambo ya kumfarakanisha mtu na mkewe, wala hawakuweza kumdhuru yeyote kwa uchawi huo ela kwa Idhini ya Allâh, walikuwa wakijifunza yanayowadhuru wala hayawanufaishi. Kwa hakika walijua kuwa anayechagua hili, Akhira hana fungu (la kuingia Peponi), ubaya mkubwa waliouzia nafsi zao lau wangalikuwa wakijua."[(1)] [2: 102].

3.

﴿قَالَ مُوسَى أَتَقُولُونَ لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَكُمْ أَسِحْرٌ هَذَا وَلاَ يُفْلِحُ السَّاحِرُونَ﴾.

"Mûsâ akasema: "Mnasema (hivi) juu ya haki ilipowajia? Huu ni <u>uchawi</u>? Na <u>wachawi</u> hawafaulu." [10: 77].

[(1)] Aya hii tumeifafanua kwa upana katika: *Ufunguo Wa Imani Na Utamu Wa Qur'âni*.

4.

“Walipotupa, Mûsâ alisema: “Mliyoleta ni uchawi; Allâh sasa hivi Ataubatilisha. Hakika Allâh Hastawishi vitendo vya waharibifu. Allâh Ataithubutisha haki kwa Maneno Yake, ingawa watachukia (hao) wabaya.” [10: 81,82].

﴿فَلَمَّا أَلْقَوْا قَالَ مُوسَى مَا جِئْتُمْ بِهِ السِّحْرُ إِنَّ اللهَ سَيُبْطِلُهُ إِنَّ اللهَ لاَ يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ. وَيُحِقُّ اللهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ﴾.

5.

“Mûsâ akaona hofu katika nafsi yake. Tukamwambia: “Usiogope! Hakika wewe ndiwe utakayekuwa mwenye kushinda. Kitoe kilicho katika mkono wako wa kulia: kitavimeza walivyovitengeneza. Wao wametengeneza hila za uchawi tu, mchawi hafaulu popote afikapo.” [20: 67-69].

﴿فَأَوْجَسَ فِي نَفْسِهِ خِيفَةً مُوسَى. قُلْنَا لاَ تَخَفْ إِنَّكَ أَنْتَ الأَعْلَى. وَأَلْقِ مَا فِي يَمِينِكَ تَلْقَفْ مَا صَنَعُوا إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سَاحِرٍ وَلاَ يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَى﴾.

6.

“Tukampelekea Mûsâ Wahyi ya kwamba: “Tupa fimbo yako.” Mara ikavimeza vyote vile walivyovibuni (wale wachawi). Ukweli ukasimama na yakaharibika waliyokuwa wakiyatenda. Kwa hivyo walishindwa hapo, na wakawa wenye kudhalilika. Wachawi wakapinduliwa (wakapinduka) wanasujudu. Wakasema: “Tumemwamini Mola wa viumbe vyote. Mola wa Mûsâ na Haruni.”

﴿وَأَوْحَيْنَا إِلَى مُوسَى أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ. فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ. فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَاغِرِينَ. وَأُلْقِيَ السَّحَرَةُ سَاجِدِينَ. قَالُوا آمَنَّا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ. رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ﴾.

[7: 117-122].

7.

"Sema: "Najilinda kwa Mola wa viumbe vyote. Dhidi ya shari ya Alivyoviumba; shari ya giza la usiku liingiapo; shari ya wale wanaopuliza mafundoni na dhidi ya shari ya hasidi anapohusudu." [113: 1-5].

﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ. مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ. وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ. وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ. وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ﴾.

Imâm Qurtuby amefafanua: **"Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni,"** yaani: wale wachawi wanawake waliokuwa wakivuvia vifundo vya uzi wakati wanapovisomea." [*Tafsîrul-Qurtuby:* (20: 257].

al-Hâfidha Ibnu Kathîr amesema: **"Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni,"** Mujâhid, 'Ikrima al-Hasan Qatâda na adh-Dhahhâk wamesema: "Yaani: ni wachawi." [*Tafsîr Ibnu Kathîr* (4: 573)].

Ibnu Jarîr at-Tabary amesema: "Yaani dhidi ya shari ya wachawi wanawake waliokuwa wakivuvia katika vifundo vya uzi wakati wavisomeapo. al-Qâsimy amesema: "Na kwa kauli hiyo watu wa taawili (tafsiri) ndivyo walivyosema." [*Tafsîrul-Qâsimy* (10: 302)].

Aya zilizotaja wachawi na uchawi, ni nyingi na ni mashuhuri hata kwa mwenye ujuzi mchache katika Uislamu.

2. Pili:dalili za Hadîth:

1.

'Âisha رضي الله عنها amesimulia: "Mtu mmoja katika kabila la Banî Zuraiq anayeitwa Labîd bin al-A'sam, alimsihiri Mtume صلى الله عليه وآله وسلم, hata Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akawa akidhani kuwa amefanya jambo wala hakufanya.

عَنْ عَائِشَةَ، رَضِيَ اللهُ عَنْهَا قَالَتْ: سَحَرَ رَسُولَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَجُلٌ مِنْ بَنِي زُرَيْقٍ، يُقَالُ لَهُ لَبِيدُ بْنُ الأَعْصَمِ، حَتَّى كَانَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ

يُخَيَّلُ إِلَيْهِ أَنَّهُ كَانَ يَفْعَلُ الشَّيْءَ وَمَا فَعَلَهُ، حَتَّىٰ إِذَا كَانَ ذَاتَ يَوْمٍ أَوْ ذَاتَ لَيْلَةٍ وَهُوَ عِنْدِي، لَكِنَّهُ دَعَا وَدَعَا، ثُمَّ قَالَ: **﴿يَا عَائِشَةُ، أَشَعَرْتِ أَنَّ اللهَ أَفْتَانِي فِيمَا اسْتَفْتَيْتُهُ فِيهِ، أَتَانِي رَجُلَانِ، فَقَعَدَ أَحَدُهُمَا عِنْدَ رَأْسِي، وَالآخَرُ عِنْدَ رِجْلَيَّ، فَقَالَ أَحَدُهُمَا لِصَاحِبِهِ: مَا وَجَعُ الرَّجُلِ؟ فَقَالَ: مَطْبُوبٌ، قَالَ: مَنْ طَبَّهُ؟ قَالَ: لَبِيدُ بْنُ الأَعْصَمِ، قَالَ: فِي أَيِّ شَيْءٍ؟ قَالَ: فِي مُشْطٍ وَمُشَاطَةٍ، وَجُفِّ طَلْعِ نَخْلَةٍ ذَكَرٍ. قَالَ: وَأَيْنَ هُوَ؟ قَالَ: فِي بِئْرِ ذَرْوَانَ﴾**. فَأَتَاهَا رَسُولُ اللهِ صَلَّىٰ اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي نَاسٍ مِنْ أَصْحَابِهِ، فَجَاءَ فَقَالَ: **﴿يَا عَائِشَةُ، كَأَنَّ مَاءَهَا نُقَاعَةُ الحِنَّاءِ، أَوْ كَأَنَّ رُءُوسَ نَخْلِهَا رُءُوسُ الشَّيَاطِينِ﴾**. قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللهِ: أَفَلَا اسْتَخْرَجْتَهُ؟ قَالَ: «**قَدْ عَافَانِي اللهُ، فَكَرِهْتُ أَنْ أُثَوِّرَ عَلَى النَّاسِ فِيهِ شَرًّا**». فَأَمَرَ بِهَا فَدُفِنَتْ.

Hata ulipokuwa mchana – au usiku mmoja – naye yupo kwangu, akaita na akaita, kisha akanambia: **“Ee ‘Âisha, wajua kuwa Allâh Amenijibu swali nililomwuliza? Wamenijia watu wawili, mmoja akaketi kichwani kwangu na mwingine miguuni mwangu. Mmojawapo akamwuliza mwenziwe: “Nini ugonjwa wa mtu huyu?” Akamjibu: “Amesihiriwa.” Akamwuliza: “Ni nani aliyemsihiri?” Akamjibu: “Ni Labîd bin al-A’sam.” Akamwuliza: “Katika kitu gani?” Akamjibu: “Katika kichana na nywele zinazodondoka (ndevuni na kichwani) na gamba la karara la mtende.” Akamwuliza: “Liko wapi?” Akamjibu: “Katika kisima cha Dharwân.”** Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akakiendea kisima hicho pamoja na watu katika Maswahaba zake. Akaja, akasema: **“Ee ‘Âisha, maji yake ni kama mchemsho wa hina, na vichwa vya mitende yake ni kama vichwa vya nyoka.”** Nikamwambia: “*Yâ Rasûlallâh,* si ungaliutoa!” Akasema: **“Allâh Ameniafu (Ameniponya), nikachukia kueneza shari kwa watu.”** Akaamuru (sihiri) ikazikwa.” [Bukhârî (10/222 *Fat-hi*) na Muslim (14/174 katika *Kitâbus-Salâm, Bâbus-Sihri*)].

Maana ya Hadîth:
Mayahudi – Allâh Awalaani – waliafikiana na Labîd bin al-A'sam, naye ni katika wachawi wakubwa wa Kiyahudi, amfanyie sihiri Mtume صلى الله عليه وآله وسلم na wampe dinari tatu. Na kweli yule muovu akafanya sihiri juu ya nywele chache za Mtume صلى الله عليه وآله وسلم – yasemekana kuwa alizipata kwa kijakazi aliyekuwa akienda katika nyumba za Mtume صلى الله عليه وآله وسلم - na akazifungia sihiri na akaiweka katika kisima cha Dharwân.

Dhahiri inavyoonyesha kutokana na kukusanya isnadi za Hadîth hii, ni kuwa sihiri hii ilikuwa ni aina ya kumfunga mtu asiweze kumjamii mkewe. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akawa akidhani kuwa anaweza kumjamii mmojawapo katika wakeze. Anapomkaribia huwa hawezi kufanya hivyo. Lakini uchawi huu haukugusa akili yake wala tabia yake, ulikuwa umekomea hapo tu tulipotaja.

Na pana ikhtilafu katika muda wa sihiri hii. Kumesemwa ni siku arubaini, na pia kumesemwa vinginevyo. Allâh Ndiye Anayejua. Kisha Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akamuomba Mola wake na akawa anasisitiza katika dua. Allâh Akaijibu dua yake, Akawateremsha Malaika wawili. Mmoja akaketi kichwani mwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم na mwingine miguuni mwake. Mmojawapo akamwuliza mwenziwe: "Anani?" Akamjibu: "Amesihiriwa." Akamwuliza: "Ni nani aliyemsihiri?" Akamjibu: "Ni Labîd bin al-A'sam" ambaye ni Myahudi. Kisha akabainisha kuwa alimsihiri katika kichana na nywele zinazodondoka (katika kichwa na ndevu za) Mtume صلى الله عليه وآله وسلم na akaweka katika gamba la karara la mtende-dume ili sihiri iwe na nguvu na athari zaidi, halafu akazika chini ya mwamba katika kisima cha Dharwân. Wale Malaika walipomaliza kuibainisha hali ya Mtume صلى الله عليه وآله وسلم. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم aliamuru sihiri itolewe na ikazikwa. Riwaya nyingine imesema: "Akaichoma." Na kutokana na ukusanyaji wa isnadi za Hadîth hii, inadhihirika kuwa Mayahudi walimfanyia Mtume صلى الله عليه وآله وسلم sihiri kali mno, lengo lao lilikuwa ni kumuuwa; na katika sihiri muna inayouwa kama inavyojulikana, lakini Allâh Akamhifadhi kutokana na vitimbi vyao. Akamkhafifishia katika aina nyepesi ya sihiri; nayo ni kufungwa.

- ***Shaka na jawabu yake*:**

al-Mâziry رحمه الله amesema: "Hadîth hii imepingwa na watu wa bid'a (uzushi) kwa kuwa (eti) inaangusha daraja ya Utume na inaitilia shaka, na kuijuzisha, huondoa uaminifu katika Sharia; wakasema: "Pengine huenda wakati huo akadhania kuwa Jibrîl عليه السلام anamjia na kumbe hakuna Jibrîl, na kwamba ameletewa Wahyi ilihali hakuletewa."

Akajibu: "Hili walilosema ni ubatilifu moja kwa moja. Kwa sababu dalili ya Utume – nao ni mwujiza – umeonyesha ukweli wake katika anachokifikisha kutoka kwa Allâh na kuhifadhika kwake Mtume صلى الله عليه وآله وسلم ndani yake, na kujuzisha kilicho na dalili kinyume chake ni batili." [*Zâdul-Muslim* (4/221)].

Abul-Jakany al-Yûsufy رحمه الله amesema: "Ama Mtume صلى الله عليه وآله وسلم kupatwa na ugonjwa kwa sababu ya sihiri, hilo halipelekei dosari katika daraja ya Utume; kwa sababu ugonjwa usio na kasoro duniani huwa ukiwapata Manabii na huzidisha daraja zao Akhira. Kwa hivyo wakati huo atakapodhania – kwa sababu ya ugonjwa wa sihiri – kuwa yuwafanya jambo katika mambo ya kidunia na ilihali hakulifanya, kisha hali hiyo ikamwondokea kabisa kwa sababu ya Allâh kumjulisha mahala pa sihiri, naye kuitoa mahala pake na kuizika; basi hapana nuksani wala dosari itakayogusa Utume kutokana na haya yote; kwa sababu ni ugonjwa kama magonjwa mengine.

Haikumwathiri katika akili yake, bali ni nje ya mwili wake tu kama vile machoni mwake alipodhania kuwa mara huwa amefanya kitu kwa kumjamii mkewe naye hakufanya, na jambo hili katika kipindi cha ugonjwa, halidhuru."

Akasema: "Ajabu ni kwa anayedhania hili lililotokea kwa sababu ya ugonjwa uliosababishwa na sihiri kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم kuwa ni lenye kutia kasoro katika Utume wake pamoja na kuwa imeelezwa wazi katika Qur'âni katika kisa cha Nabii Musa pamoja na wachawi wa Firauni, alipodhania – kwa sababu ya sihiri yao – kuwa fimbo zao zinatembea. Allâh Akamthibitisha kama Aya ilivyoeleza:

﴿قُلْنَا لاَ تَخَفْ إِنَّكَ أَنْتَ الأَعْلَى. وَأَلْقِ مَا فِي يَمِينِكَ تَلْقَفْ مَا صَنَعُوا إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سَاحِرٍ وَلاَ يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَى. فَأُلْقِيَ السَّحَرَةُ سُجَّدًا قَالُوا آمَنَّا بِرَبِّ هَارُونَ وَمُوسَى﴾.

"Tukamwambia: 'Usiogope! Hakika wewe ndiwe utakayekuwa mwenye kushinda. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia: kitavimeza walivyovitengeneza. Hakika wao wametengeneza hila za uchawi tu, wala mchawi hafaulu (hafuzu) popote afikapo. Basi wachawi wakaangushwa (wakapinduliwa chini) wanasujudu, na kusema: "Tumemuamini Mola wa Haruni na Musa." [20: 68-70].

Wala hakuna yeyote mwenye ilimu wala mwenye akili razini aliyesema kuwa vile Nabii Musa kudhania kuwa fimbo zao zinatembea ni jambo lenye kutia dosari katika Utume wake. Bali jambo kama hili kutokezea kwa Manabii عليهم الصلاة والسلام huwazidishia nguvu ya Imani; kwa sababu Allâh Anawanusuru dhidi ya maadui wao, Anawafanyia miujiza inayoshinda, Anawakhizi wachawi na makafiri na Anajaalia mwisho mwema ni kwa wachamungu kama ilivyobainishwa katika Aya za Qur'âni." [*Zâdul-Muslim* (4/22)].

2.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ﴿اجْتَنِبُوا السَّبْعَ الْمُوبِقَاتِ﴾. قَالُوا: يَا رَسُولَ اللهِ وَمَا هُنَّ؟ قَالَ: ﴿الشِّرْكُ بِاللهِ، وَالسِّحْرُ، وَقَتْلُ النَّفْسِ الَّتِي حَرَّمَ اللهُ إِلَّا بِالْحَقِّ، وَأَكْلُ الرِّبَا، وَأَكْلُ مَالِ الْيَتِيمِ، وَالتَّوَلِّي

Abû Huraira رضي الله عنه amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema: **"Jiepusheni mambo saba yenye kuangamiza."** (Maswahaba) wakauliza: "*Yâ Rasûlallâh,*, ni yepi hayo?" Akawajibu: **"Ni kumshirikisha Allâh, <u>sihiri</u> (<u>uchawi</u>), kuuwa nafsi Aliyoiharamisha Allâh ela kwa haki, kula riba, kula mali ya yatima, kukimbia siku ya Vita (Jihâd) na kuwasingizia uzinifu wanawake waliotakasika walio**

Waumini wasiojua (maovu).” [Bukhârî (5/393 *Fat-hi*) na Muslim (2/83 *Nawawy*)].

يَوْمَ الزَّحْفِ، وَقَذْفُ الْمُحْصَنَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ الغَافِلاَتِ﴾.

- ***Ushahidi*:**

Ushahidi katika Hadîth hii, ni kuwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم ametuamuru kujiepusha na sihiri, na akatubainishia kuwa sihiri ni katika madhambi makubwa yanayoangamiza. Hili linatujulisha kwamba sihiri ni jambo la hakika wala si ngano za uwongo.

3. ‘Abdullâh bin ‘Abbâs رضي الله عنهما amesimulia: “Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

“Atakayejifunza ilimu katika unajimu, ameshajifunza sehemu katika sihiri, azidishe katika sihiri kile anachozidisha katika unajimu.” [Abû Dâwûd (3905), *Ibnu Mâjah* (3726)].

﴿مَنِ اقْتَبَسَ عِلْمًا مِنَ النُّجُومِ، اقْتَبَسَ شُعْبَةً مِنَ السِّحْرِ زَادَ مَا زَادَ﴾.

- ***Ushahidi*:**

Ushahidi katika Hadîth hii ni kuwa, Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amebainisha mojawapo ya njia inayopelekea kujifunza sihiri, ili Waislamu wajihadhari nayo; na hii ni dalili kuwa sihiri ni ilimu ya uhakika inayofunzwa. Na pia linalojulisha hilo ni Kauli ya Allâh:

“Wakajifunza kwao ambayo kwa mambo hayo waliweza kumfarikisha mtu na mkewe (na mengineyo).”

﴿فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ﴾.

Imebainika kuwa sihiri ni ilimu kama ilimu nyinginezo, ina misingi yake. Aya na Hadîth zipo katika mstari wa kushutumu kujifunza sihiri.

4. ‘Imrân bin Husain رضي الله عنه amesimulia: “Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

“Si katika sisi anayebashiri au kubashiriwa mabaya, au

﴿لَيْسَ مِنَّا مَنْ تَطَيَّرَ أَوْ تُطُيِّرَ لَهُ، أَوْ تَكَهَّنَ

anayefanya ukuhani au anayefanyiziwa ukuhani, au akafanya <u>sihiri</u> au akafanyiziwa. Na atakayemwendea kuhani akamsadiki katika anayosema, basi ameshakufuru ambayo Allâh Alimteremshia Mu<u>h</u>ammad.” [*Bazzâr*. al-Haithamy amesema katika kitabu chake *al-Majma’* (5/20): “Wapokezi wa <u>H</u>adîth hii ni *<u>S</u>a<u>h</u>î<u>h</u>*.” Na al-Mundhiry amesema katika *at-Targhîb* (4/52): “Isnadi yake ni *jayyid.*”]

أَوْ تُكُهِّنَ لَهُ، أَوْ سَحَرَ أَوْ سُحِرَ لَهُ، وَمَنْ أَتَى كَاهِنًا فَصَدَّقَهُ فِيمَا يَقُولُ، فَقَدْ كَفَرَ بِمَا أَنْزَلَ اللهُ عَلَى مُحمدٍ﴾.

- ***Ushahidi*:**

Ushahidi ni kuwa, Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amekataza sihiri na kumwendea mchawi. Na Mtume صلى الله عليه وآله وسلم hawezi kukataza ispokuwa jambo linalokuwepo na lenye uhakika.

5. Abû Mûsâ al-Ash‘ary ﷺ amesimulia: “Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

“Hatoingia Peponi anayedumu kunywa pombe, wala mwenye kuamini <u>sihiri</u>, wala mwenye kukata undugu.” [*Ibnu <u>H</u>ibbân*].

﴿لاَ يَدْخُلُ الجَنَّةَ مُدْمِنُ خَمْرٍ وَلا مُؤْمِنٌ بِسِحْرٍ، وَلا قَاطِعِ رَحِمٍ﴾.

- ***Ushahidi*:**

Ushahidi ni kuwa, Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amekataza kuitakidi kuwa sihiri huathiri kwa dhati yake (kwa nguvu zake); bali yapasa kwa Muislamu kuitakidi kuwa sihiri au jambo lingine haliathiri ela kwa Matakwa ya Allâh. **“Wala hawakuwa wenye kumdhuru yeyote kwa hayo ela kwa Idhini ya Allâh.”**

6. ‘Abdullâh bin Mas‘ûd ﷺ amesema: “Atakayemwendea mpiga ramli au <u>mchawi</u> au kuhani, akamwuliza na akamsadikisha katika anayosema, basi ameshakufuru aliyoteremshiwa Mu<u>h</u>ammad.” [Bazzâr. <u>H</u>adîth hii isnadi yake ni *jayyid*, (*at-Targhîb*)].

❖ ***Tatu: maneno ya Ulamaa*:**

1. al-Khattâby رحمه الله amesema: “Baadhi ya watu wamekanusha kuwepo sihiri na wamebatilisha uhakika wake. Jawabu ni kwamba, sihiri ni jambo limethubutu na ni hakika inayopatikana. Kila umma miongoni mwa Waarabu, Waajemi, Wahindi na baadhi ya Mafursi, wameafikiana kuwepo kwake. Na hawa ndio watu bora zaidi ulimwenguni na wenye ujuzi zaidi na hekima. Allâh Amesema**: “… wakiwafundisha watu uchawi”.** Na Akaamuru kujikinga kwayo, Akasema: **“… (na najikinga) Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni.”** Na pia kumepokewa Hadîth nyingi kuhusiana na jambo hilo, atakayepinga atakuwa anapinga jambo lionekanalo. Na Fuqahâ (Wanazuoni wa Sharia) wameeka tanzu nyingi za adhabu zinazomlazimu mchawi. Basi jambo ambalo halina asili haliwezi kufikia kiwango hiki cha umaarufu na maelezo marefu. Kukana kuwepo sihiri ni ujahili, na kumrudi anayeukana ni upuuzi na ufidhuli.” [*Sharhus-Sunnah* (12/188)].
2. Imâm Qurtuby amesema: “Ahlus-Sunnah wamesema kwamba sihiri ni jambo lipo na lina hakika. Mu’tazila na Abû Is-hâq al-Istarâbâdy katika wafuasi wa (Imâm) Shâfi wamesema kwamba sihiri haina hakika, bali ni kuzuga, kusawiri na kutia shaka kwa jambo fulani ambalo liko kinyume na lilivyo. Na ni sehemu katika purukushani na mazingaombwe. Allâh Amesema: **“…zikaonekana mbele yake (Musa) kwa uchawi wao, zinakwenda mbio.”** [20: 66]. Wala Hakusema: “Zinakwenda kwa uhakika.” Lakini Amesema: **“… zikaonekana mbele yake (Musa).” Na pia Akasema: “… waliyazuga macho ya watu.”** [7: 116].

Akasema: “Na hili halina hoja ndani yake, kwa sababu sisi hatupingi kuzuga na mengineyo ni katika jumla ya sihiri; lakini nyuma yake yamethubutu mambo yaliojuzishwa na akili na masikio yakapokea. Katika hayo, ni yale yaliokuja katika Aya hii katika kutaja sihiri na kujifunza. Lau kama lisingalikuwa na hakika, isingaliwezekana kujifunza, wala Allâh Asingelieleza kuwa wao wanafundisha watu; ikajulisha kuwa ni hakika.

Na Kauli Yake katika kisa cha wachawi wa Firauni: **“… wakaleta uchawi mkubwa.”** [7: 116], na *Sûratul-Falaq* pamoja na itifaki ya

wafasiri wa Qur'âni kwamba sababu ya kuteremka kwake, ni sihiri ya Labîd bin al-A'sam, Hadîth hiyo ni miongoni mwa zilizotajwa na Imâm Bukhârî, Imâm Muslim na wengineo kutoka kwa 'Âisha رضي الله عنها , amesema: "Alimsihiri Mtume صلى الله عليه وآله وسلم Yahudi mmoja katika Banî Zuraiq anayeitwa Labîd bin al-A'sam …" mpaka mwisho wa Hadîth (kama ilivyotangulia). Hadîth hiyo imeeleza kuwa, Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alipoifungua sihiri alisema: **"Allâh Ameniponya."** Na ponyo huwa ni kwa kuondoka ugonjwa; kwa hivyo ikajulisha kuwa sihiri ni kweli na ni hakika; ni jambo lililokatikiwa kwa kuelezwa na Allâh na Mtume Wake juu ya kuwepo kwake na kutokea. Na juu ya msimamo huu, wameafikiana wenye mamlaka na satwa ambao ijimai yafungamana kwao. Wala hawazingatiwi makapi wa ki-Mu'tazila na kuwakhalifu kwao wenye haki." Akasema: "Sihiri imeenea tangu zama zilizopita na watu wameizungumzia (sana). Wala hakuna yeyote katika Maswahaba wala tabiina aliyejitokeza kuipinga asili yake." [*Tafsîrul-Qurtuby* (2: 46)].

3. al-Mâziry amesema: "Sihiri ni jambo lenye ithbati na lenye uhakika kama mambo mengine, na ina athari kwa aliyesihiriwa, kinyume na anayedai kuwa haina hakika na kwamba kinachotendeka ni taswira tu zilizo batilifu zisizo na hakika. Hayo aliyosema ni batili, kwa sababu Allâh Ameitaja katika Kitabu Chake Kitukufu, na kwamba sihiri hufunzwa na ni miongoni mwa mambo yanayokufurisha na ni katika yanayofarikisha baina ya mtu na mkewe. Katika ile Hadîth ya kusihiriwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم imeeleza kuwa ni vitu vilivyozikwa na vikatolewa; na yote haya ni mambo ambayo hayawezi kuwa katika jambo lisilo na uhakika, na watu watajifunza vipi jambo lisilo na uhakika?"

Amesema: "Si ajabu akilini Allâh Abadilishe ada wakati wa kutamka maneno yaliobuniwa au kutengeneza vitu au kuchanganya nguvu (za vitu) katika mpango asioufahamu ela yule mchawi.

"Mwenye kutazama vitu vyenye kuuwa kama vile sumu na vyenye kutia maradhi kama vile dawa moto, na vyenye kutia siha kama vile dawa zinazouwa vijasumu, hatostaajabu akilini mwake huyu mchawi naye

awe na ujuzi wa nguvu zinazouwa au maneno yanayoangamiza au apelekee mtafaruku." [*Zâdul-Muslim* (4/225)].

4. Imâm Nawawy رحمه الله amesema: "Usahihi ni kuwa, sihiri ina hakika, na kwa kauli hiyo ndio Jumhuri (ya Ulamaa) wamekatikiwa na watu wote wameshika hapo; Qur'âni na Hadîth *Sahîh* zilizo mashuhuri zinaonyesha jambo hilo." [Nimenakili kutoka *Fat-hul-Bârî* (10:222)].

5. Ibnu Qudâma رحمه الله amesema: "Sihiri ina hakika; kuna inayouwa, inayotia maradhi, inayomnyang`anya mtu mkewe ikamzuia kumjamii na kuna inayomfarikisha mtu na mkewe."

Akasema: "Ni mashuhuri miongoni mwa watu kuwepo mwanamume aliyefungwa asiweze kumjamii mkewe, na inapofunguliwa sihiri aliyofungwa akawa anaweza kumjamii baada ya kuwa alishindwa kabisa. Jambo hilo likawa haliwezi tena kupingika." Akasema: "Kumepokewa habari za wachawi ambazo haiwezekani watu kuafikiana juu ya uwongo huo." [*al-Mughnî:* 19/106].

Katika *al-Kâfî* amesema: "Sihiri ni zunguo na mafundo yanayoathiri moyoni na katika viwiliwili; hutia maradhi, huuwa na hufarikisha baina ya mtu na mkewe. Allâh Amesema: **"Wakajifunza kwao ambayo kwa mambo hayo waliweza kumfarikisha mtu na mkewe (na mengineyo)."** Na pia Akasema: **"Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni."** Yaani wachawi wanaofunga mafundo katika sihiri zao na wakivuvia. Lau kama sihiri isingalikuwa na hakika, Allâh Asingaliamrisha kujikinga dhidi yake." [*Fat-hul-Majîd* (314)].

6. Ibnul-Qayyim amesema katika *Badâi'ul-Fawâid*: **"**Kauli Yake Allâh: **"Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni,"** na Hadîth ya 'Âisha رضي الله عنها zimetujulisha juu ya kuathiri sihiri, na kwamba ina uhakika." [Nimenakili kutoka *Fat-hul-Majîd* (315) iliyotiwa taaliki (maelezo) na al-Arnaut. *Badâi'ul-Fawâid* (2/227)].

7. Abul-'Izzi al-Hanafy amesema: "Ulamaa wamekhitilafiana katika uhakika wa sihiri na aina zake. Lakini wengi wanasema: "(Sihiri) huenda ikaathiri katika kufa kwa aliyesihiriwa na ugonjwa wake pasipo yeye kufikwa na jambo la dhahiri". [*Sharhul-'Aqîdatit-Tahâwiyyah*: 505].

FASILI YA TATU
VIGAWANYO VYA SIHIRI

- ❖ Vigawanyo vya sihiri kwa ar-Râzy.
- ❖ Vigawanyo vya sihiri kwa ar-Râghib.
- ❖ Uhakiki na uwazi wa vigawanyo vya sihiri.

FASILI YA TATU
VIGAWANYO VYA SIHIRI

- ***Kuigawanya sihiri:***

Abû ‘Abdillâhi ar-Râzy amesema [*Tafsîr ar-Râzy* (2/244) tumebadili kidogo]: “Aina za sihiri ni nane:

* *Kwanza*: sihiri ya Wakaldani na Wakashdani waliokuwa wakiziabudu sayari saba zinazotembea. Walikuwa wakiitakidi kuwa nyota hizo ndizo zinazoupeleka ulimwengu, ndizo zinazoleta kheri na shari. Watu hao, Allâh Aliwapelekea Nabii Ibrâhîm عليه الصلاة والسلام.

* *Pili*: sihiri ya wenye njozi za maono (*wahmi*) na nafsi zenye nguvu. Kisha akatoa dalili kwamba njozi za maono zina athari kwa kuwa mtu anaweza kutembea juu ya kigogo kilichowekwa ardhini, na hawezi kutembea juu yake ikiwa kimewekwa juu ya mto au mfano wa hilo.

Akasema: “Ndipo matabibu wakaafikiana juu ya kumkataza anayetokwa na mnoga (damu puani) kutotazama vitu vyekundu; na mwenye kifafa kutotazama vitu vyenye kung’aa sana au kuzunguka duara. Kwa sababu nafsi imeumbwa ni yenye kutii *wahmi* (njozi za maono).”

* *Tatu*: kuomba msaada kwa mapepo wa ardhini, nao ni majini. Wao ni aina mbili: Waumini na makafiri.

Akasema: “Watu wenye tajriba wameshuhudia kuwa, kuwasiliana na mapepo hawa wa ardhini, huwa ni kwa amali sahali zaidi katika mazunguo (ambayo si Qur’âni). Na aina hii huitwa maazima na *taskhîr* ya kuwatiisha mapepo.

* *Nne*: kuzuga, kiinimacho na mazingaombwe. Msingi wake ni kuwa, macho huenda yakakosea na yakashughulika na kitu maalumu zaidi ya kingine. Kwani humuoni anayefanya mazingaombwe ambaye ni mahiri anadhihirisha jambo litakalowaduwaza watazamaji na anayachukua macho yao yamwelekee yeye mpaka atakapowamalizia shughuli yake kwa jambo hilo hufanya jambo lingine kwa haraka sana, na hapo wale

watu wakaona jambo lingine ambalo silo walilotarajia; na hapo wakastaajabu. Lau angalinyamaza wala asizungumze jambo litakalowageuza fikra zao kinyume na anachotaka kukitenda wala nafsi na njozi za maono zisingetaharaki katika jambo lingine analotaka kulitoa, basi wote wanaomtazama wangelitambua kila anachofanya.

* *Tano*: matendo ya ajabu yanayodhihiri kwa kuunganisha vifaa kwa mpango wa kiuhandisi kama vile aliyepanda farasi ambaye ana honi mkononi mwake, kila ipitapo saa moja, honi inalia bila ya yeyote kuigusa.

Akasema: "Na miongoni mwa haya ni kuunganisha sanduku la saa. Jambo hili kwa hakika haitakiwi kuhesabiwa kuwa ni katika sihiri. Kwa sababu lina sababu maalumu ya uhakika, yeyote atakayefahamu pia anaweza kufanya."

Nami nasema: "Mambo haya yamekuwa ni mazowea kwa wakati huu baada ya maendeleo ya kisayansi yaliosababisha kuvumbuliwa maajabu mengi."

* *Sita*: kujisaidia kwa sifa maalum zilizo ndani ya dawa na mafuta. Jambo hili, halipingiki; kwani taathira ya sumaku inaonekana wazi.

* *Saba*: kufungamana na moyo, ambapo mchawi hudai kuwa yeye analijua *al-Ismul-A'dhwam* (Jina Tukufu la Allâh) na kwamba majini wanamtii na wanamfwata katika mambo mengi. Basi kutakapoafikiana anayesikia maneno haya na akawa ni mtu mwenye akili dhaifu asiyeweza kupambanua, ataitakidi kuwa ni kweli tu, na moyo wake utapata aina fulani ya woga na hofu, hofu ikipatikana, nguvu ya hisia hudhoofika; na wakati huo mchawi akamakinika kufanya atakalo.

* *Nane*: kuchongeleza na kujikaribisha kwa watu kwa utaratibu, jambo hili limeenea kwa watu. [*Tafsîr Ibnu Kathîr* (1/147)].

Ibnu Kathîr رحمه الله amesema: "ar-Râzy ameingiza aina nyingi za sihiri hizi zilizotajwa katika fani ya sihiri kwa sababu ya ufinyu wa kuijua;

kwa sababu sihiri kilugha ni kitu kilichofichika.” [*Tafsîr Ibnu Kathîr* (1/147)].

*****

- ***Ugawaji wa ar-Râghib:***

ar-Râghib amesema: “Sihiri hutamkwa kwa maana mengi:

* *Kwanza*: kilicho finyu na kidogo. Kama kusema: “*Sahartussabiyya* (nimemhadaa mtoto na nimemvutia).” Na kila anayekivutia kitu, basi amekisihiri. Vile vile washairi husema: “*Sihrul‘uyûn* (sihiri ya macho),” kwa kule macho hayo kuwavutia watu. Na pia matabibu husema: “Mazingira yenye kusihiri (kuroga),” kama vile Qur’âni ilivyoeleza: **“… bali sisi ni watu tuliorogwa”** [15:15]. Yaani tumeepushwa na ujuzi. Na pia katika Hadîth imekuja: **“Hakika katika ubainifu muna sihiri.”**

* *Pili*: yanayotokeza kwa kuhadaa na kuzuga kusikokuwa na hakika, kama vile anavyofanya mtu wa kiinimacho kuyaweka mbali macho na kile anachokifanya kwa mkono mwepesi (*mkono wa paka*).

* *Tatu*: yanayopatikana kwa msaada wa mashetani kwa aina fulani ya kujikurubisha kwao. Katika hilo muna ishara ya Kauli Yake Allâh: **“... bali mashetani ndio waliokufuru, wakiwafundusha watu uchawi.”**

* *Nne*: yanayopatikana kwa kuziomba sayari na kuwateremsha mapepo yake – kama wanavyodai.” [*Fat-hul-Bârî:* (10/222) na *al-Mufradât* س ح ر].

*****

UHAKIKI NA UWAZI WA VIGAWANYO VYA SIHIRI

Kutokana na kudurusu vigawanyo vya ar-Râzy, ar-Râghib na Ulamaa wengine, tumekuta kuwa wao wameingiza katika sihiri ambayo hayamo. Sababu yake ni kuwa, wao wameegemea juu ya maana ya kilugha ya sihiri, ambayo ni: “Kilichofichika sababu yake na kuwa finyu.” Hapa

watakuwa wameingiza uvumbuzi wa maajabu na mambo yanayotokana na wepesi wa mkono, na pia kuchongeleza baina ya watu na mfano wa hayo miongoni mwa mambo yaliofichika sababu yake na njia zake kuwa finyu.

Yote hayo hayatuhusu katika utafiti huu. Makusudio na mhimili wa utafiti huu, unazunguka katika sihiri ya uhakika ambayo kwayo mchawi anautegemea kwa majini na mashetani.

Kuna hakika moja ambayo haina budi kubainishwa, nayo ni iliyotajwa na ar-Râzy vile vile ar-Râghib inayoitwa “maruhani (mapepo) wa sayari (nyota).” Kwa kweli haki ambayo tunamwabudia Allâh kwayo ni kwamba, sayari ni viumbe katika viumbe vya Allâh, zimeamriwa kufwata Amri Yake, wala hazina maruhani wala taathira yoyote kwa viumbe abadan.

Pengine mtu anaweza akauliza: “Sisi twashuhudia baadhi ya wachawi wanaotamka majina wanayodai kuwa ni ya sayari au yanaashiria sayari hizo na wanaziomba, baadaye uchawi wao hutimia na hutendeka mbele ya mtazamaji.”

Jawabu ni kuwa: “Jambo hili litakaposihi, basi si kutokana na taathira ya sayari, bali ni kutokana na taathira ya shetani kwa ajili ya kuwapoteza wachawi na kuwafitini; kama ilivyopokewa kuwa makafiri walipokuwa wakiomba masanamu ambao ni mawe yalio kiziwi, mashetani walikuwa wakiwajibu kwa sauti inayosikika itokayo ndani ya masanamu hayo. Basi wakidhani kuwa ndio miungu, na ilihali si hivyo. Njia za kupoteza ni nyingi zina matawi. Allâh Atukinge sisi na nyinyi shari ya mashetani-watu na majini.

FASILI YA NNE
MCHAWI ANAVYOMLETA JINI

1. Njia ya kwanza: njia ya *iqsâm* (kuapa).
2. Njia ya pili: njia ya kuchinja.
3. Njia ya tatu: njia ya *sufliyyah*.
4. Njia ya nne: njia ya najisi.
5. Njia ya tano: njia ya *tankîs*.
6. Njia ya sita: njia ya unajimu.
7. Njia ya saba: njia ya kiganja.
8. Njia ya nane: njia ya athari.

FASILI YA NNE
MCHAWI ANAVYOMLETA JINI

- ***Maafikiano baina ya mchawi na shetani*:**

Aghlabu yanayojiri, ni muafaka baina ya mchawi na shetani, kwamba wa kwanza awe atatenda baadhi ya matendo ya kishirikina au baadhi ya matendo ya ukafiri bayana – kwa siri au dhahiri – naye shetani amtumikie mchawi au amwamuru atakayemtumikia mchawi yule.

Kwa sababu mara nyingi huwa ni baina ya mchawi na shetani katika viongozi wa makabila ya majini na mashetani; basi kiongozi huyu akamwamuru mmojawapo wa masafihi na wapumbavu wa kabila ili amtumikie mchawi huyu na amtii katika kutekeleza amri zake miongoni mwa mambo yaliotendeka, au kufarikisha baina ya wawili, au kutia mapenzi kati yao, au kumfunga mwanamume asiweze kumjamii mkewe… hadi mwisho wa mambo aina hii ambayo tutayaeleza kwa tafsili Inshâ-allâh. [Tazama: Fasili ya sita ya kitabu hiki].

Basi hapo mchawi anamtumia jini huyu kwa matendo ya shari anayoyataka. Yule jini akimuasi, mchawi hujikurubisha kwa kiongozi wa kabila la kijini kwa aina fulani ya maazima (matalasimu) ambayo ndani yake yamebeba taadhima ya kumtukuza kiongozi huyu na kumuomba uokovu badala ya kumuomba Allâh! Basi kiongozi huyu humwadhibu yule jini na humwamuru kumtii mchawi, au humtuma mwengine amtumikie mchawi huyu mshirikina.

Kwa hivyo, ndipo tunapoona mafungamano baina ya mchawi na jini aliyeamrishwa na kiongozi wake, ni mafungamano ya kutenzwa nguvu na bughudha. Na hapa ndipo tuonapo jini huyu mara nyingi humletea madhara huyu mchawi katika mkewe, wanawe, mali yake au kitu kingine. Bali mara nyingine humletea madhara mchawi mwenyewe naye hatambui; kama vile kuumwa na kichwa daima, au kukosa usingizi, au kufazaika usiku, na mengineyo. Bali wachawi wa *sufliyyah* aghlabu hawapati watoto kwa sababu yule jini humuuwa mtoto katika kizazi kabla ya kukamilika umbo lake. Jambo hili ni mashuhuri miongoni mwa wachawi; hata baadhi yao wameacha uchawi ili wapate watoto.

Nakumbuka siku moja nilikuwa nikimtibu mwanamke aliyesibiwa na sihiri. Nilipomsomea Qur'âni, yule jini aliyewakilishwa kwa sihiri alitamka kwa ulimi wa yule mwanamke. Akasema: "Siwezi kumtoka."

Nikamwuliza: "Kwa nini?" Akajibu: "Kwa sababu nahofia mchawi asije akaniuwa!"

Nikamwambia: "Ondoka mahala hapa uwende kwingineko asipopajua mchawi."

Akasema: "Nyuma yangu atamtuma jini atakayenipeleka."

Nikamwambia: "Lau utasilimu na ukadhihirisha toba yako kwa ukweli na ikhlaas (uaminifu), tunaweza – kwa msaada wa Allâh – tukakufundisha Aya za Qur'âni zitakazokulinda na shari ya makafiri wa kijini na zitakuhami."

Jini akasema: "Laa, sitosilimu, nitabaki na ukristo wangu."

Nikamwambia: "Hakuna kulazimishana katika Dini. La muhimu ni umtoke mwanamke huyu."

Akasema: "Sitamtoka!"

Nikamwambia: "Kwa hivyo tunaweza– kwa msaada wa Allâh – sasa tukakusomea Qur'âni mpaka uteketee." Kisha nikampiga kipigo kikali, akalia. Akasema: "Nitatoka nitatoka." Basi – *Alhamdulillâh* – akatoka. Fadhila ni za Allâh Pekee!

Na yafahamika kuwa, mchawi kila awapo ana ukafiri mwingi na ukhabithi tele, majini nao huwa watiifu zaidi wa amri yake, na kinyume chake ni kinyume vile vile.

- ***Mchawi humleta vipi jini?***

Muna njia nyingi za kila aina, zote zimekusanya ushirikina au ukafiri bayana. Katika hizo nitataja – Inshâ-allâh – njia nane kwa kuonyesha

aina ya ushirikina au ukafiri katika kila njia. Yote hayo tutayataja kwa ufupi. [Na sitotaja kwa ukamilifu ili yeyote asije akaitumia, bali nitaondoa mambo muhimu yaliomo humo]. Nimesema hivyo kwa sababu baadhi ya Waislamu hawawezi kutofautisha baina ya tiba ya Qur'âni na tiba ya sihiri; tiba ya kwanza ni ya kiimani, na ya pili ni ya kishetani. Jambo linalowazidishia watu utata ni kuwa, baadhi ya wachawi wanaposoma azima zao za kikafiri, huwa wakisoma kwa sauti ya chini na wakitoa sauti ya juu katika Aya za Qur'âni anazozisikia yule mgonjwa, basi akidhani kuwa tiba yake ni ya Qur'âni na kumbe si hivyo. Basi hapo anafwata kila amri anayopewa. Lengo na makusudio ya kuzibaini njia hizi, ni kuwaonya ndugu zangu kutokana na njia ya shari, na ili njia ya waovu ipate kubainika.

*****

Njia Ya Kwanza
(Njia Ya Iqsâm)

Mchawi anaingia katika chumba chenye giza, kisha anawasha moto, juu yake anatia aina ya uvumba kulingana na maudhui yanayotakiwa, ikiwa yuwataka kufarikisha au kutia uadui na chuki na mfano wake, huweka uvumba wenye harufu mbaya juu ya moto, na akitaka kumtia mtu mapenzi au kumfungua fundo – mwanamume kwa mkewe – au kuifungua sihiri, atatita fusho lenye harufu nzuri, halafu yule mchawi anaanza kuisoma azima yake – ya kishirikina – nayo ni talasimu maalumu iliyokusanya kuwaapia majini kwa bwana wao na kuwaomba kwa mkubwa wao, vile vile imekusanya aina nyinginezo za ushirikina kama vile kuwaadhimisha wakubwa wa kijini, kuwaomba uokovu na mengineyo. Kwa sharti yule mchawi – Allâh Amlaani – awe hana usafi, ima awe ana janaba, amevaa nguo ya najisi n.k.

Anapomaliza kuisoma azima ya ukafiri, mbele yake hujitokeza pepo katika umbo la mbwa, nyoka au umbo lolote lile. Yule mchawi humwamuru analotaka. Wakati mwingine hakijitokezi kitu bali husikia sauti, na wakati mwingine hasikii chochote bali hufunga juu ya athari (yoyote) ya anayetakiwa kufanyiwa sihiri kama vile unywele wake au

kipande cha nguo chenye harufu yake n.k. halafu humwamuru jini analotaka.

***Maelezo juu ya njia hii*:**
Kwa kuidurusu njia hii, yamebainika mambo haya:

1. Majini hupenda chumba chenye giza.
2. Majini wanakula harufu ya mafusho ambayo hayakutajiwa Jina la Allâh.
3. Ushirikina ulio dhahiri na bayana katika njia hii, ni kule kuwaapia majini na kuwaomba msaada.
4. Majini hupendelea najisi, na mashetani huikaribia najisi.

*****

Njia Ya Pili
(Njia Ya Kuchinja)

Mchawi humleta ndege, mnyama, kuku, njiwa au chochote kwa sifa maalumu kulingana na matakwa ya jini – na aghlabu huwa ni kitu cheusi kwa sababu majini hupendelea zaidi rangi nyeusi – kisha anakichinja wala hataji Jina la Allâh wakati wa kuchinja – mara nyingine humpaka mgonjwa damu ile na mara nyingine huwa hafanyi hivyo – kisha anakitupa kitu hicho sehemu gofu, katika kisima au mahame (mahali palipohamwa) ambapo aghlabu huwa ndio maskani ya majini, wala hataji Jina la Allâh anaporusha, halafu anarudi nyumbani akisoma azima ya ushirikina na akimwamuru jini amfanyie analotaka.

***Maelezo juu ya njia hii*:**
Shirki hupatikana katika njia hii kwa mojawapo kati ya mawili:

Mosi: kumchinjia jini, nako ni haramu kwa itifaki ya Ulamaa wote waliopita na wa sasa. Bali ni shirki hasa, kwa sababu ni kumchinjia asiyekuwa Allâh, haifai kwa Muislamu kula achilia mbali kufanya hivyo. Pamoja na hayo, majahili katika kila zama na wakati, huwa wakiifanya amali hii chafu.

Yahyâ bin Yahyâ anasema: "Wahbi amenambia: mmoja katika masultani alichimbua kisima na akataka kutumia maji yake. Akawachinjia majini katika kisima hicho ili wasiyazamishe maji yale, akawalisha watu nyama hiyo. Habari ilipomfikia Ibnu Shihâb az-Zuhry alisema: "Ama yeye, amechinja kisicho halali kwake na akawalisha watu kisicho halali kwao, Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amekataza kula kilichochinjiwa majini." [*Âkâmul-Marjân*: 78].

Katika *Sahîh Muslim* muna Hadîth iliyopokewa kutoka kwa 'Alî bin Abîtâlib ﷺ amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

"Allâh Amlaani anayemchinjia asiyekuwa Allâh." ﴿لَعَنَ اللهُ مَنْ ذَبَحَ لِغَيْرِ اللهِ﴾.

Pili: azima ya ushirikina, nayo ni maneno hayo na talasimu katika hali ya kuwaleta majini, zimekusanya ushirikina ulio wazi kabisa kama alivyosema Shaikhul-Islâm Ibnu Taimiyya katika sehemu nyingi ya vitabu vyake. [Kama vile *al-Ibânah fî 'Umûmir-Risâlah*].

*****

Njia Ya Tatu
(Njia Ya Sufliyyah)

Njia hii ni mashuhuri kwa wachawi kama *at-Tarîqatus-Sufliyyah*. Mwenye njia hiyo huwa ana kundi kubwa la mashetani wanaomtumikia na kupitisha amri yake; kwa sababu yeye ni mkubwa wa wachawi kwa ukafiri na ulahidi(1) – Laana ya Allâh iwe juu yake!

***Ufupi wa njia hii ni kama ifwatavyo*:**
Mchawi – Laana ya Allâh imshukie – huwa akiuvaa Msahafu chini ya miguu yake kama viatu, kisha anaingia nao chooni, halafu anaanza kusoma matalasimu ya ukafiri ndani ya choo, kisha anatoka anaketi chumbani na anamwamuru jini amtendee jambo analotaka, basi majini nao hukimbilia kumtii na kutekeleza amri zake; si kwa lingine bali ni

(1) Ulahidi: ukanaji Mungu.

kwa kuwa amemkufuru Allâh Mtukufu, na amekuwa ni ndugu wa mashetani. Atarejea na hasara kubwa, Laana ya Allâh Mola wa viumbe imshukie popote alipo!

Mchawi huyu wa *sufliyyah* anasharutishwa ayatende madhambi makubwa – mbali na tuliyoyataja – kama vile kumnajisi maharimu (mama, binti yake n.k.), ulawiti, uzinifu au kutukana Dini; yote hayo ni kwa ajili ya kumridhisha shetani!!

*****

Njia Ya Nne
(Njia Ya Najisi)

Katika njia hii, mchawi maluuni huandika Sura yoyote katika Qur'âni Tukufu kwa damu ya hedhi au chochote cha najisi, kisha husoma talasimu ya ushirikina, jini anakuja na anamwamuru atakalo.

Wala haifichiki katika njia hii jinsi ukafiri unavyojitokeza bayana; kwa sababu kuifanyia stihizai Sura bali Aya ya Qur'âni, ni ukafiri mkubwa wa kumkufuru Allâh Mtukufu, basi seuze kuiandika kwa najisi? Twajilinda kwa Allâh Atuepushiye hizaya, twamuomba Azithibitishe nyoyo zetu katika Imani, Atufishe katika Imani na Atufufue katika kundi la mbora wa viumbe.

*****

Njia Ya Tano
(Njia Ya Tankîs)

Katika njia hii, mchawi – Laana ya Allâh imshukie – huiandika Sura ya Qur'âni Tukufu kwa herufi moja moja kinyume-nyume, yaani huanzia mwisho kurudia mwanzo, kisha husoma azima yake ya ushirikina, halafu jini hufika, naye humwamuru matilaba yake.

Katika njia hii pia, ni haramu pamoja na ushirikina na ukafiri uliomo ndani yake.

*****

Njia Ya Sita
(Njia Ya Unajimu)

Njia hii vile vile huitwa *ar-Rasd* (ulinzi/uangalizi), kwa sababu mchawi huwa akilinda kutokeza nyota fulani kisha huiomba kwa visomo vya kichawi, halafu yuwasoma talasimu nyingine iliyobeba ushirikina na ukafiri Anaoujua Allâh. Halafu hufanya harakati fulani – akidai kuwa anamteremsha rohani (pepo) wa nyota hiyo – lakini kwa hakika ni ibada ya kuiabudu nyota hii badala ya Allâh; hata kama mnajimu hatambui, hiyo ni ibada na kumuadhimisha asiyekuwa Allâh. Basi hapo mashetani huitika amri ya mchawi huyu maluuni huku akidhani kuwa ile nyota ndiyo iliyomsaidia; lakini nyota iliyosingiziwa uwongo huu masikini haijui chochote kuhusu habari hiyo. Wachawi wanadai kuwa sihiri hii haiwezi kufunguliwa mpaka idhihiri nyota ile ile kwa mara nyingine. Na muna nyota ambazo hazidhihiri ela mwaka mara moja tu. Basi hungoja mpaka itokeze halafu wanasoma visomo vya kuiomba msaada nyota hii ili iwafungulie sihiri walio nayo. [Ama wale wanaotibu kwa Qur'âni, huibatilisha sihiri hiyo papo hapo kwa Fadhila za Allâh Mtukufu].

Wala haifichiki yaliomo katika njia hii kutokana na kumuadhimisha asiyekuwa Allâh na kuomba msaada kwa asiyekuwa Allâh; na yote hayo ni ushirikina, na zaidi ya hapo ni matalasimu ya ukafiri.

*****

Njia Ya Saba
(Njia Ya Kiganja)

Katika njia hii, mchawi humleta mtoto mdogo ambaye hajabaleghe kwa sharti awe hana udhu, anakishika kiganja cha mkono wa kushoto cha mtoto na anakichora mraba kama hivi:



Kando ya mraba huu huandika talasimu ya sihiri – aghlabu huwa ni ya kiushirikina – huiandika hiyo talasimu pande zote nne, kisha huweka katika kiganja cha mtoto katikati ya mraba huu, zeti na maua rangi ya samawati (buluu), au zeti na wino rangi ya samawati, kisha anaandika talasimu nyingine kwa herufi moja moja juu ya karatasi mstatili (ndefu), halafu karatasi hii huwekwa juu ya uso wa mtoto halafu huvaa kofia, halafu yule mtoto hufunikwa kwa guo zito, na katika hali hii yule mtoto huwa anatazama kiganja chake, na bila shaka huwa haoni kwa sababu ya giza. Halafu yule mchawi maluuni huanza kusoma azima kali ya ukafiri; basi mara yule mtoto anahisi kuna mwangaza na huziona picha zikitaharaki katika kiganja chake. Yule mchawi humuuliza yule mtoto: "Waona nini?" Mtoto yuwasema: "Mbele yangu naona sura ya mtu." Mchawi humwambia: "Mwambie: Waambiwa na mwenye azima ufanye kadha na kadha." Basi zile picha huwa zikitaharaki kulingana na amri. Na aghlabu huwa wakiitumia njia hii katika kutafuta vitu vilivyopotea.

Basi vile vile hayafichiki yaliomo katika njia hii miongoni mwa ushirikina, ukafiri na matalasimu yasiyofahamika.

*****

Njia Ya Nane
(Njia Ya Athari)

Katika njia hii, mchawi humtaka mgonjwa ampelekee baadhi ya athari zake kama vile kitambaa, kilemba, kanzu, shati au chochote kinachobeba harufu ya jasho la mgonjwa, halafu akiifunga nguo hiyo nchani mwake, kisha hupima kiasi cha vidole vinne halafu hukishika imara kitambaa kile, kisha husoma *Sûratut-Takâthur* au Sura yoyote fupi kwa sauti ya juu, halafu husoma matalasimu ya ushirikina kwa sauti ya chini, kisha huwanadia majini akisema: "Ikiwa maradhi aliyonayo sababu yake ni majini, basi ipunguzeni (nguo hii), na ikiwa yatokana na kijicho, kirefusheni, na ikiwa yanahitajia tiba, basi kiacheni kama kilivyo."

Halafu hukipima kwa mara nyingine, akiona kimerefuka zaidi ya vidole vinne, humwambia: "Wewe umesibiwa na husuda." Ikiwa kimepungua, humwambia: "Umesibiwa na jini." Na ikiwa kiko vile vile kipimo cha vidole vinne, humwambia: "Huna kitu, nenda kwa daktari."

***Maelezo juu ya njia hii*:**

1. Kumrenga mgonjwa wakati mchawi ainuapo sauti yake kwa Qur'âni ili mgonjwa adhanie kuwa yuwatibu kwa Qur'âni, na ilihali si hivyo, mambo yote yamo kwenye talasimu aliyoisoma kwa siri.
2. Kuomba msaada kwa majini na kuwanadia; yote haya ni kumshirikisha Allâh Mtukufu.
3. Majini wana uwongo mwingi, ni kipi kitakachokujulisha kwamba jini huyu ni mkweli au ni muongo katika jambo hili. Na tumeyatahini matendo ya baadhi ya wachawi, mara wakiwa wakweli na mara nyingi zaidi wakiwa waongo; kwani mgonjwa mmoja alitujia na akatwambia kuwa, mchawi amemwambia: "Umesibiwa na husuda." Tulipomsomea Qur'âni, yule jini alitamka na wala hakuwa amesibiwa na husuda, basi wapo na wengine wengi wasiohesabika.

Yawezekana muna njia nyinginezo ambazo sizijui.

- ***Alama za kumjua mchawi*:**

Ikipatikana alama moja miongoni mwa alama hizi kwa yeyote anayetibu, basi huyo ni mchawi bila shaka yoyote. Alama zenyewe ni hizi:

1. Humwuliza mgonjwa jina lake na jina la mama yake.
2. Huchukua athari fulani ya mgonjwa kama vile kanzu, shati, kofia, kitambaa, fulana n.k.
3. Mara nyingine huwa anataka mnyama mwenye sifa maalumu, huwa hataji Jina la Allâh anapomchinja. Wakati mwingine ile damu yake hupaka sehemu ya maumivu kwa mgonjwa, au huitupa mahala pasipokaliwa.
4. Kuandika talasimu.
5. Kusoma maazima na matalasimu yasiyofahamika.
6. Kumpa mgonjwa *hijabu* iliyokusanya miraba ambayo ndani yake muna herufi na nambari.

7. Humwamuru mgonjwa kuwaepuka watu kwa muda maalumu katika chumba kisichopenyeza mwangaza wa jua, chumba hicho makabwela hukiita *al-Hijba*.
8. Mara nyingine humtaka mgonjwa asiguse maji kwa muda maalumu, aghlabu huwa ni siku arubaini; na hii ni alama kuwa jini anayemtumikia mchawi huyu, ni Mkristo.
9. Humpa mgonjwa vitu avizike ardhini.
10. Humpa mgonjwa makaratasi ayachome na ajifukize kwayo.
11. Hurogonya.[1]
12. Mara nyingine mchawi humwambia mgonjwa (kabla yeye kumweleza) jina lake, jina la mji wake na tatizo alilokuja nalo.
13. Humwandikia mgonjwa herufi zilizokatwakatwa katika karatasi (*hijabu*) au katika sahani nyeupe ya kauri, na humwamuru mgonjwa aitie maji na anywe maji yale.

Basi utakapojua kuwa mtu huyo ni mchawi,[2] nakuonya usimwendee, laa si hivyo, itakuwajibikia kauli ya Mtume صلى الله عليه وآله وسلم isemayo:

"Atakayemwendea kuhani (mganga wa ramli) na akamsadiki aliyosema, basi ameshayakufuru aliyoteremshiwa Muhammad."

﴿مَنْ أَتَى كَاهِنًا أَوْ عَرَّافًا فَصَدَّقَهُ بِمَا يَقُولُ فَقَدْ كَفَرَ بِمَا أُنْزِلَ عَلَى مُحَمَّدٍ﴾.

[*Bazzâr*, Hadîth hii ni *Hasan* kwa *shawâhid* zake,[3] pia imepokewa na Ahmad na al-Hâkim].

---

[1] Huzungumza maneno yasioeleweka.

[2] Katika sehemu nyingine – kama vile Mombasa, Lamu, Zanzibar – watu hawa hawaitwi wachawi au waganga, bali huitwa *waalimu* ili mtu asione vibaya kuwaendea; *Maalim Fulani*. Lakini alama zao ni zizi hizi.

[3] *Shawâhid* ni wingi wa *Shâhid*: Ni Hadîth iliyo sawa au kama hiyo iliyotajwa, lakini imepokewa na Swahaba mwingine; au Hadîth ile ikawa imepokewa na Swahaba yule yule lakini akawa ameipokea kulingana na maana yake na ubainifu wake katika baadhi ya maswala, kwa namna ambayo kwa mtizamo wa juu-juu wa mtiririko wa Hadîth hiyo itadhaniwa kuwa ni Hadîth mbili alizozisikia Swahaba yule yule katika vikao viwili (tofauti) alizozisikia kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم bila ya wasta (kupokea kutoka kwa mtu

FASILI YA TANO
HUKUMU YA SIHIRI KATIKA SHARIA YA UISLAMU

- Hukumu ya kujifunza sihiri katika Uislamu.
- Hukumu ya mchawi katika Uislamu.
- Hukumu ya mchawi wa *Ahlul-Kitâb* (Mayahudi na Manaswara).
- Je, inafaa kuifungua sihiri kwa sihiri?
- Tofauti baina ya sihiri, mwujiza na karama.

---

mwingine) au akaisikia kwa wasta, au Hadîth moja aliisikia kwa wasta na nyingine ameisikia bila ya wasta.

FASILI YA TANO
HUKUMU YA SIHIRI KATIKA UISLAMU

***Hukumu ya mchawi katika Sharia ya Uislamu*:**

1. Imâm Mâlik رحمه الله تعالى amsema: "Mchawi anayefanya uchawi wala hakuna aliyemfanyia ela ni yeye mwenyewe, ni mithili ya aliyeambiwa na Allâh katika Qur'âni: "**Kwa yakini wanajua kwamba aliyekhiyari haya hatakuwa na sehemu yoyote katika Akhira.**" [2:102]. Kwa hivyo naona auliwe atakapofanya yeye mwenyewe." [*al-Muwatta:* 628].
2. Ibnu Qudâma رحمه الله تعالى amesema: "Adhabu ya mchawi ni kuuawa; hilo limepokewa kutoka kwa 'Umar, 'Uthmân bin 'Affân, Ibnu 'Umar, Hafsah, Jundub bin 'Abdullâh, Jundab bin Ka'bi, Qais bin Sa'di na 'Umar bin 'Abdul-'Azîz; nayo ndio kauli ya Abû Hanîfa na Mâlik."
3. Imâm Qurtuby رحمه الله تعالى amesema: "Mafuqahaa wamekhitilafiana katika hukumu ya mchawi ambaye ni Muislamu na dhimmi (asiye Muislamu anayekuwa chini ya himaya ya dola ya Kiislamu). Imâm Mâlik akasema, Muislamu atakapofanya sihiri yeye mwenyewe kwa maneno ya ukafiri, basi atauliwa wala hatotakiwa atubie, na toba yake haikubaliwi kwa sababu jambo hilo hulifanya kwa siri kama vile mzandiki na mzinifu; na ni kwa kuwa Allâh Mtukufu Ameuwita uchawi kuwa ni ukafiri Aliposema: **"… (Malaika hao) hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: "Sisi ni mtihani (wa kutazamwa kutii kwenu); basi usikufuru."**

Nayo ndio kauli ya Imâm Ahmad bin Hambal, Abû Thawr, Is-hâq, Shâfi na Abû Hanîfa. [*Tafsirul-Qurtuby:* 2/48].

4. Ibnul-Mundhir رحمه الله تعالى amesema: "Mtu atakapokiri kuwa amefanya sihiri kwa maneno ya ukafiri, yapasa auliwe asipotubia, vile vile lau ubainifu utathubutu, ubainifu huo ukaelezea maneno ambayo ni ukafiri, atauliwa.

Iwapo maneno aliyosema kuwa alirogea kwayo si ukafiri, basi haifai kuuliwa. Ikiwa amesababisha kwa yule aliyerogwa kosa linalopasa kisasi, atachukuliwa kisasi ikiwa amefanya hivyo. Na ikiwa ni kosa lisilo na kisasi, atatozwa diya (fidia)." [*Tafsîrul-Qurtuby:* 2/48].

5. al-Hâfidh Ibnu Kathîr رحمه الله تعالى amesema: "Ametoa dalili kwa Kauli ya Allâh: **"Lau wao wangaliamini …"** kila aliyesema kuwa mchawi ni kafiri kama ambavyo hiyo ni riwâya ya Imâm Ahmad bin Hambal na kundi la *Salaf* (wema waliotangulia). Na kumesemwa kuwa hawi kafiri, lakini adhabu yake ni kukatwa shingo kama alivyopokea Shâfi na Ahmad wakisema: "Sufyân bin 'Uyaina ametuhadithia kutoka kwa 'Amru bin Dînâr kwamba alimsikia Bajâlah bin 'Abadah akisema: "'Umar bin al-Khattâb ﵁ aliandika kuwa: "Muuweni kila mchawi mume na mke." Tukawauwa wachawi watatu."

Akasema: "Hadîth hii imehadithiwa na Bukhârî." [Tazama: *Sahîhul-Bukhârî*: 6/257].

Akasema: "Na pia iliwahi kutokea kuwa Hafsah Mama wa Waumini alirogwa na mjakazi wake, akaamuru akauliwa."

Imâm Ahmad amesema: "Imethubutu kwa Maswahaba watatu wa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم kumuuwa mchawi." [*Tafsîr Ibnu Kathîr* (1/144)].

6. al-Hâfidh Ibnu Hajar رحمه الله تعالى amesema: "Kwa Imâm Mâlik ni kuwa, hukumu ya mchawi ni hukumu ya mzandiki; toba yake haikubaliwi, na atauliwa kwa njia ya adhabu iwapo itamthubutukia hilo; na kwa kauli hii Imâm Ahmad pia amesema."

Imâm Shâfi amesema: "Hatauliwa ispokuwa atakapokubali kuwa ameuwa kwa uchawi wake, hapo naye atauliwa." [*Fat-hul-Bârî:* 10/236].

***Kwa ufupi*:**
Imebainika kuwa Jumhuri ya Ulamaa wanasema mchawi auliwe – ispokuwa Imâm Shâfi رحمه الله تعالى – amesema: "Hatauliwa ispokuwa atakapouwa kwa sihiri yake, hapo naye atauliwa kwa kisasi."

* Ibnu Qudâma رحمه الله تعالى amesema: "Abû Hanîfa رحمه الله تعالى amesema: "Atauliwa kwa ufahamu wa Hadîth hii; na kwa kuwa sihiri ni jinai inayopasa kumuua Muislamu, likapasisha kumuuwa dhimmi kama kuuwa." [*al-Mughnî:* 10/115].
* al-Hâfidh Ibnu Hajar رحمه الله تعالى amesema: "Imâm Mâlik رحمه الله تعالى amesema: "Mchawi wa *Ahlul-Kitâb* hauliwi ela atakapouwa kwa sihiri yake, hapo atauliwa." Na akasema pia: "Atakaposababisha madhara kwa Muislamu kwa sihiri yake ambaye hana mkataba, atakuwa amevunja mkataba na itakuwa halali kuuuliwa." Mtume صلى الله عليه وآله وسلم hakumuuwa Labîd bin al-A'sam kwa sababu yeye (Mtume صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa hajilipizii kisasi, na pia alichelea kama angalimuuwa, fitina ingelichemka baina ya Waislamu na washirika wake Ansâr." [*Fat-hul-Bârî:* 10/236].
* Imâm Shâfi رحمه الله تعالى amesema: "Mchawi wa *Ahlul-Kitâb* hauliwi ela atakapouwa kwa sihiri yake, hapo naye atauliwa." [*Fat-hul-Bârî*:10/236].
* Ibnu Qudâma رحمه الله تعالى amesema: "Ama mchawi wa *Ahlul-Kitâb* hauliwi kwa sihiri yake ela atakapouwa kwa sihiri hiyo, nayo aghlabu huwa ikiuwa, kwa hivyo atauliwa kwa kisasi, kama ilivyothubutu kuwa Labîd bin al-A'sam alimroga Mtume صلى الله عليه وآله وسلم naye (Mtume صلى الله عليه وآله وسلم) hakumuuwa, na shirki ni kubwa kuliko sihiri yake na wala hakuuliwa kwa sababu yake.

Akasema: "Hadîth zimepokewa kuhusu mchawi wa Waislamu kwa sababu yeye hukufuru kwa ile sihiri yake, na huyu (ambaye si Muislamu) ni kafiri asilia, na kiasi chao hutanguliwa kwa kuitakidi ukafiri na kuzungumza kwayo, na hutanguka kwa zinaa kwa muhsan (mwenye mke/mume) kwani dhimmi – kwao – hauliwi, kwa hiyo zinaa lakini Muislamu huuliwa kwayo. Allâh Ndie Anayejua zaidi." [*al-Mughnî:* 10/115].

JE, INAFAA KUIFUNGUA SIHIRI KWA SIHIRI?

1. Ibnu Qudâma رحمه الله تعالى amesema: "Ama anayefungua sihiri, ikiwa anafungua kwa Qur'âni, dhikri au kwa maneno yasio na ubaya, basi hapana ubaya. Na ikiwa ni kwa kitu kama sihiri, basi Imâm Ahmad bin Hambal amejizuia (kusema lolote)." [*al-Mughnî***:** 10/114].

2. al-Hâfidh Ibnu Hajar رحمه الله تعالى amesema: "Itajibiwa kuhusu kauli ya Mtume صلى الله عليه وآله وسلم isemayo:

﴿النُّشْرَة مِنْ عَمَل الشَّيْطَان﴾.

"*Nushra (kago)* ni katika amali ya shetani."

Kuwa hiyo ni ishara katika asili yake, anayekusudia kheri, basi ni kheri, laa si hivyo itakuwa ni shari. Lakini yawezekana *nushra* ikawa ipo aina mbili." [*Fat-hul-Bârî*: 10/233].

Nami nasema: Hivi ndivyo sawa, *nushra* zipo aina mbili:

*Kwanza***:** *nushra* inayojuzu; nayo ni kuifungua sihiri kwa Qur'âni, dua au nyuradi za ki-Sharia.

*Pili***:** *nushra* iliyoharamishwa, nayo ni kuifungua sihiri kwa sihiri kwa kuomba msaada wa mashetani, kuwakaribia, kuwaomba uokovu na kuwaridhisha. Labda aina hii ndio iliyokusudiwa na Mtume صلى الله عليه وآله وسلم aliposema: **"*Nushra* ni katika amali ya shetani."** Aina hii ya *nushra* itajuzu vipi na ilihali Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amekataza katika Hadîth nyingi mtu kuenda kwa wachawi na makuhani na akabainisha kuwa anayewasadikisha ameshakufuru aliyoteremshiwa Muhammad صلى الله عليه وآله وسلم.

3. Ibnul-Qayyim رحمه الله تعالى amesema: "*Nushra* ni kuifungua sihiri kwa aliyesihiriwa, nayo ni aina mbili:

Kwanza: kuifungua sihiri kwa sihiri kama hiyo, nayo ndio amali ya shetani, na juu ya kauli hiyo ndio inayochukuliwa kauli ya al-Hasan al-Basry, mwenye kufanya na kufanyiwa *nushra* wakajikurubisha kwa shetani kwa alipendalo, naye akaibatilisha amali yake kwa aliyesihiriwa.
Pili: nushra ya zunguo (la Qur'âni), kinga na dua zinazoruhusiwa; jambo hili linajuzu.

JE, INAFAA KUJIFUNZA SIHIRI?

1. al-Hâfidh Ibnu Hajar رحمه الله تعالى amesema: "Kauli Yake Allâh Isemayo: **"Sisi ni mtihani (wa kutazamwa kutii kwenu); basi usikufuru."** Inaashiria kuwa kujifunza sihiri ni ukafiri." [*Fat-hul-Bârî:* 10/225].

2. Ibnu Qudâma رحمه الله تعالى amesema: "Kujifunza na kufundisha sihiri ni haramu, wala hatujui kama muna ikhtilafu ndani yake miongoni mwa Wanazuoni." Watu wetu wamesema (Yaani Madh-hab ya Hambal): "Mchawi hukufuru kwa kujifunza na kuifanya, aitakidi uharamu wake ama asiitakidi; yote ni mamoja." [*al-Mughnî***:** 10/106].

3. Abû 'Abdillâh ar-Râzy amesema: "Kuijua sihiri si jambo baya wala halijakatazwa, wahakiki wameafikiana juu ya hilo, kwa sababu ilimu ina utukufu ndani yake, na pia ni kwa ujumla wa Kauli ya Allâh Mtukufu Isemayo:

﴿قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لاَ يَعْلَمُونَ﴾.

"Sema: "Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojuwa na wale wasiojuwa?" [39: 9].

Lau kama uchawi usingalijulikana, basi isingaliwezekana kutofautisha baina yake na muujiza, na kujua muujiza kuwa ndio muujiza jambo hilo ni wajib, na linalosimamisha katika wajib ni wajib vilevile, hili lapelekea iwe kuitafuta ilimu ya sihiri ni wajib, na linalokuwa wajib vipi liwe ni haramu na ni jambo baya?"

4. al-Hâfidh Ibnu Kathîr رحمه الله تعالى amesema: "Maneno ya ar-Râzy yanahitaji kutazamwa kwa njia zifwatazo:

*Kwanza***:** aliposema: "Kuijua sihiri si jambo baya," ikiwa anakusudia hapana ubaya kiakili, basi wanaomkhalifu katika Mu'tazila wanakataza hili, na ikiwa anakusudia kuwa hapana ubaya ki-Sharia, basi katika Aya hii tukufu: **"Wakafuata yale waliyoyafuata mashetani, (wakadai kuwa yalikuwa) katika ufalme wa (Nabii) Suleiman;"** inatia ubaya katika kujifunza sihiri. Katika *Sahîh Muslim* Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿مَنْ أَتَى عَرَّافًا أَوْ كَاهِنًا، فَقَدْ كَفَرَ بِمَا

"Atakayemwendea anayedai ghaibu au kuhani, basi ameshakufuru aliyoteremshiwa

Muhammad.” [Imepokewa na Maimamu wanne kwa isnadi *jayyid*].

أُنْزِلَ عَلَى مُحَمَّدٍ﴾.

Katika kitabu cha *Sunan* (Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema):

“Anayefunga kifundo na akavuvia humo, basi ameshafanya sihiri.”

﴿مَنْ عَقَدَ عُقْدَةً وَنَفَثَ فِيهَا فَقَدْ سَحَرَ﴾.

Ama kauli yake isemayo: “Wala halijakatazwa, wahakiki wameafikiana juu ya hilo.” Vipi halikukatazwa pamoja na kuwa tumetaja Aya na Hadîth, na itifaki ya wahakiki inapelekea maswala haya yamenasiwa (yameandikwa) na Maimamu wa Ulamaa au wengi wao, na ziwapi *nassi* (maandiko) zao juu ya hilo? Halafu yeye kuingiza kwake sihiri katika ujumla wa Aya: **“Sema: “Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojuwa na wale wasiojuwa?”** ndani yake panahitaji kutazamwa; kwa sababu Aya hii inajulisha kuwasifu wajuzi wa ilimu ya Sharia (wala sio sihiri). Na ni kwa nini umesema kuwa hii inatokana nayo, halafu inapanda hadi katika kupasa kujifunza kwa kuwa haiwezekani kuujua muujiza ela kwa ilimu hiyo, kauli hii ni dhaifu bali ni fasidi, kwa sababu muujiza mkubwa zaidi wa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم ni Qur’âni Tukufu ambayo **haitaifikia batili mbele yake wala nyuma yake, imeteremshwa na Mwenye Hekima, Ahimidiwaye.** Halafu kuujua muujiza hakuko katika kuijua ilimu ya sihiri asilani.

Isitoshe, katika yanayojulikana kuwa ni dharura ni kuwa Maswahaba, Taabiina, Maimamu wa Waislamu na wote waliobakia, walikuwa wakiujua muujiza na wakiweza kutofautisha baina yake na jambo lingine, wala hawakuwa wakiijua sihiri na wala pia hawakujifunza wala kuifunza. Allâh Anajua zaidi.” [*Tafsîr Ibnu Kathîr* (1/145)].

5. Abû Hayyân amesema katika kitabu *al-Bahrul-Muhît:* “Ama hukumu ya kujifunza sihiri, kinachokuwa ni cha kumuadhimisha asiyekuwa Allâh miongoni mwa sayari na mashetani, huo ni ukafiri kwa ijimai (itifaki ya Umma), si halali kujifunza wala kuifanyia amali, vile vile kinachokusudiwa kujifunza kwa ajili ya kumwaga damu na kufarikisha baina ya wanandoa na marafiki. Ama ikiwa hatafundishwa chochote katika hayo, basi dhahiri ni kwamba si halali kujifunza wala kuitenda.”

Kinachokuwa ni katika aina ya kuzuga, utapeli na mazingaombwe (kiinimacho), haifai kujifunza kwa sababu ni katika ubatilifu, na iwapo atakusudia kuwa ni pumbao, mchezo na kufurahisha watu kutokana na wepesi wa harakati zake, basi inakarahishwa." [*Rawâ-i'ul-Bayân:* 1/85].

Nami nasema: "Haya ni maneno mazuri yanayofaa kutegemewa katika jambo hili."

TOFAUTI BAINA YA SIHIRI, KARAMA NA MUUJIZA

* al-Mâziry amesema: "Tofauti baina ya sihiri, muujiza na karama, ni kwamba sihiri huwa ni kwa kumenyana na maneno na matendo mpaka matilaba ya mchawi yatimie. Karama haihitajii mambo hayo, bali aghlabu hutokezea kwa mwafaka. Ama muujiza hutofautiana na karama kwa njia ya ukinzani." [*Fat-hul-Bârî*: 10/223].

* al-Hâfidh Ibnu Hajar رحمه الله تعالى amesema: "Imâmul-Haramain amenakili ijimai kuwa sihiri huwa haidhihiri ela ikitoka kwa mtu fasiki, na karama haidhihiri kwa mtu fasiki."

Akasema tena al-Hâfidh: "Yatakiwa izingatiwe hali ya anayefanya jambo lisilo la kawaida, ikiwa ameshikamana na Sharia ameepukana na yanayoangamiza, basi kitakachodhihiri kwake katika mambo yasio ya kawaida kitakuwa ni karama, la si hivyo basi hiyo ni sihiri, kwa sababu huwa inatokana na mojawapo ya aina zake kama vile kusaidiwa na shetani." [*Fat-hul-Bârî:* 10/236].

***Uzindushi*:**
Huenda mtu akawa si mchawi wala hafahamu chochote katika uchawi, halafu akawa si aliyeshikamana na Sharia, bali mara nyingine huyafanya baadhi ya madhambi yanayoangamiza, pamoja na hayo huwa akifanya baadhi ya maajabu, na huenda akawa ni katika watu wa bid'a au waabudu-makaburi. Basi kauli ya hakika kuhusu mtu huyu, huwa anasaidiwa na shetani ili awapambie watu njia yake ya uzushi, watu wapate kumfwata na waache Sunnah. Aina hii ya watu wapo wengi, hasa mtu huyo akiwa ni kiongozi wa njia iliyozushwa ya upotofu.

*****

FASILI YA SITA
KUIBATILISHA SIHIRI

***Kwanza*: sihiri ya kufarikisha:**
- Dalili za sihiri ya kufarikisha.[1]
- Kutibu sihiri ya kufarikisha.
- Sampuli ya kiutendaji ya shiri ya kufarikisha.
* Jini anayeitwa Shaqwân.
* Jini anaweka sihiri katika mto (wa kulalia).
* Hali ya mwisho ya sihiri aliyoitibu mtungaji kabla ya kukiandika kitabu hiki.

***Pili*: sihiri ya mapenzi:**
- Dalili za sihiri ya mapenzi.
- Hutokeaje sihiri ya mapenzi?
- Athari ya kinyume za sihiri ya mapenzi.
- Sihiri halali.
- Kutibu sihiri ya mapenzi.
* Mwanamume anayeongozwa na mkewe.

***Tatu*: sihiri ya kusawiri (kuzuga):**
- Dalili za sihiri ya kuzuga.
- Kuibatilisha sihiri ya kuzuga.
- Sampuli ya kiutendaji ya kuibatilisha sihiri ya kuzuga.

***Nne*: sihiri ya wazimu:**
- Dalili za sihiri ya wazimu.
- Kuitibu sihiri ya wazimu.
- Sampuli ya kiutendaji ya kuitibu sihiri ya wazimu.

***Tano*: sihiri ya upumbavu:**
- Dalili zake.

---
[1] Kufarikisha: kuwatenganisha watu.

- Namna ya kuitibu.

***Sita*: sihiri ya sauti (kelele):**
- Dalili za sihiri ya sauti.
- Kuitibu sihiri ya sauti.

***Saba*: sihiri ya magonjwa:**
- Dalili za sihiri ya magonjwa.
- Kuitibu sihiri ya magonjwa.
- Sampuli ya kuitibu sihiri ya magonjwa.

***Nane*: sihiri ya kutokwa damu:**
- Hutokeaje sihiri ya kutokwa damu?
- Kutibu sihiri ya kutokwa damu.
- Sampuli ya kutibu sihiri ya kutokwa damu.

***Tisa*: sihiri ya kuvunja ndoa:**
- Dalili za sihiri ya kuvunja ndoa.
- Kuitibu sihiri ya kuvunja ndoa.
- Sampuli ya kuitibu sihiri ya kuvunja ndoa.
- Simulizi muhimu kuhusiana na sihiri.

FASILI YA SITA
Kuibatilisha Sihiri

Katika fasili hii, tutazungumzia – Inshâ-allâh – juu ya anuwai za sihiri namna zinavyomwathiri aliyesihiriwa na kuitibu kila anuwai kwa mujibu wa Qur'âni, Hadîth, dua na nyuradi. Napenda kutanabahisha kuwa, katika fasili hii na nyinginezo zinazofungamana na tiba, utakuta mambo ambayo hayakuthubutu kwa *nassi* (maandiko) kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم katika kutibu hali makhsusi, lakini mambo hayo yako katika kaida ya ujumla iliyothubutu katika Qur'âni na Sunnah. Kwa mfano, utakuta tiba kwa Aya moja ya Qur'âni au nyingi kutoka katika Sura mbalimbali, basi yote haya yapo chini ya Kauli Yake Allâh:

﴿وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ﴾.

"Tunateremsha katika Qur'âni ambayo ni ponyo na rehma kwa wanaoamini." [17: 82].

Katika Ulamaa muna wasemao: "Makusudio ya **ponyo** hapa, ni ponyo la kimaana – yaani kutokana na shaka, shirki, ufuska na ubaya." Na muna wasemao kuwa makusudio ni **ponyo** la kimaana na kihisia pamoja.

Muna dalili nyingine ilio wazi kuliko hii, bali ndio tegemeo katika mlango huu. 'Âisha رضي الله عنها amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم aliingia kwake na kuna mwanamke aliyekuwa akimtibu ('Âisha) na akimzungua. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akamwambia:

﴿عَالِجِيهَا بِكِتَابِ اللهِ﴾.

"Mtibu kwa Kitabu cha Allâh." [Imesahihishwa na al- al-Albâny katika *Silsilatus-Sahîhah* (1931)].

Basi lau utachunguza katika Hadîth hii, utakuta kwamba Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amejumlisha wala hakuhusisha Aya maalumu au Sura maalumu, ikabainika kuwa Qur'âni yote ni **ponyo**. Na katika majaribio ya kiutendaji yaliotudhihirikia mara nyingi mno, ni kuwa Qur'âni sio tiba ya sihiri, wazimu na husuda pekee, bali ni tiba hata ya maradhi ya viungo pia.

Pengine mtu atasema: “Hapana budi kuwepo dalili makhsusi katika kila Aya tunayoichagua katika Qur’âni ili tumtibu mgonjwa, au tutasimama mpaka tupate *nassi* (maandiko) thabiti kuwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alizungua kwa Aya hii ugonjwa huu.”

Basi twawaambia watu hawa: Mtume صلى الله عليه وآله وسلم aliweka kaida ya ujumla katika kila zunguo. Imethubutu katika *Sahîh Muslim* kuwa watu walisema: “*Yâ Rasûlallâh,*, tulikuwa tukizungua zama za ujahiliya.” Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akawaambia:

﴿اعْرِضُوا عَلَيَّ رُقَاكُمْ، لَا بَأْسَ بِالرُّقَى مَا لَمْ يَكُنْ فِيهِ شِرْكٌ﴾.

“Nileteeni zunguo lenu (nilitazame). Zunguo halina ubaya maadamu halijakuwa ni shirki.” Muslim (14/187 *Nawawy*)].

Kutokana na Hadîth hii, twachukulia kujuzu kwa zunguo la Qur’âni, Sunnah, dua, mengineyo au hata mazunguo ya zama za ujahiliya maadamu hayana ushirikina.

*****

Allâh Amesema katika <u>*S*</u>*ûratul-Baqarah*:

﴿وَاتَّبَعُوا مَا تَتْلُو الشَّيَاطِينُ عَلَى مُلْكِ سُلَيْمَانَ وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أُنْزِلَ عَلَى الْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ هَارُوتَ وَمَارُوتَ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولاَ إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلاَ تَكْفُرْ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ وَمَا هُمْ بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلاَّ بِإِذْنِ اللهِ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمْ وَلاَ يَنْفَعُهُمْ وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الآخِرَةِ مِنْ خَلاَقٍ وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْا بِهِ أَنْفُسَهُمْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ. وَلَوْ أَنَّهُمْ آمَنُوا وَاتَّقَوْا لَمَثُوبَةٌ مِنْ عِنْدِ اللهِ خَيْرٌ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ﴾.

“Wakafuata yale waliyoyafuata mashetani, (wakadai kuwa yalikuwa) katika ufalme wa (Nabii) Suleiman; na Suleiman hakukufuru, bali mashetani ndio waliokufuru, wakiwafundisha watu uchawi (waliokuwa wakiujuwa wenyewe tangu zamani), na (uchawi) ulioteremshwa kwa Malaika wawili, Haruta na Maruta, katika (mji wa) Babil. Wala (Malaika hao) hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: ‘Sisi ni mtihani (wa kutazamwa kutii kwenu); basi usikufuru. ‘Wakajifunza kwao ambayo kwa mambo hayo waliweza <u>kumfarikisha mtu na mkewe</u> (na mengineyo). Wala hawakuwa wenye kumdhuru yeyote kwa hayo ela kwa Idhini ya Allâh. Na wanajifunza ambayo yatawadhuru wala hayatawafaa. Kwa yakini wanajua kwamba aliyekhiyari haya hatakuwa na sehemu yoyote katika Akhira. Bila shaka ni kibaya kabisa walichouzia (starehe za) nafsi zao (za Akhira). Laiti wangalijua, (wasingefanya hivi).” [2: 102, 103].

عَنْ جَابِرٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ

Jâbir ﵁ amesimulia: “Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema: **“ibilisi**

hukiweka kiti chake juu ya maji, kisha akavituma vikosi vyake. Basi mwenye cheo cha karibu zaidi naye ni yule mwenye fitina kubwa zaidi. Mmoja wao huja na kusema: "Nimefanya kadha na kadha." Yeye humwambia: "Hujafanya kitu!" Kisha huja mwingine akasema: "Sikumwacha (Mwanaadamu) mpaka nimemfarikisha yeye na mkewe." Basi hapo humkaribisha kwake na akimwambia: "wewe ni askari mzuri sana!" al-A'mash amesema: "Nadhani alisema: **"… basi huwa naye."** [Muslim (17/157 *Nawawy*)].

عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ﴿إِنَّ إِبْلِيسَ يَضَعُ عَرْشَهُ عَلَى الْمَاءِ ثُمَّ يَبْعَثُ سَرَايَاهُ فَأَدْنَاهُمْ مِنْهُ مَنْزِلَةً أَعْظَمُهُمْ فِتْنَةً يَجِيءُ أَحَدُهُمْ فَيَقُولُ: فَعَلْتُ كَذَا وَكَذَا فَيَقُولُ مَا صَنَعْتَ شَيْئًا. قَالَ ثُمَّ يَجِيءُ أَحَدُهُمْ فَيَقُولُ مَا تَرَكْتُهُ حَتَّى فَرَّقْتُ بَيْنَهُ وَبَيْنَ امْرَأَتِهِ قَالَ فَيُدْنِيهِ مِنْهُ وَيَقُولُ نِعْمَ أَنْتَ﴾. قَالَ الأَعْمَشُ أُرَاهُ قَالَ: ﴿فَيَلْتَزِمُهُ﴾.

*** *Taarifa yake*:**
Ni amali ya sihiri ya kufarikisha baina ya wanandoa, au kueneza chuki na bughudha baina ya marafiki au washirika n.k.

*** *Aina zake*:**
1. Kufarikisha baina ya mtu na mama yake.
2. Kufarikisha baina ya mtu na baba yake.
3. Kufarikisha baina ya mtu na nduguye.
4. Kufarikisha baina ya mtu na rafiki yake.
5. Kufarikisha baina ya mtu na mshirika wake katika biashara au jambo lingine.
6. Kufarikisha baina ya mtu na mkewe, na aina hii ndio hatari zaidi na ndio iliosambaa mno.

*** *Dalili za sihiri ya kufarakisha*:**
1. Kwa ghafla hali hubadilika kutoka katika mapenzi hadi katika bughudha.
2. Kuwa na shaka nyingi baina yao.

3. Kutopeana nyudhuru.
4. Kuzikuza sababu za khitilafu hata kama ni ndogo.
5. Kubadilika sura ya mwanamume machoni mwa mkewe na kubadilika sura ya mke machoni mwa mumewe. Mwanamume humuona mkewe katika mandhari mbaya – hata kama ni mzuri kiasi gani – na uhakika ni kwamba, shetani aliyewakilishwa kwa sihiri hii, yeye ndiye anayesawirisha usoni mwake sura mbaya, na mwanamke naye humuona mumewe katika mandhari yanayohofisha na kutia woga.
6. Aliyesihiriwa huichukia kila amali inayotendwa na upande mwingine.
7. Aliyesihiriwa hupachukia mahali alipoketi mwenziwe. Utamuona mwanamume anapokuwa nje ya nyumba yupo katika hali nzuri ya kinafsi, lakini aingiapo nyumbani husikia dhiki kubwa ya kinafsi.

al-Hâfidh Ibnu Kathîr رحمه الله تعالى amesema: "Sababu ya kufarikisha baina ya wanandoa kwa sihiri, ni vile anavyosawirisha mwanamume au mwanamke mandhari au tabia mbaya ya mwenzie, au mfano wa hayo miongoni mwa sababu zinazopelekea kufarikiana." [*Tafsîr Ibnu Kathîr* (1/144)].

**** Sihiri hutokezeaje?***

Mtu humwendea mchawi[1] na akamtaka afarikishe baina ya fulani na mkewe. Mchawi naye humtaka ampe jina la mwanamume anayekusudiwa na jina la mama yake, na hutaka mojawapo ya athari zake (nywele, nguo, kofia n.k.), asipovipata hivyo, humfanyia sihiri katika maji - kwa mfano - na humwamuru ayamwage katika njia ya anayekusudiwa, basi anapoyakanyaga tu huwa ameshasibiwa na sihiri; au amwekee katika chakula au kinywaji [hali hii ni ikiwa jamaa huyo hakujikinga na nyuradi za asubuhi na jioni na dua za Mtume zinazomkinga mtu na sihiri].

---

[1] Kumbuka tena, katika miji hii kama vile Mombasa, baadhi ya wanaotenda matendo haya huwa hawaitwi wachawi, bali huitwa *waalimu; Maalim Fulani*, nao pia huingia katika mas'ala haya ya uchawi. Hawajali wanachotenda hata kama kinakhalifu Sharia, bora pesa mkononi.

**** Tiba*:**

Tiba huwa ni kwa mihula mitatu:

* ***Muhula wa kwanza*:** muhula kabla ya tiba, nao:

1. Kuandaa mazingira sahihi ya kiimani, aziondoe picha zote zilizopo katika nyumba anayofanyiwa tiba ili Malaika waweze kuingia.
2. Mgonjwa kutoa vihirizi, hijabu na kago na kuzichoma.
3. Pasiwepo nyimbo (mziki) na mazumari.
4. Pasiwepo na uhalifu wa Sharia kama vile mwanamume kuvaa dhahabu, au mwanamke asiyejisitiri, au mtu kuvuta sigara.
5. Kumpa mgonjwa na jamaa zake darasa juu ya Imani inayomhusu na inayoepusha nyoyoni mwao kufungamana na asiyekuwa Allâh.
6. Kuichunguza hali kwa kumwuliza mgonjwa baadhi ya maswali ili apate hakika kutokana na dalili zote au nyingi, kwa mfano:

a) Je, mara nyingine wamuona mumeo kwa mandhari mbaya?

b) Huwa munakosana kwa mambo madogo?

c) Je, huwa una wasaa unapokuwa nje ya nyumba lakini uingiapo nyumbani wasikia dhiki za kinafsi?

d) Je, mmoja kati ya wanandoa huona dhiki wakati wa kujamiiana?

e) Je, mmoja wenu huwa akipata hamaniko na wasiwasi usingizini mwake au huona ndoto za kutisha?

Utaendelea kumwuliza maswali, iwapo atakuwa ana dalili mbili au zaidi, utaendelea kumtibu.

7. Utatawadha kabla ya kuanza tiba na utamwamuru aliye nawe naye atawadhe.
8. Mgonjwa akiwa ni mwanamke, usianze kumtibu mpaka umheshimu na umfunge nguo zake ili asiwe uchi wakati wa kutibu.
9. Usimtibu mwanamke ilihali amevaa nguo kinyume na Sharia, kama vile akiwa ameufunua uso wake, au amejipaka manukato, au akiwa amepaka rangi ya kucha kujifananisha na makafiri.
10. Usimtibu mwanamke ela awepo mmojawapo katika maharimu zake.
11. Asiingie pamoja nawe yeyote ispokuwa maharimu wake.
12. Jiepushe na hila na nguvu zako na uombe msaada kwa Allâh Mtukufu.

* ***Muhula wa pili*****:** kutibu

Mkono wako utauweka juu ya kichwa cha mgonjwa, na utasoma zunguo hili sikioni mwake kwa makini [Tazama vizuri zunguo hili, kwani mara nyingi nitakuwa nikikurejesha ulisome]:

١. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ مِنْ هَمْزِهِ وَنَفْخِهِ وَنَفْثِهِ. ﴿بِسْمِ اللهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ. الحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ. الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ. مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ. إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ. اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ. صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ المَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلاَ الضَّالِّينَ﴾.

٢. ﴿بِسْمِ اللهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ. الـم. ذَلِكَ الْكِتَابُ لاَ رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِلْمُتَّقِينَ. الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ وَيُقِيمُونَ الصَّلاَةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ. وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ وَبِالآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ. أُولَئِكَ عَلَى هُدًى مِنْ رَبِّهِمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ.﴾

٣. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿وَاتَّبَعُوا مَا تَتْلُو الشَّيَاطِينُ عَلَى مُلْكِ سُلَيْمَانَ وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أُنْزِلَ عَلَى الْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ هَارُوتَ وَمَارُوتَ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولاَ إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلاَ تَكْفُرْ فَيَتَعَلَّمُونَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهِ وَمَا هُمْ بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلاَّ بِإِذْنِ اللهِ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمْ وَلاَ يَنْفَعُهُمْ وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الآخِرَةِ مِنْ خَلاَقٍ وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْا بِهِ أَنْفُسَهُمْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ﴾. [2:102] Aya hii utaikariri mara nyingi

٤. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿وَإِلَهُكُمْ إِلَهٌ وَاحِدٌ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ. إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ وَاخْتِلاَفِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنْفَعُ النَّاسَ وَمَا أَنْزَلَ اللهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ مَاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ وَتَصْرِيفِ الرِّيَاحِ وَالسَّحَابِ الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالأَرْضِ لآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ﴾ [2:163,164].

٥. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿اللهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لاَ تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلاَ نَوْمٌ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي اللأَرْضِ مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلاَّ بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلاَ يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِنْ عِلْمِهِ إِلاَّ بِمَا شَاءَ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضَ وَلاَ يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ﴾ .[2:255]

٦. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ آمَنَ بِاللهِ وَمَلاَئِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لاَ نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ. لاَ يُكَلِّفُ اللهُ نَفْسًا إِلاَّ وُسْعَهَا لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ رَبَّنَا لاَ تُؤَاخِذْنَا إِنْ نَسِينَا أَوْ أَخْطَأْنَا رَبَّنَا وَلاَ تَحْمِلْ عَلَيْنَا إِصْرًا كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِنَا رَبَّنَا وَلاَ تُحَمِّلْنَا مَا لاَ طَاقَةَ لَنَا بِهِ وَاعْفُ عَنَّا وَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا أَنْتَ مَوْلاَنَا فَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ﴾ .[2:285,286]

٧. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿شَهِدَ اللهُ أَنَّهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ وَالْمَلاَئِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ. إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللهِ الإِسْلاَمُ، وَمَا اخْتَلَفَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلاَّ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ وَمَنْ يَكْفُرْ بِآيَاتِ اللهِ فَإِنَّ اللهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ﴾..[3:18,19]

٨. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿إِنَّ رَبَّكُمُ اللهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَى عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ أَلاَ لَهُ الْخَلْقُ وَالأَمْرُ تَبَارَكَ اللهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ. ادْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً إِنَّهُ لاَ يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ. وَلاَ تُفْسِدُوا فِي الأَرْضِ بَعْدَ إِصْلاَحِهَا وَادْعُوهُ خَوْفًا وَطَمَعًا إِنَّ رَحْمَةَ اللهِ قَرِيبٌ مِنَ الْمُحْسِنِينَ﴾.[7:54-56]

٩. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿وَأَوْحَيْنَا إِلَى مُوسَى أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ. فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ. فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَاغِرِينَ. وَأُلْقِيَ السَّحَرَةُ سَاجِدِينَ. قَالُوا آمَنَّا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ. رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ﴾..[7:117-122]

١٠. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿قَالَ مُوسَى مَا جِئْتُمْ بِهِ السِّحْرُ إِنَّ اللهَ سَيُبْطِلُهُ إِنَّ اللهَ لاَ يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ. وَيُحِقُّ اللهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ﴾ [10: 81, 82]

Utaikariri Aya hii, hasa kipande hiki: ﴿إِنَّ اللهَ سَيُبْطِلُهُ﴾.

١١. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سَاحِرٍ وَلاَ يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَى﴾..[20:69]. Aya hii utaikariri mara nyingi.

١٢. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لاَ تُرْجَعُونَ. فَتَعَالَى اللهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ. وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللهِ إِلَهًا آخَرَ لاَ بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ إِنَّهُ لاَ يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ. وَقُلْ رَبِّ اغْفِرْ وَارْحَمْ وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ﴾. [23: 115, 118].

١٣. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. بِسمِ اللهِ الرَّحمنِ الرَّحيمِ. ﴿وَالصَّافَّاتِ صَفًّا. فَالزَّاجِرَاتِ زَجْرًا. فَالتَّالِيَاتِ ذِكْرًا. إِنَّ إِلَهَكُمْ لَوَاحِدٌ. رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَرَبُّ الْمَشَارِقِ. إِنَّا زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِزِينَةٍ الْكَوَاكِبِ. وَحِفْظًا مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ مَارِدٍ. لاَ يَسَّمَّعُونَ إِلَى الْمَلَإِ الأَعْلَى وَيُقْذَفُونَ مِنْ كُلِّ جَانِبٍ. دُحُورًا وَلَهُمْ عَذَابٌ وَاصِبٌ. إِلاَّ مَنْ خَطِفَ الْخَطْفَةَ فَأَتْبَعَهُ شِهَابٌ ثَاقِبٌ﴾. [37: 1-10].

١٤. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ
فَلَمَّا حَضَرُوهُ قَالُوا أَنْصِتُوا فَلَمَّا قُضِيَ وَلَّوْا إِلَى قَوْمِهِمْ مُنْذِرِينَ. قَالُوا يَا قَوْمَنَا إِنَّا سَمِعْنَا كِتَابًا
أُنْزِلَ مِنْ بَعْدِ مُوسَى مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ وَإِلَى طَرِيقٍ مُسْتَقِيمٍ. يَا قَوْمَنَا
أَجِيبُوا دَاعِيَ اللهِ وَآمِنُوا بِهِ يَغْفِرْ لَكُمْ مِنْ ذُنُوبِكُمْ وَيُجِرْكُمْ مِنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ. وَمَنْ لاَ يُجِبْ
دَاعِيَ اللهِ فَلَيْسَ بِمُعْجِزٍ فِي الأَرْضِ وَلَيْسَ لَهُ مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءُ أُولَئِكَ فِي ضَلاَلٍ مُبِينٍ﴾.
[46: 29-32].

١٥. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ وَالإِنْسِ إِنِ اسْتَطَعْتُمْ أَنْ تَنْفُذُوا مِنْ
أَقْطَارِ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ فَانْفُذُوا لاَ تَنْفُذُونَ إِلاَّ بِسُلْطَانٍ. فَبِأَيِّ آلاَءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ. يُرْسَلُ
عَلَيْكُمَا شُوَاظٌ مِنْ نَارٍ وَنُحَاسٌ فَلاَ تَنْتَصِرَانِ. فَبِأَيِّ آلاَءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ﴾. [55:33-36].

١٦. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. ﴿لَوْ أَنْزَلْنَا هَذَا الْقُرْآنَ عَلَى جَبَلٍ لَرَأَيْتَهُ خَاشِعًا
مُتَصَدِّعًا مِنْ خَشْيَةِ اللهِ وَتِلْكَ الأَمْثَالُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ. هُوَ اللهُ الَّذِي لاَ إِلَهَ
إِلاَّ هُوَ عَالِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ. هُوَ اللهُ الَّذِي لاَ إِلَهَ إِلاَّ هُوَ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ
السَّلاَمُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَيْمِنُ الْعَزِيزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ سُبْحَانَ اللهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ. هُوَ اللهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ
الْمُصَوِّرُ لَهُ الأَسْمَاءُ الْحُسْنَى يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ﴾.
[59:21-24].

١٧. أَعُوْذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. بِسمِ اللهِ الرَّحمنِ الرَّحيمِ. ﴿قُلْ أُوحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ
نَفَرٌ مِنَ الْجِنِّ فَقَالُوا إِنَّا سَمِعْنَا قُرْآنًا عَجَبًا. يَهْدِي إِلَى الرُّشْدِ فَآمَنَّا بِهِ وَلَنْ نُشْرِكَ بِرَبِّنَا أَحَدًا.
وَأَنَّهُ تَعَالَى جَدُّ رَبِّنَا مَا اتَّخَذَ صَاحِبَةً وَلاَ وَلَدًا. وَأَنَّهُ كَانَ يَقُولُ سَفِيهُنَا عَلَى اللهِ شَطَطًا. وَأَنَّا
ظَنَنَّا أَنْ لَنْ تَقُولَ الإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَى اللهِ كَذِبًا. وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِنَ الإِنْسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ
مِنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا. وَأَنَّهُمْ ظَنُّوا كَمَا ظَنَنْتُمْ أَنْ لَنْ يَبْعَثَ اللهُ أَحَدًا. وَأَنَّا لَمَسْنَا السَّمَاءَ

فَوَجَدْنَاهَا مُلِئَتْ حَرَسًا شَدِيدًا وَشُهُبًا. وَأَنَّا كُنَّا نَقْعُدُ مِنْهَا مَقَاعِدَ لِلسَّمْعِ فَمَنْ يَسْتَمِعِ الْآنَ يَجِدْ لَهُ شِهَابًا رَصَدًا﴾. [72: 1-9].

١٨. أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. بِسمِ اللهِ الرَّحمنِ الرَّحِيمِ. ﴿قُلْ هُوَ اللهُ أَحَدٌ. اللهُ الصَّمَدُ. لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ. وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ﴾. [112].

١٩. أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. بِسمِ اللهِ الرَّحمنِ الرَّحِيمِ. ﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ. مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ. وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ. وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ. وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ﴾. [113].

Utaikariri mara nuingi Aya hii: ﴿وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ﴾.

٢٠. أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ. بِسمِ اللهِ الرَّحمنِ الرَّحِيمِ. ﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ. مَلِكِ النَّاسِ. إِلَهِ النَّاسِ. مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ. الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ. مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ﴾. [114].

Baada ya kusoma zunguo hili sikioni mwa mgonjwa kwa makini na sauti ya juu, atakuwa baina ya hali tatu:

Hali ya kwanza: Ima mgonjwa atapandwa na jini aliyewakilishwa kwa sihiri, na atazungumza kwa ulimi wa mgonjwa; basi hapo utaamiliana na jini huyu kama unavyofanya wakati mtu anapoguswa na jini. Na nimeelezea jambo hilo kwa tafsili katika kitabu *Wiqâyatul-Insân, Minaljinni Wash-shaiṯân,*" (Kinga ya Mwanaadamu Dhidi ya Jini na shetani), kwa hivyo sitoitaja humu ili kitabu kisiwe kirefu.

Lakini utamwuliza jini huyu maswali mengi:

1. "Jina lako ni nani? Una dini gani?" Na hapo utaamiliana naye kulingana na dini yake. Akiwa si Muislamu, utamweleza asilimu, na akiwa ni Muislamu, utambainishia kuwa anayofanya katika kumtumikia mchawi ni kinyume na Uislamu na haijuzu.

2. Utamwuliza mahala ilipo sihiri. Lakini usimsadiki mpaka ubainikiwe na ukweli wake. Lau atakwambia: "Sihiri ipo mahali kadha," utamtuma mtu akaitoe, akiipata itakuwa ni kweli, la sivyo basi jini huyo ni muongo, kwa sababu majini wana uwongo mwingi.

3. Utamwuliza kuwa yuko peke yake aliyewakilishwa kwa sihiri au yuko na wengine? Iwapo yuko na wengine, utamtaka awalete, na umfahamu kama tulivyoeleza katika *Wiqâyatul-Insân, Minaljinni Wash-shaiṯân.* Fasili ya Pili.

4. Mara nyingine jini hukwambia: "(Mtu) fulani ndiye aliyekwenda kwa mchawi na akamtaka aifanye sihiri hii." Katika hali hii usimsadiki jini, kwa sababu yeye hutaka kutia uadui baina ya watu, na ushahidi wake ki-Sharia hurudishwa haukubaliwi, kwa sababu yeye ni fasiki, na ufasiki wake uko wazi kwa kuwa yuwamtumikia mchawi. Allâh Amesema:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَأٍ فَتَبَيَّنُوا أَنْ تُصِيبُوا قَوْمًا بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوا عَلَى مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِينَ﴾.

"Enyi mlioamini! Fasiki akiwajia na habari (yoyote ile), basi ipelelezeni (kwanza), msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda." [49: 6].

5.

Iwapo jini ataeleza mahala ilipo sihiri na mkaitoa, basi utayachukua maji na uyasomee Aya hizi:

﴿وَأَوْحَيْنَا إِلَى مُوسَى أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ. فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ. فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَاغِرِينَ. وَأُلْقِيَ السَّحَرَةُ سَاجِدِينَ. قَالُوا آمَنَّا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ. رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ﴾.[7:117-122]

﴿قَالَ مُوسَى مَا جِئْتُمْ بِهِ السِّحْرُ إِنَّ اللهَ سَيُبْطِلُهُ إِنَّ اللهَ لاَ يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ. وَيُحِقُّ اللهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ﴾. [10:81,82]

﴿إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سَاحِرٍ وَلاَ يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَى﴾. [20:69]

Utazisoma Aya hizo katika maji kwa namna ambayo pumzi unazosomea Qur'âni zinateremkia kwenye maji, halafu utaiyeyusha sihiri hii ya karatasi au manukato au kitu kingine katika maji haya. Kisha utayamwaga maji haya mahali mbali na njia wapitiazo watu.

Yule jini akisema kuwa aliyesihiriwa ameinywa sihiri, basi utamwuliza mgonjwa iwapo yuwahisi maumivu mengi tumboni, ikiwa yuwahisi, basi jini amesema kweli, kinyume chake ni uwongo.

Ukweli wa jini ukibainika, utaafikiana naye amtoke mgonjwa wala asimrudie, na wewe utaibatilisha sihiri Inshâ-allâh, halafu utayasomea maji Aya zilizotangulia mbele kidogo na utaongezea Aya ya 120 ya *Sûratul-Baqarah*. Halafu aliyesihiriwa atayanywa na kuogea siku kadhaa. [Aya hizi tumezichagua kutokana na jitihada zetu tu].

Iwapo jini atasema kuwa aliyesihiriwa ameikanyaga sihiri au amefanyiwa katika mojawapo ya athari zake (nywele, nguo n.k.), katika hali hii utamsomea Aya – zilizotangulia – katika maji, atakunywa na ataogea kwa muda wa siku kadhaa nje ya choo, na maji yale yatamwagwa njiani au mahala popote pasipokuwa chooni mpaka maumivu yatakapoisha.

Halafu utamwamuru jini atoke wala asirudi mara nyingine, atatoa ahadi (ya kutorudi), na umwamuru atoke. [Ahadi yenyewe imetajwa katika *Wiqâyatul-Insân, Minaljinni Wash-shaitân,* au kwa lafdhi yoyote nyingine inayokubalika ki-Sharia].

Halafu mgonjwa akupitie baada ya wiki moja, na utamsomea zunguo kwa mara nyingine. Asipohisi kitu, basi sihiri – *Alhamdulillâh* – imekwisha, na ikiwa atapandwa kwa mara ya pili, basi jini ni muongo na wala hakutoka. Utamwuliza sababu ya kutotoka na uamiliane naye kwa upole, akikubali basi *Alhamdulillâh*, akikataa basi ni kipigo na kila aina ya adhabu. Na iwapo hakupandwa na jini lakini akahisi kisunzi, kutetemeka au jambo lingine, utampa kanda (kaseti) iliyorekodiwa *Âyatul-Kursy* iliyokaririwa kwa muda wa saa moja, ataisikiliza kwa kipokea sauti cha masikioni (*headphone*) mara tatu kwa siku kwa muda

wa mwezi mmoja kamili, halafu baada ya mwezi akupitie ili umsomee, na hapo Inshâ-allâh atakuwa ameshapona. Ikiwa bado hajapona, utamrekodia *Sûratus-Sâffâti*, *Yâsîn*, *ad-Dukhân* na *al-Jinni* katika kanda, atakuwa akiisikiliza mara tatu kwa siku kwa muda wa wiki tatu**,** basi kwa Idhini ya Allâh atapona. Na ikiwa bado hajapona (jini amekua sugu), utaongeza muda.

Hali ya pili: wakati wa kuzunguliwa mgonjwa ahisi kisunzi, kutetemeka au kuumwa sana na kichwa, lakini hapandwi na jini. Katika hali hii, utalikariri zunguo mara tatu, akipandwa utamfanyia kama ilivyo katika *hali ya kwanza*, asipopandwa lakini kutetemeka na maumivu ya kichwa yanapungua na kutulia, utamsomea zunguo masiku kadhaa na atapona kwa Idhini ya Allâh.

Kama hajapona kabisa, utafanya hivi:

1. Utamrekodia *Sûratus-sâffâti* yote mara moja na *Âyatul-Kursy* iliyokaririwa mara nyingi katika kanda na aisikilize mara tatu kila siku.
2. Ahifadhi Swala za jamaa.
3. Baada tu ya Swala ya alfajiri aseme: mara mia (100)

﴿لاَ إِلـهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَ لَهُ الحَمْدُ وَ هُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ﴾.

Lâ ilâha illallâhu wahdahû lâ sharîka lah, lahulmulku walahulhamdu wahuwa 'alâ kulli shay-in qadîr.[1]

kwa muda wa mwezi mmoja, pamoja na kufahamu kuwa, maumivu yatamzidi katika siku kumi za mwanzo au siku 15 kila siku takriban, halafu yataanza kupungua kidogo kidogo, mwisho wa mwezi yatakuwa yameisha kabisa. Wakati huo utamsomea, wala hatahisi chochote Inshâ-allâh na sihiri itakuwa imeshabatilika.

Huenda maumivu yakaendelea mwezi wote pamoja na kuhisi dhiki nyingi kifuani, wakati huo utamsomea zunguo mara kadhaa na atapandwa na jini Inshâ-allâh halafu utafanya kama tulivyoeleza katika *hali ya kwanza*.

---

(1) Hakuna mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allâh Peke Yake, Ufalme ni Wake na Himdi zote ni Zake, Naye ni Muweza juu ya kila kitu.

Hali ya tatu: mgonjwa asihisi kitu wakati anapozunguliwa. Wakati huo utamwuliza kuhusu dalili kwa mara nyingine, ukiona dalili si za kutosha, mtu huyu hakusihiriwa wala si mgonjwa, na waweza ukazidi kuyakinisha kwa kumzungua mara tatu. Iwapo dalili ziko za kutosha na ukamkariria zunguo wala asihisi kitu – ingawaje hili ni nadra sana – utampa yanayofwatia:

1. Utamrekodia *Sûratu Yâsîn*, *Dukhân* na *al-Jinni* katika kanda, awe akiisikiliza mara tatu kila siku.
2. Kukithirisha kuleta istighfari mara mia (100) au zaidi, kila siku.
3. Kukithirisha kusema: لاَحَوَلَ وَلاَ قُوَّةَ إِلاَّ بِاللهِ mara mia (100) au zaidi kila siku. Yote hayo ni kwa kipindi cha mwezi mmoja, halafu utamsomea zunguo na utamfanyia kama ilivyo katika *hali ya kwanza* na *hali ya pili*.

* ***Muhula wa tatu katika mihula ya tiba*****:** Muhula baada ya tiba.
Allâh Atakapomponya mikononi mwako na akajisikia mzima wa afya, (usijinaki na ukasema "mimi… mimi", bali) utamhimidi Allâh Mtukufu Aliyekuafikia katika hilo, na uzidi mazidada kumuhitajia Yeye ili upate kuafikiwa katika hali nyinginezo, wala isiwe ndio sababu ya wewe kupotea na kutakabari,

﴿وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِنْ شَكَرْتُمْ لأَزِيدَنَّكُمْ وَلَئِنْ كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ﴾.

"(Kumbukeni) Alipotangaza Mola wenu (kuwa) "Mukishukuru, Nitawazidishia; na mukikufuru (jueni kuwa) adhabu Yangu ni kali sana." [14: 7].

Katika kipindi hiki, huyu aliyeaguliwa yupo katika hali ya kuweza kufanyiwa tena sihiri. Kwa sababu wengi katika wanaofanya sihiri wanapofahamu kuwa yule mgonjwa alikwenda kwa tabibu kwa ajili ya tiba, wao humrudia tena mchawi ili awafanyie tena sihiri kwa mara nyingine. Kwa hivyo mgonjwa atakiwa asimweleze yeyote.

Lakini kwa vyovyote vile, utampa kinga hizi:
1. Kudumu katika Swala za jamaa.

2. Kutosikiliza muziki na nyimbo.
3. Kutawadha kabla ya kulala, na atasoma *Âyatul-Kursy*.
4. Kupiga *Bismillâhi* katika kila jambo.
5. Baada ya Swala ya alfajiri aseme mara mia (100):

﴿لاَ إِلـهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَ لَهُ الحَمْدُ وَ هُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ﴾.

Lâ ilâha illallâhu wahdahû lâ sharîka lah, lahulmulku walahulhamdu wahuwa 'alâ kulli shay-in qadîr.[1]

6. Asipitiwe na siku ela awe amesoma sehemu katika Qur'âni, au asikilize iwapo hajui kusoma.
7. Kusuhubiana (kuandamana) na watu wema.
8. Kudumu kuzisoma nyuradi za asubuhi na jioni.

*****

SAMPULI YA KIUTENDAJI YA KUTIBU SIHIRI YA KUFARIKISHA

Sampuli Ya Kwanza

Jini Anayeitwa Shaqwân

Mwanamke huyu alikuwa akimchukia mumewe chuki kubwa. Dalili za sihiri zilikuwa zimejitokeza wazi, hata alikuwa akiona dhiki nyumbani mwa mumewe, bali hata akimwonea dhiki mumewe pia. Alikuwa akimuona mumewe katika mandhari ya kuogofya na kutisha, kana kwamba ni mnyama mwitu.

Halafu mumewe akaenda naye kwa tabibu wa Qur'âni. Jini akazungumza kuwa yeye amekuja kwa njia ya sihiri, na kazi yake ni kufarikisha baina ya mume huyu na mkewe. Yule tabibu akampiga sana. Lakini hakusikia. Mumewe akanieleza kuwa, yeye alikuwa akienda kwa tabibu huyu na mkewe kwa muda wa mwezi. Mwishowe jini akamtaka amwache mkewe japo talaka moja. Na kwa masikitiko, yule bwana akakubali na akamwacha talaka moja, halafu akamrejea, yule mwanamke akapona muda wa wiki moja, halafu akamrudia tena. Yule

---

(1) Hakuna mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allâh Peke Yake, Ufalme ni Wake na Himdi zote ni Zake, Naye ni Muweza juu ya kila kitu.

bwana akanijia na mkewe, nilipomsomea Qur'âni, jini alipanda na tukajadiliana kama hivi nitakavyoeleza kwa ufupi.

= nilimwuliza: Nani jina lako?
- akajibu: Shaqwân.
= una dini gani?
- ni Mkristo.
= kwa nini umemwingia mwanamke huyu?
- ili nifarikishe baina yake na mumewe.
= nitakwambia jambo, ukikubali basi *Alhamdulillâh*, la si hivyo basi una hiyari.
- usijisumbue, mimi sitamtoka, kwani ameenda naye kwa fulani na fulani.
= sijakutaka umtoke.
- kwa hivyo watakaje?
= nataka usilimu, ukikubali basi *Alhamdulillâh*, la si hivyo hakuna kulazimishana katika Dini.

Halafu nikamwelezea Uislamu, na baada ya mjadala mrefu akasilimu, *Alhamdulillâh*.

= je, umesilimu kiuhakika au watuhadaa?
- wewe huwezi kunilazimisha jambo, mimi nimesilimu moyoni mwangu lakini…
= nini?
- mbele yangu naona kundi la majini Wakristo wananitisha na naogopa wasije wakaniuwa.
= hili ni jambo dogo na rahisi, kama kweli itaonekana umesilimu moyoni mwako, tutakupa silaha ya nguvu, hakuna yeyote miongoni mwao awezaye kukusogelea.
- nipe sasa hivi.
= hapana, mpaka kikao kimalizike.
- wataka nini baada ya hapo?
= iwapo umesilimu kiuhakika na ili toba yako iwe imetimia kweli, basi ni uache dhuluma na umtoke mwanamke huyu.
- ndio, nimesilimu lakini nitawezaje kujinasua na mchawi?
= hili ni jambo rahisi lakini iwapo utaafikana nasi juu ya hilo.
- ndio.

= kwa hivyo sihiri iko wapi?
- katika ua la nyumba anapoishi mwanamke. Lakini siwezi kusema ni mahali gani hasa, kwa sababu huko kuna jini aliyewakilishwa kuilinda sihiri hii, na kila inapojulikana yeye huihamishia mahali pengine.
= tangu miaka mingapi washirikiana na mchawi huyu?
- yapata miaka kumi au ishirini (mimi mwandishi ndiye nimeghafilika kidogo) na nimewaingia wanawake watatu kabla ya mwanamke huyu.

Halafu akatutolea kisa cha wanawake hawa watatu.
= uliponidhihirikia ukweli wake, nilimwambia chukua silaha yako tuliokuahidi.'
- ni ipi?
= *Âyatul-Kursy*, kila unapokaribiwa na jini utamsomea, naye atakukimbia. Je umeihifadhi?
- ndio nimeihifadhi kutokana na mwanamke huyu kuikariri. Lakini vipi nitajinasua na mchawi?
= toka sasa uelekee Makka uishi huko katika Haram katikati ya majini Waumini.
- lakini je, Allâh Atanikubalia baada ya kufanya maasi yote haya? Nilimwadhibu sana mwanamke huyu, na niliwaadhibu wanawake niliowaingia kabla yake.
= ndio, Allâh Amesema:

﴿قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ لاَ تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللهِ إِنَّ اللهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ﴾.

"Sema: "Enyi waja Wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na rehma ya Allâh, bila shaka Allâh Husamehe dhambi zote; hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu." [39: 53].

Akalia kisha akasema:
- nitakapotoka, mtakeni mwanamke huyu anisamehe kwa kumwadhibu.

Halafu akaahidi na akatoka. Kisha nikayasomea maji Aya za Qur'âni nikampa yule mwanamume ayamimine katika ua la nyumba. Baada ya muda, yule bwana aliniletea salamu kuwa mkewe yu katika kheri, *Alhamdulillâh*. Mimi (mwandishi) sina chochote, mambo yote Anayo Allâh.

SAMPULI YA PILI
Jini Yuwaweka Sihiri Chini Ya Mto (Wa Kulalia)

[Pana uwezekano wa majini kubeba vitu, kwa dalili ya Kauli ya Allâh isemayo:

"… nani atakayeniletea kiti chake cha enzi kabla hawajakuja kwangu hali ya kuwa wamekwisha kusilimu? Mjasiri mmoja wa majini akasema: "Mimi <u>nitakuletea</u> kabla hujainuka mahali pako hapo …" [27: 38,39].

﴿أَيُّكُمْ يَأْتِينِي بِعَرْشِهَا قَبْلَ أَنْ يَأْتُونِي مُسْلِمِينَ. قَالَ عِفْرِيتٌ مِنَ الْجِنِّ أَنَا آتِيكَ بِهِ قَبْلَ أَنْ تَقُومَ مِنْ مَقَامِكَ﴾.

Mumewe alinijia akanambia: "Tangu nimuowe, tumo katika khitilafu kubwa, bali yuwanichukia sana, wala hawezi kunivumilia hata neno moja, yuwatamani kuniepuka na huwa starehe nyumbani maadamu mimi sipo, niingiapo husikia dhiki kana kwamba mwili wake unawaka moto kwa ghadhabu na hasira!"

Nilipomsikilizisha zunguo (yule mwanamke), alianza kuhisi vidole kufa ganzi, dhiki kifuani mwake na kuumwa na kichwa, lakini hakupandwa na jini. Nikampa Sura za Qur'âni zilizorekodiwa katika kanda na nikamwambia aisikilize kwa muda wa siku 45 halafu arudi. Baadaye muda huo kupita alikuja mumewe, akasema: "Pametokea jambo la ajabu!

Nikasema: "Kheri! Pametokea nini?"

Akasema: "Baada muda kupita na tukaafikiana tukujie, mke wangu alipandwa na jini, na jini akazungumza. Akasema: "Nitawaambia kila kitu kwa sharti msinipeleke kwa Sheikh. Mimi nimemjia kwa njia ya sihiri. Na mkitaka kujua ukweli wangu, leteni mto huu" akaashiria mto uliokuwepo chumbani "na muufungue mtakuta sihiri humo." Na kweli waliufungua mto na wakakuta ndani yake muna vipande vya vikaratasi vyenye maandishi na herufi. Halafu akawaambia: "Vichomeni vikaratasi hivi, sihiri imeshabatilika, nami nitamtoka wala sitomrudia kwa sharti

nimsimamie halafu nipeane naye mkono hivi sasa." Yule mumewe akamwambia jini hapana ubaya. Na kweli mwanamke aliinuka kutoka chini halafu akaunyoosha mkono wake kana kwamba yuwapeana mkono na mtu.

Aliponitolea kisa hiki, nilimwambia: "Lakini umekosea kumruhusu apeane mkono naye, kwa sababu jambo hili ni haramu wala halifai. Imethubutu kuwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amekataza mwanamume kupeana mkono na mwanamke ajinabi."

Baada ya wiki, yule mwanamke akaugua tena, akamleta tena, basi sikuimaliza *A'ûdhubillâhi* mwanamke akapanda jini, na tukajadiliana ifwatavyo:

= nikasema: ee kadhabu kwa nini umerejea tena?
- akasema: nitakwambia kila kitu lakini usinipige!
= sema!
- ndio, niliwadanganya, nami ndiye niliyeweka sihiri ndani ya mto ili wanisadiki na wala sikumtoka.
= kwa hivyo unawafanyia hila!
- nifanyeje nami nimefungwa mwilini mwake kwa sihiri?
= wewe ni Muislamu?
- ndio.
= haijuzu Muislamu kushirikiana na mchawi kwa sababu jambo hili ni haramu, na pia ni katika madhambi makubwa…je, wataka Pepo?
- ndio, naitaka.
= kwa hivyo utaachana na mchawi na utafwatana na Waumini umwabudu Allâh, kwa sababu njia ya mchawi ni njia ya uovu na mateso duniani na Akhera.
- lakini nitawezaje hivyo naye amenitawala?
= ndio, amekutawala kwa maasi yako. Lakini kama ungetubia kikwelikweli na ukarejea kwa Allâh Asingejaalia njia dhidi yako

﴿وَلَنْ يَجْعَلَ اللهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلاً﴾.

"Allâh Hatawajaalia makafiri njia ya kuwashinda Waumini." [4: 142].

- nimetubia kwa Allâh, nitatoka wala sitarudi tena.

Halafu akamuahidi Allâh Mtukufu na akatoka. *Alhamdulillâh*. Mumewe alinijia baada ya muda akinipa habari njema kuwa mkewe yu katika kheri.

*****

SAMPULI YA TATU

Hali Ya Mwisho Nilioitibu Kabla Ya Kuandika Kitabu Hiki

Mumewe alinijia akanambia: "Yeye (mke wangu) hunichukia wala hataki kuishi nami pamoja na kuwa nampenda. Chuki hii imekuja pasina kuwepo sababu!"

Yule (mwanamke) alipoisikia Qur'âni, alipandwa na jini, yakawepo majadiliano yafwatayo:

= nilimwuliza: ni Muislamu wewe?
- ndio, ni Muislamu.
= kwa nini umemwingia mwanamke huyu?
- nimekuja kwa njia ya sihiri. Fulani (mwanamke) ndiye aliyemfanyia sihiri na akaiweka katika kichupa cha manukato alichokuwa nacho, nami nilikuwa nikienda nyuma yake kwa muda. Halafu (siku moja) mwizi alipanda juu ya nyumba (akitaka kuiba), akafazaika nami nikamuingia.

Hapa yatakiwa nitanabahishe kuwa, mchawi humtuma jini kwa anayemkusudia kumsihiri, yule jini huwa akimfwata aliyekusudiwa kusihiriwa mpaka atakapopata fursa ya kumwingia, amwingie. Na fursa za majini ni nne:

1. wakati wa hofu nyingi.
2. hasira nyingi.
3. kughafilika mno.
4. kuyaelekea matamanio (ya maasi).

Basi mtu atapokuwa katika mojawapo ya hali hizo nne, shetani humakinika kumwingia, ispokuwa akimtaja Allâh au akawa ana udhu, hapo jini hawezi kumwingia. Na husemwa – kulingana na

nilivyoambiwa na majini wenyewe iwapo wamesema kweli – mtu akimtaja Mola wake wakati ule tu anapoingiwa na jini, jini huchomeka! Kwa hivyo wakati wa jini kumwingia mtu, ndio wakati mgumu zaidi katika maisha ya jini mwenyewe.
- mwanamke huyu masikini ni mwema.
= kwa hivyo utatoka kwa kumtii Allâh wala hutarudi.
- kwa sharti amtaliki yule mke mwingine.
= sharti yako haikubaliwi, ima utoke au tukudhuru.
- nitatoka!
Akatoka, *Alhamdulillâh*.

Halafu nikambainishia yule mwanamume kuwa yale maneno ya jini kuwa fulani (mwanamke) ndiye alimfanyia (mkeo) sihiri, hayakubaliki, na majini husema uwongo ili wafarikishe watu, mche Allâh wala usimsadiki.

SAMPULI YA NNE
Jini Ataka Kumwingia Tabibu

Mmoja katika matabibu wa Qur'âni alinambia: "Bwana mmoja alimleta mkewe, na akanieleza kuwa mkewe humchukia sana na husikia raha nisipokuwepo nyumbani."

Nilipomwuliza yule mwanamke dalili anazoziona, nikafahamu kuwa ana sihiri ya kufarikisha. Aliposikia zunguo, jini alizungumza na majadiliano yakawa kama hivi nitakavyoeleza kwa ufupi:
= nilimwuliza: nani jina lako?
- akajibu: sitakwambia jina langu.
= una dini gani?
- Uislamu.
= je, inajuzu Muislamu kumwadhibu Muislamu?
- mimi nampenda wala simwadhibu, lakini nataka awe mbali na mumewe.
= yaani unataka kuwatenganisha?
- ndio.
= si halali kwako kufanya hivyo, mtoke kwa kumtii Allâh.

- laa… laa…, mimi nampenda
= yeye anakuchukia.
- laa… yeye yuwanipenda.
= umesema uwongo, yeye amekuja hapa ili akutoe mwilini mwake.
- sitatoka!
= kwa hivyo nitakuchoma kwa Qur'âni – kwa Nguvu na Uwezo wa Allâh.

Nikamsomea Aya, akapiga mayowe.

= utatoka?
- ndio nitatoka lakini kwa sharti.
= sharti gani hilo?
- nitatoka kwake na nikuingie wewe.
= hakuna ubaya, toka kwake na uingie kwangu ukiweza.

Akangoja kidogo halafu akalia.

= nini kikulizacho?
- hakuna jini yeyote awezaye kukuingia leo!!
= kwa nini?
- kwa sababu wewe leo asubuhi umesoma mara mia (100):

﴿لاَ إِلـهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَ لَهُ الحَمْدُ وَ هُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ﴾.

Lâ ilâha illallâhu wahdahû lâ sharîka lah, lahulmulku walahulhamdu wahuwa 'alâ kulli shay-in qadîr.[1]

= Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema kweli aliposema: **"Atakayesema kila siku:**

﴿لاَ إِلـهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَ لَهُ الحَمْدُ وَ هُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ﴾.

Lâ ilâha illallâhu wahdahû lâ sharîka lah, lahulmulku walahulhamdu wahuwa 'alâ kulli shay-in qadîr.

mara mia (100), itakuwa ni sawa na kutoa watumwa kumi, ataandikiwa hasanati mia, atafutiwa mabaya mia na itakuwa ni hifadhi kwake kutokana na shetani mchana wake huo mpaka afike jioni. Wala hakuna yeyote aliyefanya jambo bora kuliko alilofanya yeye ispokuwa mtu aliyefanya kwa wingi zaidi yake." Bukhârî (6/338 *Fat-hi*) na Muslim (17/17 *Nawawy*)].

---

[1] Hakuna mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allâh Peke Yake, Ufalme ni Wake na Himdi zote ni Zake, Naye ni Muweza juu ya kila kitu.

- kwa hivyo ninamtoka.
Akaahidi akamtoka. Fadhla ni za Allâh.

*****

SIHIRI YA MAPENZI (*tiwalah)*

﴿إن الرُّقَى والتَّمائِم والتِّوَلة شرْك﴾.

Mtume صلى الله عليه وآله وسلم Amesema: **"Mazunguo, kago na *tiwalah* ni ushirikina."** [Ahmad (1/381), Abû Dâwûd (3883), Ibnu Mâjah (3530), al-Hâkim (4/418) na al- al-Albâny katika *Sahîhah* (331)].

Ibnul-Athîr amesema: "*Tiwalah:* ni kinachompendekezesha mwanamke kwa mumewe katika sihiri na mengineyo. Na (Mtume صلى الله عليه وآله وسلم) ameifanya ni katika ushirikina kwa kuitakidi kwao kuwa kitu hicho huathiri na hufanya kinyume cha Alivyokadiria Allâh." [*an-Nihâyah*: 1/200].

Napenda kutanabahisha kuwa, mazunguo yaliokusudiwa katika Hadîth iliyotangulia, ni mazunguo yalio na maneno ya kuomba msaada wa majini, mashetani na wengineo[1] yanayoingia katika ushirikina. Ama zunguo la Qur'âni, au dua na nyuradi za ki-Sharia, yote hayo yanajuzu kwa ijimai (itifaki) ya Wanazuoni wa Sharia. Imethubutu katika *Sahîh Muslim*, kuwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema: **"Mazunguo hayana ubaya maadamu si ushirikina."** [Muslim (14/187 *Nawawy*)].

**** Dalili za sihiri*:**

1. Mahaba na mapenzi yaliozidi.
2. Kupenda mno kujamii.
3. Kutoweza kuwa mbali naye.
4. Shauku nyingi ya kumuona.
5. Kumtii kiupofu.

---

[1] Kama vile kuyaomba mapepo ya jadi ya kina babu na babu ambayo yenyewe hayawezi kujisaidia achilia mbali kumsaidia mwingine.

**** Sihiri ya mapenzi hutokeaje?***

Mara nyingi hutokea khitilafu nyumbani baina ya mume na mke, lakini huisha haraka na maisha yakachukua mkondo wake kama kawaida. Lakini muna wanawake wasioweza kuvumilia hilo, huwa wakikimbilia kwa wachawi ili wawaekee sihiri itakayompendekezesha kwa mumewe. Jambo hili latokana na uchache wa Dini ya mwanamke, au hutokana na kutojua kuwa jambo hili ni haramu halifai. Basi hapo mchawi akataka mojawapo ya athari za mumewe (kitambaa, kofia, nguo, fulana n.k.) kwa sharti kiwe kimebeba harufu ya jasho la mumewe – yaani kisiwe ni kipya au kimefuliwa – bali kiwe kimeshatumiwa, halafu achukue baadhi ya nyuzi zake, azivuvie na afunge mafundo halafu anamwamuru aizike mahala palipohamwa. Au huwa akitaka amfanyie sihiri katika maji au chakula, na sihiri kali zaidi ni inayokuwa katika najisi, na kali kuliko hiyo ni inayokuwa kwa damu ya hedhi. Halafu humwamuru amwekee mumewe katika chakula chake, au kinywaji chake, au katika manukato yake.

**** Athari za kinyume za sihiri ya mapenzi*:**

1. Mara nyingine mwanamume huugua kwa sababu ya sihiri hii. Nilimjua mwanamume fulani aliugua miaka mitatu kwa sababu hiyo.
2. Mara nyingine sihiri hubadilika kinyume akawa anamchukia mkewe, na hili latokana na wachawi wengi kutofahamu misingi ya sihiri.
3. Mara nyingine mke humfanyia mumewe sihiri-mchanganyiko ili awachukie wanawake wote na ampende yeye pekee. Basi ikasababisha mume kumchukia mama yake, dada zake, shangazi zake, khalati zake (mama wadogo / wakubwa) na wote miongoni mwa jamaa zake miongoni mwa wanawake.
4. Wakati mwingine, sihiri-mchanganyiko hugeuka, mume akawachukia wanawake wote hata mkewe. Nami naijua hali kama hii, mwanamume akamchukia mkewe, akamtaliki. Yule mwanamke (mtaka yote aliyekosa yote) akaenda kwa mchawi mara ya pili ili amfungulie sihiri hii. Lakini alishtuka kukuta kuwa mchawi ameshakufa. (*Mchimba kisima huingia mwenyewe!*).

**** Sababu za sihiri ya mapenzi*:**

1. Mlipuko wa khitilafu baina ya wanandoa.

2. Tamaa ya mwanamke katika mali ya mwanamume hasa anapokuwa tajiri.
3. Mwanamke kuhisi kuwa mumewe huenda akaowa mwengine – pamoja na kuwa jambo hili linajuzu ki-Sharia – wala hakuna kasoro katika hilo, lakini mwanamke zama hizi (mwana-maendeleo!) – hasa walioathirika na vyombo vya habari vinavyoangamiza – hudhani kuwa mumewe atakapoowa mwengine, hii itakuwa ni dalili kuwa yeye hampendi, na hili ni kosa baya; kwa sababu muna sababu nyingi zinazomfanya mwanamume kumuowa mke wa pili, wa tatu na wa nne hata kama bado anampenda yule yule wa kwanza. Kwa mfano, kama ana raghba ya watoto wengi, kutoweza kuvumilia kutojimai wakati mkewe yu katika hedhi au nifasi, au ana raghba ya kukita mafungamano na familia fulani au mambo mengine mengi.

**** Sihiri iliyo halali*:**
Hii ni nasaha ninayompa mwanamke Muislamu, nayo ni kuwa, yeye aweza akamsihiri mumewe kama alivyohalalishiwa na Allâh kwa kujipamba sana mbele ya mumewe, jicho lake (mume) lisione kitu kibaya, wala asimnuse ela harufu nzuri, tabasamu inayong'aa, maneno mazuri, tangamano jema, kuyalinda mali ya mume, kuwachunga watoto na kuwahifadhi, kumtii yeye ela katika maasia.

Lakini lau tutazama katika jamii zetu leo, tutakuta mambo ni kinyume cha kushangaza katika mambo haya. Utamkuta mwanamke yuwajipamba vizuri kabisa na kuvaa mapambo alionayo na yuwatoka kana kwamba ni siku yake ya arusi, hali hii ni akiwa yuwaenda katika sherehe au kumzuru rafiki yake. Arudipo nyumbani mwake, huyaosha mapambo yake na huzivua nguo zake akaziweka mahali pake mpaka siku ya sherehe nyingine au ziara nyingine, na mumewe masikini aliyemnunulia nguo hizi na dhahabu zile, amenyimwa starehe hii, hamuoni mkewe nyumbani ela na nguo za zamani na hutoa harufu ya jikoni, kitunguusaumu na kitunguumaji (na hata kikwapa!).

Lau mwanamke atazingatia, angejua kuwa mumewe ndiye mwenye haki zaidi katika mapambo haya. Mumeo akienda kazini, harakisha kumaliza kazi za nyumbani halafu uwoge, ujipambe na umngoje, akija kutoka

kazini mwake, mbele yake amuone mke mzuri, chakula kimeshaandaliwa na nyumba iko safi; ili azidi kukupenda na kukushika vizuri; basi Wallahi hii ndio sihiri halali, hasa unaponuia kumtii Allâh kwa jambo hilo la kumpambia mume na kumsaidia macho yake yasitazame haramu, kwa sababu aliyeshiba hatamani chakula, bali anayekitamani na kukikodolea macho, ni aliye na njaa. Yazingatie maneno haya, yana thamani.

TIBA YA SIHIRI YA MAPENZI

1. Utamsomea mgonjwa zunguo nililotaja mbele kidogo, ispokuwa tu utaiondoa Aya ya 102 ya *Sûratul-Baqarah*, na mahala pake utaziweka Aya 14, 15, 16 za *Sûratut-Taghâbun*, nazo ni:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ مِنْ أَزْوَاجِكُمْ وَأَوْلاَدِكُمْ عَدُوًّا لَكُمْ فَاحْذَرُوهُمْ وَإِنْ تَعْفُوا وَتَصْفَحُوا وَتَغْفِرُوا فَإِنَّ اللهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ. إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلاَدُكُمْ فِتْنَةٌ وَاللهُ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ. فَاتَّقُوا اللهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَاسْمَعُوا وَأَطِيعُوا وَأَنْفِقُوا خَيْرًا لأَنْفُسِكُمْ وَمَنْ يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ﴾.

2. Aghlabu aliyesihiriwa aina hii ya sihiri huwa hapandi jini, bali husikia kufa ganzi katika viungo, au kuumwa na kichwa, au dhiki moyoni, au maumivu makali tumboni hasa iwapo ameinywa sihiri, na huenda akatapika.

Akihisi maumivu tumboni, au kutaka kutapika, msomee Aya hizi katika maji na umwambie ayanywe mbele yako, akitapika kitu rangi ya njano, au nyekundu, au nyeusi, sihiri itakuwa imeshabatilika *Walhamdu Lillâh*. Laa si hivyo, mwambie anywe maji haya wiki tatu au zaidi mpaka sihiri ibatilike.

Aya zenyewe ni hizi:

١. ﴿قَالَ مُوسَى مَا جِئْتُمْ بِهِ السِّحْرُ إِنَّ اللهَ سَيُبْطِلُهُ إِنَّ اللهَ لاَ يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ. وَيُحِقُّ اللهُ الحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ﴾. [10: 81,82].

٢. ﴿وَأَوْحَيْنَا إِلَى مُوسَى أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ. فَوَقَعَ الحَقُّ وَبطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ. فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَاغِرِينَ. وَأُلْقِيَ السَّحَرَةُ سَاجِدِينَ. قَالُوا آمَنَّا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ. رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ﴾. [7:117-122].

٣. ﴿إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سَاحِرٍ وَلاَ يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَى﴾. [20:69]

4. *Âyatul-Kursy*.

Aya hizi utazisoma katika maji. Mwanamume afahamu kuwa, tiba hii awe akimficha mkewe, kwa sababu lau atajua; huenda akamfanyia tena sihiri kwa mara nyingine.

*****

SAMPULI YA KIUTENDAJI YA KUITIBU SIHIRI YA MAPENZI
Mtu Anayeongozwa Na Mkewe

Bwana huyu alinijia akanambia kuwa, alikuwa ni mtu wa kawaida kwa mkewe, na yapata miezi kadhaa pametokea maajabu!

Anasema: siwezi kusubiri kuwa mbali na mke wangu hata dakika moja! Hata niwapo kazini, huwa nikimuwaza tu, na nirejeapo kutoka kazini nikaingia nyumbani, hukimbilia kumtazama ili nimuone. Ninapokuwa nina wageni sebuleni, kila mara huwaacha na nikaingia ndani ili nimuone. Namwonea wivu wa kupita hadi na mipaka usio kawaida, hujamiiana naye sana na amekuwa kana kwamba ndiye anayeniongoza; akiingia jikoni nami niko nyuma yake, akiingia chumba cha kulala niko nyuma yake, akisafisha na akifagia nyumba niko nyuma yake (kama mkia). Sijui ni jambo gani limenipata. Akiniomba jambo hata liweje, hukimbilia nimfanyie …

Nikamsomea Aya za Qur'âni katika maji. Nikamwambia anywe na aogee kwa muda wa wiki tatu halafu arudi bila yule mwanamke kufahamu. Baada ya muda kumalizika, alirudi akanieleza kuwa mambo

yamepungua, lakini hayajaisha kabisa. Nikamkaririia tiba. Basi *Al<u>h</u>amdulillâh*, mambo yakawa mazuri.

TATU: SIHIRI YA KUZUGA

Allâh Amesema:

"Wakasema: "Ewe Musa! Je, utatupa wewe (mbele ya watu waone) au tutakuwa sisi ndio watupao kwanza?" (Musa) akawaambia: "Tupeni." Basi walipotupa, <u>waliyazuga</u> macho ya watu na wakawaogopesha, wakaleta uchawi mkubwa. Tukampelekea Wahyi Musa ya kwamba, 'tupa fimbo yako.' Mara ikavimeza vyote vile walivyovibuni (wale wachawi). Ukweli ukasimama na yakaharibika waliyokuwa wakiyatenda. Kwa hivyo walishindwa hapo, na wakawa wenye kudhalilika. Wachawi wakapinduliwa (wakapinduka) wanasujudu. Wakasema: "Tumemwamini Mola wa viumbe vyote; Mola wa Mûsâ na Haruni." [7: 115-122].

﴿قَالُوا يَا مُوسَى إِمَّا أَنْ تُلْقِيَ وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ نَحْنُ الْمُلْقِينَ. قَالَ أَلْقُوا فَلَمَّا أَلْقَوْا سَحَرُوا أَعْيُنَ النَّاسِ وَاسْتَرْهَبُوهُمْ وَجَاءُوا بِسِحْرٍ عَظِيمٍ. وَأَوْحَيْنَا إِلَى مُوسَى أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ. فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ. فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَاغِرِينَ. وَأُلْقِيَ السَّحَرَةُ سَاجِدِينَ. قَالُوا آمَنَّا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ. رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ﴾.

Allâh Amesema:

"Wakasema: "Ewe Musa! Je! Utatupa wewe (kwanza) au tutakuwa sisi wa kwanza kutupa?". (Musa) akasema: "Bali tupeni (nyinyi kwanza)!" Tahamaki kamba zao na fimbo zao <u>zikaonekana</u> mbele yake (Musa) kwa uchawi wao,

﴿قَالُوا يَا مُوسَى إِمَّا أَنْ تُلْقِيَ وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَلْقَى. قَالَ بَلْ أَلْقُوا فَإِذَا حِبَالُهُمْ وَعِصِيُّهُمْ يُخَيَّلُ إِلَيْهِ مِنْ سِحْرِهِمْ أَنَّهَا تَسْعَى﴾.

zinakwenda mbio." [20: 65,66].

**** Dalili za sihiri ya kuzuga*:**

1. Mtu huona, kitu kinachotaharaki kimetulia, na kilichotulia kinataharaki.
2. Kidogo hukiona kikubwa, na kikubwa hukiona kidogo.
3. Huviona vitu katika hali isiyokuwa ya hakika, mithili watu walipoziona fimbo na kamba kuwa ni nyoka wanaotembea.

**** Hutokeaje sihiri ya kuzuga?***

Mchawi huleta kitu kinachojulikana na watu, halafu akasemasema maazima yake ya kiushirikina na matalasimu yake ya kiukafiri na akiwaomba msaada mashetani; basi watu wakaona mambo katika hali isiyokuwa hakika yake.

Nimehadithiwa na aliyemuona mchawi, aliweka yai mbele yao na akalisomea maazima, akaliona linazunguka kwa haraka ya ajabu.

Na mwingine naye amenihadithia kuwa, alimuona mchawi ameleta mawe mawili na akaanza kusemasema matalasimu yake, mara akayaona mawe yanagongana kama vile kondoo wapiganavyo pembe.

Basi yote haya mchawi hufanya mbele ya watu ima kwa ajili ya kupora mali yao au kudhihirisha uhodari na maajabu. Na mara nyingine mchawi huingiza aina hii ya uchawi katika aina nyingine. (Kivipi?).

Katika sihiri ya kufarikisha, mwanamume humuona mkewe aliye kipusa kuwa ni mbaya, na katika sihiri ya mapenzi huona kinyume chake. Aina hii ya sihiri hutofautiana na aina nyingine ya sihiri inayoitwa kiinimacho ambayo hutegemea mkono mwepesi (*mkono wa paka*).

**** Kuibatilisha sihiri ya kuzuga*:**

Sihiri hubatilishwa kwa kila kinachofukuza mashetani mfano wa:

1. Mwadhini.
2. Kusoma *Âyatul-Kursy*.
3. Nyuradi za ki-Sharia za kufukuza mashetani.

4. *Bismillâhir-Rahmânir-Rahîm.*
Kwa sharti mtu awe ana udhu.

Utakapofanya hayo na hila zake zisibatilike, basi huyo ni mwanamizungu (mwanakiinimacho), hutegemea mkono mwepesi wala si mchawi.

SAMPULI YA KIUTENDAJI YA KUBATILISHA SIHIRI YA KUZUGA

Mchawi Afanya Msahafu Unazunguka

Mojawapo katika vijiji fulani, alikuwepo mchawi aliyekuwa akionyesha uhodari wake mbele ya watu na akileta Msahafu!! Kisha akiufunga kwa uzi wa *Sûratu Yâsîn*, halafu uzi ule akiufunga na ufunguo, halafu akiuwenua Msahafu akiufanya umefungwa hivi katika uzi, hatimaye akisemasema talasimu na akiuambia Msahafu: "Zunguka kulia," nao Msahafu huzunguka upande wa kulia kwa haraka ya ajabu. Halafu akisema: "Zunguka kushoto," Msahafu wazunguka kushoto kwa haraka ya ajabu bila ya kuuharakisha mkono wake. Watu wamemuona mara nyingi mpaka wakakaribia kufitiniwa naye, hasa kwa kuwa yuwafanya hivi kwa kutumia Msahafu. Na maoni yalioenea kwa watu ni kuwa mashetani hawawezi kugusa Msahafu. Nilipoijua habari hiyo, nilimwendea pamoja na shababu mmoja [kwa sasa ameshafariki, Allâh Amrehemu]. Wakati huo nilikuwa katika Madrasa ya upili (*Thanawiyyah*). Nikashindana naye mbele ya watu afanye Msahafu kama nilivyotaja. Watu wakashangaa na kustaajabu, kwa sababu wamemuona akifanya hivyo mara nyingi (hata imekuwa ni kawaida tu). Na kweli alileta Msahafu na uzi wa *Sûratu Yâsîn*, akaufunga katika ufunguo, akaushika ufunguo mkononi mwake. Wakati huo nilimwita sahibu yangu nikamwambia: "Kaketi upande ule mwingine na ukariri kuisoma *Âyatul-Kursy*. Nami nikaketi janibu ya mkabala wake katika kikao naisoma *Âyatul-Kursy* moyoni mwangu." Watu wameketi wanatazama. Alipomaliza kuisoma talasimu yake, aliuambia Msahafu: "Zunguka kulia." Msahafu haukuzunguka! Akaisoma tena talasimu akauambia Msahafu "zunguka kushoto." Msahafu haukutukuta! Allâh Akamkhizi mbele ya watu

"… bila shaka Allâh Humnusuru anayeinusuru Dini Yake." [22: 40].

﴿وَلَيَنْصُرَنَّ اللهُ مَنْ يَنْصُرُهُ﴾.

Haiba yake ikaanguka mbele ya watu. Shukrani zote ni za Allâh Pekee, Kwake tu tumeamini na Ndiye tunayemtegemea.

*****

NNE: SIHIRI YA WAZIMU

Imepokewa kutoka kwa Khârijah bin as-Salti, naye kutoka kwa ami yake, kwamba yeye alimwendea Mtume صلى الله عليه وآله وسلم , akasilimu, kisha akarejea kwake. Akawapitia watu waliokuwa wana mwendawazimu aliyefungwa kwa chuma. Watu wake wakamwambia: "Sisi tumehadithiwa kwamba mtu wenu huyu amekuja na kheri, je muna kitu cha kumponyea?" Basi nikamzungua kwa *Sûratul-Fâtiha* siku tatu, akapona, wakanipa mbuzi mia (100). Nikamwendea Mtume صلى الله عليه وسلم na nikamweleza habari hiyo. Akaniuliza: **"Ulisema vingine isiokuwa hivi?"** Nikamjibu: "Laa (hapana)." Akasema: **"Kula kwa Jina la Allâh. Naapa kwa uhai wangu! Kama yuko aliyekula kwa zunguo la ubatilifu, hakika wewe umekula kwa zunguo la haki."**

عن خارجة بن الصلت، عن عمه: أنه رجع من عند رسول الله – صلى الله عليه وسلم – فمر على أعرابي مجنون موثق بالحديد. فقالوا: أعندك شيء نداويه به؟ فإن صاحبك قد جاء بخير، فقلت: نعم، فرقيته بأم الكتاب ثلاثة أيام: كل يوم مرتين، فبرأ، قال: فأعطوني مائة شاة، فلم آخذها حتى أتيت رسول الله – صلى الله عليه وسلم –، فأخبرته، فقال: ﴿قُلْتَ غَيْرَ هَذَا؟﴾. قلت: لا، قال: ﴿كُلْهَا بِاسْمِ اللهِ. لَعَمْرِي لَمَنْ أَكَلَ بِرُقْيَةِ بَاطِلٍ، لَقَدْ أَكَلْتَ بِرُقْيَةِ حَقٍّ﴾.

Riwâyah nyingine imesema: "Akamzungua kwa *Sûratul-Fâtiha* siku tatu asubuhi na jioni, kila aimalizapo huyakusanya mate yake halafu

akamtemea.” [Abû Dâwûd. Mlango wa *Tibbi* (19) ikasahihishwa na Imâm Nawawy katika *al-Adhkâr* (87)].

* ***Dalili za sihiri ya wazimu***:

1. Kutokuwepo kiakili na kusahau mno.
2. Kuboronga katika maneno.
3. Macho kumkodoka.
4. Kutotulia mahali pamoja.
5. Kutoendela katika kazi fulani.
6. Kutojishughulisha na mandhari.
7. Katika hali ya ugonjwa kuzidi, huenda asipopajua, na huenda akalala mahala palipohamwa.

* ***Hutokezeaje sihiri ya wazimu?***

Jini aliyetumwa kwa sihiri hii, humwingia aliyesihiriwa na kufanya makao katika ubongo – kama alivyolazimishwa na mchawi – kisha huzibana seli za ubongo n.k. zinazohusiana na kufikiri na kukumbuka, au hufanya mambo ambayo Anayejua ni Allâh tu; basi hapo dalili zikaanza kuonekana kwa mtu aliyesihiriwa.

KUITIBU SIHIRI YA WAZIMU

1. Utamsomea zunguo nililolitaja hapo mbeleni.
2. Atakapopandwa na jini, utamfanyia kama nilivyotaja hapo mbeleni na kama nilivyobainisha katika kutibu wazimu katika kitabu *Wiqâyatul-Insân, Minaljinni Wash-shaitân,* (Kinga ya Mwanaadamu Dhidi ya Jini na shetani), ukurasa wa 79-93].
3. Asipopandwa na jini, utamkariria zunguo mara tatu au zaidi, asipopandwa tena na jini, utamrekodia Sura hizi katika kanda (kaseti) na aisikilize kila siku mara mbili au tatu kwa muda wa mwezi mmoja kamili. Aya zenyewe ni hizi: Aya za zunguo - [zilizotajwa katika fasili ya saba-*njia nyingi za kumtibu aliyefungwa*-. Na pia hapana ubaya kuongeza Aya au Sura nyinginezo zinazonasibiana na mambo haya] – *(Sûratul) Baqarah – Hûd – Al-Hijri – As-Sâffâti – Qâf – Ar-Rahmân – Al-Mulk – Al-Jinni – Al-A’lâ – Az-Zilzalah – Al-Humazah – Al-Kâfirûn – Al-Falaq – An-Nâs*, pamoja na kufahamu kuwa, mgonjwa ataona dhiki

kubwa wakati anapozisikiliza Sura hizi, na huenda akapanda jini katika muda huu na jini likazungumza. Huenda maumivu yakazidi kwa muda wa siku 15 halafu yakaanza kupungua kidogokidogo mpaka mwisho wa mwezi, na hapo atakuwa kama kawaida yake, utaendelea kumsomea zunguo hilo kwa ajili ya kuhakikisha tu.

4. Mgonjwa – wakati anapotibiwa – asitumie dawa za kutuliza maumivu; kwani huharibu matibabu.
5. Hapana ubaya kuketi katika mwangaza wa taa wakati wa matibabu, kufanya hivyo, husaidia kumuudhi jini na kuharakisha ponyo.
6. Yawezekana muda wa matibabu ukawa ni chini ya mwezi mmoja, na pia yawezekana ukazidi hadi miezi mitatu au zaidi.
7. Katika kipindi cha matibabu, ni lazima mgonjwa ajiepushe na maasi yote madogo au makubwa kama vile kusikiliza nyimbo, kuvuta sigara, kuacha Swala, kutembea uchi iwapo ni mwanamke (au kujipodoa hadharani) na mengineyo.
8. Mgonjwa anapohisi maumivu katika tumbo, hii ni dalili kuwa sihiri ilikuwa ni ya kula au kunywa, kwa hivyo utamsomea Aya za zunguo kwa ukamilifu katika maji na anywe katika kipindi cha matibabu ili uchawi ulio ndani ya tumbo lake, ubatilike au autapike.

*****

SAMPULI YA KUITIBU SIHIRI YA WAZIMU

Niliwahi kujiwa na kundi la watu wakiwa na kijana barobaro aliyefungwa kwa chuma, aliponioana aliruka kwa miguu yake na akazitupa pingu alizofungwa nazo, wale jamaa wakamrukia na wakambwaga chini. Nikaanza kumsomea Qur'âni, lakini kila nimsomeapo, yeye hunitemea mate usoni mwangu, mwisho niliwapa kanda (kaseti) ya Qur'âni wamtilie aisikilize kwa muda wa siku 45 halafu anirudie. Baada ya ule muda niliowapa kumalizika, alikuja akitembea naye yu katika hali ya ukamilifu wa nguvu zake za akili na akiniomba msamaha kwa alionitendea hapo mbeleni japo hakuwa akifahamu jambo hilo, basi nilipomsomea mara ya pili, hakukutokea lolote, akatoka salama salimini; *Al<u>h</u>amdulillâh*. Hapana nguvu ya kufanyia utiifu wala kuepukia maasi ela ni kwa msaada wa Allâh. Halafu

akaniuliza kuwa: “Napaswa kutoa sadaka maalumu au kufunga au jambo lolote kwa ajili ya ponyo nililopata?” Nikamjibu: “Ama kwa upande wa kuwa ni wajib, hapana. Lakini ukitaka kutoa sadaka kwa masikini wa mjini mwako au kufunga kwa sababu ya kumshukuru Allâh, jambo hilo ni zuri.”

*****

HALI YA PILI

Nilijiwa na barobaro aliyeikana akili yake na akajishuku katika silika yake. Nilipomsomea zunguo, ilibainika kuwa amesibiwa na sihiri ya wazimu hasa naye alikuwa anataka kuowa. Nikampa aya za Qur’âni zilizorekodiwa katika kanda awe akisikiliza, na Aya nyinginezo nilizozisoma katika maji, nikamwambia anirudie baada ya mwezi. Baada ya siku ishirini takriban, nilijiwa na mmoja katika jamaa zake na akanipa habari njema kuwa yule kijana amekuwa na akili yake timamu. *Alhamdulillâhi Rabbil‘âlamîn*, kisha akaowa. Hapana nguvu ya kufanyia utiifu wala kuepukia maasi ela ni kwa msaada Wake (Allâh).

TANO: SIHIRI YA UPUMBAVU

*** *Dalili za sihiri ya upumbavu:***

1. Kupenda upweke.
2. Upweke kamili (wa kujishughulisha na mambo yake tu).
3. Kunyamaa daima.
4. Kuchukia mikusanyiko.
5. Kutokuwepo kiakili.
6. Kuumwa na kichwa daima.
7. Kutulia na kujikunyata (kujikunja) daima.

*** *Hutokeaje sihiri ya upumbavu?***

Mchawi humtuma jini kwa mtu aliyekusudiwa na anamwamuru akite katika bongo na amsababishie mtu yule kuwa pweke na kuwa mbali na watu. Yule jini hujitahidi kufanya kazi ile kadiri awezavyo. Na dalili

zake hudhihiri kwa aliyesihiriwa kulingana na nguvu au udhaifu wa jini aliyepewa kazi ya sihiri ile.

* ***Kuitibu sihiri ya upumbavu*:**

1. Utamsomea zunguo lililopita.
2. Atakapopanda jini, utazungumza naye, utamwamuru na umkanye kama tulivyobainisha huko mbeleni.
3. Asipopanda jini, utamrekodia Sura hizi katika kanda, nazo ni: *Al-Fâtiha – Al-Baqarah – Âli 'Imrân – Yâsîn – As-Ssâffât – Ad-Dukhân – Adh-Dhâriyât – Al-Hashri – Al-Ma'ârij – Al-Ghâshiyah – Az-Zilzalah – Al-Qâri'ah – Al-Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*).

Utazirekodi katika kanda tatu, moja ataisikiliza asubuhi, ya pili ataisikiliza alasiri na ya tatu ataisikiliza wakati wa kulala; ataendelea hivyo kwa muda wa siku 45, na huenda siku zikaongezeka hadi 60.

4. Mda ukimalizika tu, atakuwa ameshapona Inshâ-allâh.
5. Mgonjwa ajiepushe kumeza vidonge vya kutuliza maumivu.
6. Mgonjwa atakakapohisi maumivu tumboni, utamsomea Aya za zunguo katika maji na anywe katika muda huu (wa matibabu).
7. Mgonjwa atakapohisi maumivu ya kichwa daima, utamsomea Aya za zunguo katika maji na atayaogea kila siku tatu mara moja katika kipindi kilichotajwa; kwa sharti asizidishe maji wala asiyachemshe, na aogee mahali pasafi.

*****

SITA: SIHIRI YA SAUTI

* ***Dalili ya sihiri ya sauti:***

1. Ndoto zinazofazaisha.
2. Huona ndotoni kana kwamba kuna mtu anamwita.
3. Husikia sauti zinazosema naye anapokuwa macho, lakini haoni mtu (anayemsemesha).
4. Wasiwasi mwingi.
5. Kuwashuku sana marafiki na wendani.

6. Huona – usingizini – kana kwamba anataka kuanguka kutoka mahali pa juu.
7. Huona wanyama wanaomfukuza usingizini.

**** Hutokezeaje sihiri ya sauti?***

Mchawi humtuma jini na akimpa kazi ili amshughulishe mtu huyu usingizini na anapoamka, kwa hivyo huyu jini hujifananisha katika usingizi na wanyama wanaowinda wanaomshambulia, na huwa akimwita anapokuwa macho, na pengine humwita kwa sauti za watu anaowajua au kwa sauti za ajabu kisha akimtia shaka kwa karibu au mbali. Dalili zake zinakhitilafiana kulingana na nguvu ya sihiri yenyewe na udhaifu wake. Na pengine dalili zake huzidi mpaka zikamfikisha katika wazimu, na pengine huwa dhaifu hata isizidi wasiwasi.

**** Kuitibu sihiri ya sauti*:**

1. Utamsomea mgonjwa zunguo la sihiri.
2. Akipanda jini, utamtibu kama nilivyotaja mbeleni.
3. Asipopanda, utampa mafundisho haya:
4. Kutawadha kabla ya kulala na kuisoma *Âyatul-Kursy*.
5. Kuvikusanya viganja na kusoma *Mu‘awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a‘ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a‘ûdhu Birabbin-Nâs*), atavuvia ndani yake na atajipangusa mwilini mara tatu kabla ya kulala.
6. Kusoma *Sûratus-Sâffâti* asubuhi na *Sûratud-Dukhân* wakati wa kulala, au atazisikiliza (iwapo hajui kusoma).
7. Kuisoma *Sûratul-Baqarah* katika kila siku tatu au kuisikiliza.
8. Kuzisoma Aya mbili za mwisho za *Sûratul-Baqarah* kabla ya kulala.
9. Wakati wa kulala atasema:

“Bismillâhi wadha’tu jambî, Allâhummaghfirlî dhambî, wa akhsi shaytânî, wafukka rihânî,

﴿بِسْمِ اللهِ وَضَعْتُ جَنْبِي، اللَّهُمَّ اغْفِرْلِي

ذَنْبِي وَأَخْسِئْ شَيْطَانِي وَفُكَّ رِهَانِي وَاجْعَلْنِي فِي النَّدِيِّ الأَعْلَى﴾.

waj‘alnî finnadiyyil-a’lâ.”[1]

10. Utamrekodia Sura hizi katika kanda: *Fussilat – Al-Fat-hi – Al-Jinni*.

Mafundisho yote haya, atayafanya kwa muda wa mwezi mmoja kamili, atapona kwa Idhini ya Allâh.

*****

SABA: SIHIRI YA UGONJWA

* ***Dalili zake*****:**

1. Maumivu ya daima katika kiungo chochote kile.
2. Mshtuko wa misuli.
3. Kiungo chochote kupooza.
4. Kupooza mwili mzima.
5. Mojawapo katika hisia kutofanya kazi.

Napenda kutanabahisha kuwa, baadhi ya dalili hizi hufanana na dalili za maradhi ya viungo. Unaweza kutofautisha baina ya mawili hayo kwa kumsomea zunguo mgonjwa, atakapohisi – wakati wa kusomewa – kisunzi, au ganzi, au kuumwa na kichwa, au mtikiso viungoni mwake, au mabadiliko yoyote mwilini mwake, basi hayo ni maradhi ya sihiri kama tulivyosema, laa si hivyo, yatakuwa ni maradhi ya kiungo na hutibiwa kwa daktari.

* ***Huwaje sihiri ya ugonjwa?***

Yafahamika kuwa, ubongo ndio kiongozi mtawala juu ya mwili, kwa maana kila hisia miongoni mwa hisia za Mwanaadamu, ina kituo chake ubongoni huwa ikipokea ishara kutoka katika kituo hicho. Lau kidole

---

[1] Kwa Jina la Allâh, nimeweka ubavu wangu. Mola wangu, Nisamehe dhambi zangu, Mdhalilishe shetani wangu, Unifungue rehani (Uniepusha dhambi nilizotenda) na Unijaalie katika hadhra ya Malaika.

chako kitakaribia moto, kidole hicho kitapeleka ishara haraka hadi katika kituo cha hisia ubongoni, na amri itakuja kutoka kituoni kwamba kidole hicho kijiepushe haraka na chanzo cha hatari; hapo mkono nao hujiepusha mbali na moto. Hayo yote hukamilika katika nukta ya sekunde tu!

"Vyote hivi Ameviumba Allâh. Basi nionyesheni ni nini walichoumba wale wasiokuwa Yeye." [31: 11].

﴿هَذَا خَلْقُ اللهِ فَأَرُونِي مَاذَا خَلَقَ الَّذِينَ مِنْ دُونِهِ﴾.

Mwanaadamu anaposibiwa na sihiri ya maradhi, jini aliyepewa kazi hiyo na mchawi hukita ubongoni katika kituo, akastakiri katika kituo cha kusikia, kuona, hisia za mkononi au katika hisia za mguuni. Basi hapo kiungo kikawa kiko baina ya hali tatu:

1. Ima yule jini azuie – kwa Uwezo wa Allâh – ishara isiweze kufika katika kiungo, hapo kisifanye kazi, mgonjwa akasibiwa na upofu, ububu, uziwi au kupooza kiungo.
2. Ima jini azuie – kwa Uwezo wa Allâh – ishara wakati mwingine kiungo kisiweze kufanya kazi, na wakati mwingine akiachie kifanye kazi.
3. Na ima jini aufanye ubongo uwe ukitoa ishara kwa kufwatana mfululizo kwa haraka bila sababu, hapo kiungo kikawa kigumu na kisiweze kutaharaki hata kama hakikupooza.

Allâh Amesema juu ya wachawi:

"Wala hawakuwa wenye <u>kumdhuru</u> yeyote kwa hayo ela kwa Idhini ya Allâh." [2: 102].

﴿وَمَا هُمْ بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلاَّ بِإِذْنِ اللهِ﴾.

Allâh Aliyetakasika, Akathubutisha madhara yaliyompata aliyesihiriwa kutoka kwa wachawi, lakini Ameyafunga kwa Matakwa Yake, basi usione ajabu.

Madaktari wengi walikuwa hawakubali jambo hilo (la sihiri) wala hawasadiki. Lakini walipoziona hali mbalimbali kwa mboni za macho yao wenyewe, hapo wakawa hawana budi kusadiki na kusalimu amri ya Allâh Mtukufu Muweza.

Siku moja nilijiwa na daktari, akanambia: “Nimekuja kwa jambo lililonishangaza!” Nikasema: “Kheri. Kumetokea nini?” Akasema: “Bwana mmoja alinijia na mwanaye aliyepooza hawezi hata kutukuta. Nilipomchunguza, nilifahamu kuwa amesibiwa na maradhi katika uti wa mgongo. Jambo hili katika uchunguzi wa madaktari, halitibiki si kwa upasuaji wala kwa njia yoyote nyingine. Baada ya majuma kadhaa, yule bwana alinijia, nikamwuliza kuhusu mwanawe aliyepooza pande nne. Akasema: “*Alhamdulillâh*, sasa yuwaketi na yuwatembea akijizuia na ukuta.” Nikamwuliza: “Ulimtibu kwa nani?” Akasema: “Kwa Wahîd.” Yule daktari akanambia: “Ndio hivi nimekuja ili nijue maradhi haya umeyatibu vipi.” Nikamwambia: “Nilimsomea Aya za Qur’âni, kisha nikamsomea zunguo katika mafuta ya habalsoda na nikawaambia wampake katika viungo vilivyopooza.” *Alhamdulillâhi Rabbila‘âlamîn. Walâ hawla walâ quwwata illâ billâhil‘aliyyil-‘adhwîm.*

KUITIBU SIHIRI YA UGONJWA

1. Utamsomea zunguo mara tatu, atakapopandwa na jini, utamtibu kama nilivyotaja hapo mbeleni.
2. Asipopandwa na jini lakini akahisi mabadiliko kidogo, utampa mafundisho haya:

- Utamrekodia katika kanda *Sûratul-Fâtiha, Âyatul-Kursy, Sûratud-Dukhân, Sûratul-Jinni*, Sura fupifupi na *Mu‘awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a‘ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a‘ûdhu Birabbin-Nâs*). Kanda hii ataisikiliza mara tatu kila siku.
- Utamsomea zunguo hili katika mafuta ya habalsoda, na utamwambia ajisugue kwayo katika kipaji chake na mahala panapouma mwilini mwake, asubuhi na jioni. Zunguo lenyewe ni hili:

1. *Sûratul-Fatihah*.
2. *al-Mu‘awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a‘ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a‘ûdhu Birabbin-Nâs*).
3. ﴿وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ﴾.
4.

Bismillâhi arqîk, Wallâhu yashfîka min kulli dâ-in yu'dhîk, wamin sharri kulli nafsin aw 'aini h̲âsid, Allâhu yashfîk.(1)

﴿بِسْمِ اللهِ أَرْقِيْكَ وَاللهُ يَشْفِيْكَ مِنْ كُلِّ دِاءٍ يُؤْذِيْكَ وَ مِنْ شَرِّ كُلِّ نَفْسٍ أَوْ عَيْنِ حَاسِدٍ اللهُ يَشْفِيْكَ﴾.

5.
Allâhumma rabbannâs, adh-hibilba-s, washfi Antasshâfî, lâ shifâ-a illâ shifâ-uk, shifâ-allâyughâdiru saqamâ walâ alamâ.(2)

﴿اللَّهُمَّ رَبَّ النَّاسِ أَذْهِبِ الْبَأْسَ وَ اشْفِ أَنْتَ الشَّافِي لاَ شِفَاءَ إِلاَّ شِفَاؤُكَ شِفَاءً لاَ يُغَادِرُ سَقَمًا وَلاَ أَلَمًا﴾.

Ataendelea na mafundisho haya kwa muda wa siku 60, akipona ataacha. Na kama hakupona, utamzungua mara nyingine kisha utampa mafundisho yale yale kwa muda mwingine tena kama utakavyoonelea na kulingana na hali kuendelea vizuri.

SAMPULI YA KUITIBU SIHIRI YA UGONJWA
Msichana Hazungumzi Yapata Mwezi

Baba yake na ndugu yake walimleta, naye amenyamaa hazungumzi, bali hawezi kufungua kinywa hata kwa ajili ya kula pia, ispokuwa wakimfungua kwa lazima na wakimpa juisi au maziwa. Wakanambia: "Huyu yu katika hali hii yapata siku 35." Alipolisikia zunguo, papo hapo alizungumza." *Alh̲amdulillâh*.

---

(1) Kwa Jina la Allâh nakuzungua, Allâh Akuponye kutokana na kila maradhi yanayokudhuru, kutokana na shari ya kila nafsi au jicho la mwenye husuda, Allâh Akupe shifaa (ponyo).

(2) Ewe Mola, Mlezi wa watu, Ondosha huzuni, Ponya, Wewe Ndiwe Mponyaji, hakuna ponyo ispokuwa ponyo Lako, ponyo lisilobakisha ugonjwa wala maumivu.

Jini Ameuzuwia Mguu Wa Mwanamke

Aliniambia kuwa, yeye husikia maumivu makali mguuni mwake. Nikasema pengine ni baridi-yabisi (*rheumatism*). Lakini nikasema nitamsomea zunguo makhsusi, wakati huo alikuwa akitembea kwa shida. Basi alipoisikia tu *Sûratul-Fâtihah,* alipanda jini, yule jini akatamka kuwa yeye ameuzuwia mguu wake. Nikamwamuru atoke kwa ajili ya kumtii Allâh Pekee. Akatoka, na yule mwanamke akasimama akitembea bila matatizo. *Alhamdulillâh*.

Uso Wake Umegeuka Kwa Sababu Ya Jini

Bwana huyu alinijia na uso wake umegeukia upande wa kulia – ikiwa sijakosea – ukionekana wazi kabisa. Nilipomsomea zunguo, jini alizungumza na akasema kuwa yule jamaa "aliniudhi." Mimi nikamkinaisha kuwa yeye huyu bwana hakuwa amemuona, na kwamba jambo hilo ni haramu kwa jini. Nikamwamuru mema, nikamkanya mabaya. Basi akasikiliza na akatoka. *Alhamdulillâh*. Yule bwana akaenda zake baada ya kuwa mdomo wake umekuwa sawa.

Msichana Aliyeshindikana Kutibiwa Na Madaktari

Baba yake alinijia akanambia: "Binti yangu alipatwa na dhiki akazimia. Yapata miezi miwili sasa yuko katika hali yake ileile, anaanza kusikia lakini hawezi kuzungumza wala kula chakula, wala hawezi kutingisha chochote katika mwili wake. Kwa sasa amelazwa katika Hospitali ya 'Asir huko Abha (Saudi Arabia) katika chumba cha uangalizi wa wastani. Mmoja katika madaktari amenambia kuwa kila uchunguzi uko sawa, nao hawajui ana nini, ispokuwa tu wamemfungulia kitundu katika koo awe akipumua kwa hapo. Wamemtia paipu ya chakula puani ili aishi siku zake zilizobakia juu ya kitanda hiki na katika hali ile.

Kwa desturi yangu, vyovyote iwavyo huwa simwendei yeyote ili nimtibu. Lakini nikapata ujumbe wa salamu za mdomo kutoka kwa mmoja wa walinganizi fadhili na sahibu azizi, naye ni Sheikh Sa'îd bin Musfir al-Qahtâny – Allâh Amhifadhi – nikasema hapana budi kumwendea. Wakaniletea kibali cha hospitali kinachoniruhusu kuingia wakati usio wa kutembelea wagonjwa na kumtibu aliyetajwa. Na kweli, nikamkuta yupo kitandani katika hali ambayo hakuna aijuwae ispokuwa

Allâh kutokana na udhaifu na ukondefu, wala hawezi kutingisha chochote ela kichwa na kwa harakati ndogo, anasikia na anaona. Nikamwuliza dalili zote, akatingisha kichwa chake kwa kukanusha. Kwa kweli sikujua ana nini. Lakini tulienda kuswali magharibi, nikamwombea katika Swala kisha tukarejea, nikamsomea *Sûratul-Falaq* na dua hii:

Allâhumma rabbannâs, adh-hibilba-s, washfi Antasshâfî, lâ shifâ-a illâ shifâ-uk, shifâ-allâyughâdiru saqamâ walâ alamâ.[(1)]

﴿اللَّهُمَّ رَبَّ النَّاسِ أَذْهِبِ الْبَأْسَ وَ اشْفِ أَنْتَ الشَّافِي لاَ شِفَاءَ إِلاَّ شِفَاؤُكَ شِفَاءً لاَ يُغَادِرُ سَقَمًا وَلاَ أَلَمًا﴾.

Yule msichana akatamka na akazungumza – kwa Fadhila za Allâh Pekee – basi yule baba na ndugu wakalia kwa furaha. Yule baba akasimama ili anibusu kichwa. Nikamwambia: "Usiitakidi kwa watu, bali itakidi kwa Allâh – *'Azza wa Jalla* – kwani Allâh Alimtakia shifaa katika muda huu. Shifaa ikaja katika mkono wa mja miongoni mwa waja wa Allâh." Yule msichana akasema: "*Al<u>h</u>amdulillâh*." Akazungumza na akasema: "Nataka kutoka hospotali." [Baadaye akanijia nduguye akanipa bishara njema kuwa hana neno, na akataka kunialika katika karamu makhsusi, nikakataa kwa kuchelea isije ikawa ndio ujira].

Jini Yuwafahamisha Mahala Pa Sihiri

Nilijiwa na shababu aliyekuwa mgonjwa, nilipomsomea, jini alitamka kuwa yeye amewakilishwa kwa sihiri, na akatujulisha mchawi anayefanya pamoja naye, akatufahamisha mahala pa sihiri, akasema: "Sihiri ipo katika kizingiti cha mlango." Kisha nikamwamuru atoke, akatoka, halafu wale jamaa wa kijana yule wakaenda hadi mahala palipotajwa, wakafukua na wakaipata sihiri ni karatasi iliyochanwa na imeandikwa herufi, kisha wakaiyeyusha katika maji, sihiri ikabatilika, *Al<u>h</u>amdulillâh*.

---

(1) Ewe Mola, Mlezi wa watu, Ondosha huzuni, Ponya, Wewe Ndiwe Mponyaji, hakuna ponyo ispokuwa ponyo Lako, ponyo lisilobakisha ugonjwa wala maumivu.

NANE: SIHIRI YA KUTOKWA DAMU (*ISTIHÂDHA*)[1]

**** Hutokeaje sihiri ya kutokwa damu?***

Aina hii ya sihiri, huwapata wanawake pekee. Mchawi humsalitisha jini kwa mwanamke anayekusudiwa kurogwa na kumlazimisha amtoe damu. Jini huingia katika mwili wa mwanamke na akapita katika mishipa yake pamoja na damu.

Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿إِنَّ الشَّيْطَانَ يَجْرِي مِنَ ابْنِ آدَمَ مَجْرَى الدَّمِ﴾.

“shetani hupita kwa Mwanaadamu mapitio ya damu.” [Bukhârî (4/282 *Fat-hi*) na Muslim (14/155 *Nawawy*)].

shetani anapofika katika mshipa maarufu katika kizazi, humkanyaga kwa nguvu, mshipa huu ukaanza kuvuja damu. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم anasema wakati Hamnah binti Jahsh alipouliza kuhusu damu ya *istihâdha*:

﴿إِنَّمَا هِيَ رَكْضَةٌ مِنْ رَكَضَاتِ الشَّيْطَانِ﴾.

“Huo ni mkanyago wa shetani.” [Tirmidhy amesema: ni *Hasan Sahîh*. Akasema: “Nikamwuliza Muhammad bin Ismâ‘îl al-Bukhârî akasema: “Ni Hadîth *Hassan*”].

Riwâya nyingine imesema:

﴿إِنَّمَا هُوَ عِرْقٌ وَلَيْسَتْ بِالحَيْضَةِ﴾.

“Hiyo ni vena wala si hedhi.” [Riwâya hii iko kwa Ahmad na Nasâ-î kwa isnad *jayyid*].

Kulingana na hizo riwâya mbili, imefahamika kuwa *istihâdha* ni mkanyago wa shetani katika mshipa miongoni mwa mishipa iliyomo katika kizazi cha mwanamke.

---

[1] *Istihâdha:* ni damu imtokayo mwanamke katika kipindi kisichokuwa cha hedhi.

**** Ni nini sihiri ya kutokwa damu?***
Ni ile ambayo Mafuqahaa (Wanazuoni wa Sharia) wanaiita *istihâdha,* na madaktari wanaiita hemoraji (*haemorrhage*) – maradhi ya kutokwa na damu. Ibnul-Athîr amesema: "*Istihâdha* ni mwanamke aendelee kutokwa na damu baada ya siku za hedhi yake ya kawaida." [*an-Nihâyah:* 1/469].

Huenda utokaji wa damu ukaendelea kwa miezi, na huenda kiasi cha damu kikawa ni kidogo au kingi.

**** Kuitibu sihiri ya kutokwa damu*:**
Utamsomea zunguo katika maji, atakunywa na ataogea kwa muda wa siku tatu, damu itakatika kwa Idhini ya Allâh.

SAMPULI YA KUITIBU SIHIRI YA KUTOKWA DAMU

Alinijia mwanamke akitokwa na damu nyingi mno. Nikamsomea zunguo kisha nikampa kanda ya Qur'âni iliyorekodiwa. Ilichukua siku chache tu, damu ikasimama. *Alhamdulillâh*.

Kwa mnasaba wa kuziandika Aya za Qur'âni na kuzinywa (yaani kombe), Shaikhul-Islâm Ibnu Taimiyyah رحمه الله تعالى ametoa fatwa kuwa inajuzu (inafaa). Akasema: "Inajuzu kumwandikia mgonjwa yeyote sehemu katika Qur'âni kwa wino unaoruhusiwa, ioshwe na anyweshwe maji hayo, kama alivyoandika mas'ala hayo Imâm Ahmad na wengineo." [*Majmû 'ul-Fatâwâ:* 19/64].
- Ama Swala ya mwenye *istihâdha*, saumu yake na ibada nyinginezo, mahali pake ni katika vitabu vya Fiqhi (Sharia).

TISA: SIHIRI YA KUVUNJA NDOA

**** Sihiri ya kuvunja ndoa hutimia vipi?***
Mwenye chuki na makri, humwendea mchawi khabithi na akimtaka amfanyie sihiri binti ya fulani ili asiolewe, hapo mchawi akataka apewe jina lake na la mama yake na mojawapo katika athari zake (nguo, nywele, ukucha n.k.), halafu hufanya sihiri na akimwakilisha jini mmoja au zaidi kwa sihiri hii. Yule jini huenda na akaketi kwa binti huyu ili

apate fursa ya kumuingia katika mojawapo kati ya hali hizi tulizotaja mbeleni:

1. Wakati wa hofu nyingi.
2. Wakati wa ghadhabu.
3. Wakati wa mghafala mwingi
4. Wakati wa kufanya mambo ya shahawa.

Jini huwa yupo baina ya hali mbili:

1. Ima amuingie mwanamke amfanye akiona dhiki kwa kila mume anayekuja kumposa.
2. Na ima (mposaji) asiweze kuingia kwa sababu ya sihiri ya kuzuga huko nje, mwanamume akasawirisha kuwa yule mwanamke ni mbaya na ikamtia wasiwasi juu ya hilo, na hali hii kadhalika iwe kwa mwanamke.

Basi ukaona kila mwanamume anayekuja kumposa mwanamke huyu, huwa hamtaki pasina sababu yoyote hata kama mwanzo atakubali, lakini baada ya masiku atakataa, na hali hiyo yatokana na wasiwasi wa shetani kwake.

Katika hali ya sihiri kushitadi, utamkuta mwanamume anayekwenda kumposa mwanamke, tangu anapoingia katika mlango wa nyumba ya anayeposwa, husikia dhiki kubwa na maisha anayaona giza usoni mwake kana kwamba yupo gerezani, akitoka harudi tena.

Katika muda wote huo, jini humsababishia mwanamke maumivu ya kichwa katika vipindi tofauti.

*** Dalili za sihiri hii:**

1. Kuumwa na kichwa kisichoisha kila baada ya muda fulani; hata akitumia dawa.
2. Kusikia dhiki kubwa moyoni, hasa baada ya alasiri mpaka katikati ya usiku.
3. Kumuona mposaji katika mandhari mbaya.
4. Kufikiri na usahaulifu.
5. Kuwa na hamaniko jingi usingizini.
6. Wakati mwingine, husikia maumivu daima katika maida (utumbo).
7. Maumivu katika pingili la chini la uti wa mgongo.

KUTIBU SIHIRI YA KUVUNJA NDOA

1. Utamsomea zunguo, akipanda jini na akatamka, utamfanyia kama nilivyotaja mbeleni.

2. Asipopandwa na jini na akahisi mabadiliko mwilini mwake, utampa mafundisho haya:

* Avae hijabu ya ki-Sharia.
* Aswali kwa wakati wake.
* Asisikilize mziki.
* Atawadhe kabla ya kulala na kusoma *Âyatul- Kursy*.
* Avikusanye viganja kabla ya kulala, na asome *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*) pamoja na kuvuvia na kuupangusa mwili mara tatu.
* Atarekodi *Âyatul-Kursy* iliyokaririwa katika kanda kwa muda wa saa, awe akisikiliza kila siku mara moja.
* Atarekodi *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*) zilizokaririwa katika kanda kwa muda wa saa, asikilize kila siku mara moja.
* Atasomewa zunguo katika maji, atakunywa na ataogea mara moja kila baada ya siku tatu.
* Baada ya Swala ya alfajiri, atasoma mara mia (100) uradi huu:

﴿لاَ إِلـهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَ لَهُ الحَمْدُ وَ هُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ﴾.

Lâ ilâha illallâhu wahdahû lâ sharîka lah, lahulmulku walahulhamdu wahuwa 'alâ kulli shay-in qadîr.(1)

Atayatekeleza mafundisho haya kwa muda wa mwezi mmoja kamili, na baada ya mwezi – Inshâ-allâh – atakuwa katika mojawapo ya hali mbili:

1. Ima dalili zote zitakua zimeondoka, mgonjwa amepona na sihiri imebatilika.
2. Ima maumivu yatazidi na dalili zitashitadi, wakati huo atasomewa zunguo, atapandwa na jini – Inshâ-allâh – na atashughulikiwa kama tulivyoeleza mbeleni.

---

(1) Hakuna mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allâh Peke Yake, Ufalme ni Wake na Himdi zote ni Zake, Naye ni Muweza juu ya kila kitu.

SAMPULI YA KUITIBU SIHIRI YA KUVUNJA NDOA
Mwanamke Akubali Kuolewa Halafu Anakataa Asubuhi Yake

Nilijiwa na shababu akanambia: “Tunaye binti mwenye mambo ya ajabu. Anapokuja mtu kumposa, yeye hukubali kwa furaha, lakini anapolala akaamka, hubadili maoni na akakataa kuolewa naye bila ya kutoa sababu. Jambo hili limeendelea mara kwa mara mpaka tumeingiwa na wasiwasi. Nini rai yako?”

Nilipomsomea zunguo, alipanda jini na akatamka.

Nikamwuliza: “Ni nani wewe?”

Akajibu: “Ni fulani (jina nimelibana).”

Nikamwuliza: “Kwa nini umemuingia binti huyu?”

Akajibu: “Kwa sababu nampenda.”

Nikamwambia: “Yeye hakupendi. Lakini wataka nini?”

Akasema: “Sitaki aolewe.”

Nikamwuliza: “Ulikuwa ukimfanyia nini?”

Akajibu: “Yeyote anayekuja kumposa naye akakubali, mimi humtisha usingizini kwamba akiolewa nitamfanya kadha wa kadha.”

Nikamwuliza: “Una dini gani?”

Akajibu: “Ni Muislamu.”

Nikamwambia: “Jambo hili halifai ki-Sharia. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿لَا ضَرَرَ وَلَا ضِرَارَ﴾.

“Hakuna kufanya <u>madhara</u> wala kulipiza <u>madhara</u>.” [Ibnu Mâjah 2340,2341].

Kufanya hivi ni kumdhuru Muislamu na ni haramu ki-Sharia.”

Yule jini alitosheka na akatoka, yule binti akaamka. *Al<u>h</u>amdulillâh. Walâ <u>h</u>awla walâ quwwata illâ billâh.*

SIMULIZI MUHIMU KUHUSIANA NA SIHIRI

1. Yamkinika dalili za sihiri zikafanana na dalili za wazimu.
2. Kuhisi maumivu daima katika tumbo la aliyesihiriwa, ni dalili kuwa sihiri aliyofanyiwa ilikuwa ni ya kula au kunywa.
3. Tiba ya Qur'âni haiwezi kufaulu ispokuwa kwa masharti mawili:
* Istiqama (msimamo) ya anayetibu juu ya Amri ya Allâh.
* Imani ya mgonjwa na kutosheka kwake kuwa tiba ya Qur'âni ina athari.
4. Aina nyingi za sihiri huafikiana katika dalili hii: kuhisi dhiki kifuani hasa nyakati za usiku.
5. Unaweza ukatambua mahali pa sihiri kwa mambo mawili:
* Jini aliyetumwa kueleza, wala usimwamini mpaka umtume atakayeitafuta sihiri mahali palipotajwa. Ukiikuta basi ni kweli, kinyume chake ujuwe kwamba majini wana uongo mwingi.
* Mgonjwa au anayetibu, aswali rakaa mbili kwa ukweli, ikhlasi, utulivu na unyenyekevu wakati bora kama vile thuluthi ya mwisho usiku na amuombe Allâh Amuonyeshe mahali pa sihiri. Huenda ukaona katika ndoto, au ukapata hisia, au utambuzi, au dhana yako ikakwambia kuwa mahali pa sihiri ni kadhaa, basi hilo litakapokuwa, utazidi kumshukuru Allâh Mtukufu.
6. Yamkinika kusoma zunguo katika mafuta ya habalsoda na ukamwambia mgonjwa ajipake mahali pa maumivu asubuhi na jioni, atafanya hivyo kwa aina zote za sihiri.

Imethubutu katika *Sahîhul-Bukhârî* na Muslim kuwa Mtume wetu صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿الحَبَّة السَّوْدَاء شِفَاءٌ مِنْ كُلِّ دَاءٍ، إِلَّا السَّامَ﴾.

"Habalsoda ni ponyo la <u>kila ugonjwa</u> ispokuwa mauti." [Bukhârî (5687, 5688) na Muslim (2215)].

Baadhi ya nchi wanaita *habbatulbarakah*, kwingineko wanaita *shuniz*.[1]

Katika riwâya ya Muslim imesema:

---

[1] Humu kwetu: yai leusi, zenyeu, habalsoda.

﴿مَا مِنْ دَاءٍ، إِلَّا فِي الحَبَّةِ السَّوْدَاءِ مِنْهُ شِفَاءٌ، إِلَّا السَّامَ﴾.

“Hakuna ugonjwa wowote ispokuwa katika habalsoda una dawa yake ela mauti (hayana dawa).” [Muslim 2215].

*****

MGONJWA ALIYEONYESHWA NA ALLAH MAHALI PA SIHIRI

Nilijiwa na binti, nilipomsomea nilifahamu kuwa ana sihiri kali, kwani alikuwa akiona mapepo usingizini na akiwa macho n.k. La muhimu ni kuwa, niliwaambia jamaa zake: “Tumieni tiba hii na sihiri itabatilika Inshâ-allâh.” Wakaniuliza: “Ipo njia tunayoweza kujua mahali ilipo sihiri?” Nikawajibu: “Ndio.” Wakaniuliza: “Njia gani?” Nikawambia: “Ni kumuomba na kumnyenyekea Allâh hasa nyakati za thuluthi ya mwisho usiku wakati wa kujibiwa dua na kuteremka Mola wa ardhi na mbingu. [Imepokewa na Abû Huraira ﵁ amesema: “Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿يَنْزِلُ رَبُّنَا تَبَارَكَ وَتَعَالَى كُلَّ لَيْلَةٍ إِلَى السَّمَاءِ الدُّنْيَا حِينَ يَبْقَى ثُلُثُ اللَّيْلِ الآخِرُ يَقُولُ: مَنْ يَدْعُونِي، فَأَسْتَجِيبَ لَهُ مَنْ يَسْأَلُنِي فَأُعْطِيَهُ، مَنْ يَسْتَغْفِرُنِي فَأَغْفِرَ لَهُ﴾.

“Mola wetu – Aliyetukuka – Huteremka kila usiku hadi katika wingu wa dunia wakati inapobakia thuluthi ya mwisho usiku, Akisema: “Ni yupi anayeniomba Nimjibu? Ni yupi anayeniomba Nimpe? Ni yupi anayeniomba maghfira Nimsamehe?” [Muttafaq].

Na kweli, mgonjwa akasimama katika Swala, dua na kumnyenyekea Allâh – kama walivyonieleza – akaona usingizini aliyemshika mkono, akaenda naye mahali fulani nyumbani na akamuonyesha sihiri iliyozikwa hapo. Asubuhi aliwaeleza jamaa zake nao wakaenda mahali hapo hapo wakaikuta sihiri, wakaitoa na wakaibatilisha, msichana yule akapona. *Alhamdulillâhi Rabbil‘âlamîn*.

*****

FASILI YA SABA
TIBA YA ALIYEFUNGWA ASIWEZE KUMJAMII MKEWE

1. Taarifa ya kufungwa na mkewe.
2. Huwaje kufungwa?
3. Tiba ya mwanamume aliyefungwa.
4. Tiba ya mwanamke aliyefungwa.
5. Vipi tutatofautisha baina ya kufungwa na udhaifu wa nguvu za kiume?
6. Kutibu aina fulani za utasa.
7. Kutibu kushusha mapema.
8. Kinga ya maarusi (wanandoa) kabla ya kuingia ndani.

Sampuli ya kiutendaji kutibu kufungwa.

FASILI YA SABA
Tiba Ya Aliyefungwa Mkewe

**** Kufungwa*:**
Ni mwanamume aliye kamili kimaumbile na ambaye si mgonjwa, anashindwa kumjamii mkewe.

Tunapotaka kujua mtu hufungwaje, hapana budi kwanza tujue namna ya dhakari[(1)] inavyosimama.

****Fiziolojia ya kujamii kwa mwanamume*:**
Yafahamika kuwa, dhakari ya mwanamume ni kipande cha nyama kinachonyambulika, damu ikisukumwa humo husimama, na damu ikirejea, nayo hulegea.

**** Dhakari kusimama hupitia hatua tatu*:**
1. Kichocheo cha kijinsia (kujamii) kinapotokeza kwa mwanamume, mapumbu huwa yakitoa *homoni* inayozimimimina katika damu, zile *homoni* hufika mpaka kichwani na hujaa mwili mzima kama vile mkondo wa umeme.
2. Kichocheo cha kijinsia hufika katika kituo makhsusi cha kazi hiyo katika ubongo.
3. Kituo cha kichocheo cha kijinsia katika ubongo, nacho hutuma ishara kwa haraka hadi katika kituo cha mishipa ya uzazi katika uti wa mgongo, hapo ndipo vali ya mshipa wa damu iliyokuwa imefungwa, huanza kufunguka, damu ikaanza kububujika kwa nguvu katika viungo vya uzazi ikielekea katika dhakari ikimimina damu na hapo ikasimama.

**** Mwanamume hufungwaje?***
shetani wa sihiri hukita katika ubongo wa mwanamume hasa katika kituo cha kichocheo cha kijinsia kinachotuma ishara hadi katika viungo vya uzazi, halafu huviacha viungo vya uzazi vikafanya kazi yake kama

---

(1) Katika mas'ala ya tiba au Sharia, ni muhimu vitu kama hivi kutajwa wazi, si kwa nia ya matusi, bali kubainisha ili kila kitu kifahamike kwa usawa; kinyume chake, lengo halitopatikana. Ama katika mazungumzo ya kawaida, kutaja wazi wazi ni ukosefu wa staha.

kawaida. Wakati anapomkaribia mkewe na akataka kumjamii, shetani hukiharibu kituo cha kichocheo cha kijinsia katika ubongo, basi zikasimama ishara zote zinazotumwa katika viungo vinavyosukuma damu katika uume ili usimame, hapo ndipo damu inaporejea haraka kutoka katika uume na ukaanza kulegea na kusinyaa.

Kwa ajili hiyo, utamuona mwanamume yu kawaida wakati anapochezacheza na mkewe – yaani uume wake umesimama wima – lakini anapomkaribia kwa tendo la ndoa, husinyaa na asiweze kumjamii mkewe wa halali, kwa sababu uume kusimama, ndio jambo la msingi katika kukamilisha shughuli ya jimai kama tujuavyo.

Wakati mwingine utamkuta mtu ameowa wake wawili naye amefungwa kwa mmoja tu. Kwa sababu shetani wa sihiri, hukiharibu kituo cha kichocheo cha kijinsia anapomkaribia, kwa sababu huyo shetani amepewa kazi ya kumfunga na huyo mmoja tu.

*** *Fundo la mwanamume*:**
Kama vile mwanamume hufungwa asiweze kumuingilia mkewe, vilevile mwanamke naye hufungwa kwa mumewe. Kufungwa kwa mwanamke ni aina tano:

1. *Fundo la mwanamke*:
Ni mwanamke ajaribu kuzuwia mumewe kumjamii. Huwa akiyashikanisha mapaja yake kwa namna ambayo mwanamume hawezi kumjamii. Hali hiyo huwa ipo nje ya matakwa ya mwanamke. Mmoja katika barobaro ambaye mkewe alisibiwa na aina hii ya sihiri, alikuwa akimlaumu, naye husema: “Sifanyi kwa kependa kwangu!” Akamwambia: “Weka pingu katika miguu yangu kabla hatujaanza tendo hilo ili isishikane.” Na kweli alifanya hivyo. Lakini wapi, hakufaulu. Mkewe akamshauri awe akimpiga sindano ya kumpoteza fahamu anapotaka kumjamii. Mara hii alifaulu, lakini ni kwa upande mmoja tu.

2. *Fundo la ubutu (wa kuhisi)*:
Jini aliyewakilishwa kwa sihiri, hufanya makazi katika kituo cha hisia katika ubongo wa mwanamke, mumewe anapotaka kumjamii, yule jini

humkosesha hisia akawa hahisi ladha wala raha wala hampokei mahaba mumewe, mbele yake huwa kama aliyefishwa ganzi, humfanya atakavyo (lakini hata habari hana). Tezi yake huwa haitoi kiowevu kinachorutubisha uchi wa mwanamke, hivyobasi shughuli ya jimai huwa haikamiliki kwa ufanifu.

3. *Fundo la kutokwa damu*:
Tumezungumzia juu ya sihiri ya kutokwa damu katika aina ya nane miongoni mwa anuwai za sihiri, na tumeeleza hutokeaje.

Lakini aina hii ya sihiri, hukhitilafiana na sihiri ya kutokwa damu kwa jambo moja, nalo ni kuwa, fundo la kutokwa damu linahusu wakati wa kujamiiana tu, ama sihiri ya kutokwa damu, haina uhusiano na jambo hilo, bali huendelea siku nyingi.

Fundo la kutokwa damu ni mwanamume anapotaka kumjamii mkewe, shetani humsababishia kutokwa damu nyingi (*istihâdha*), hapo mwanamume asiweze kumjamii. Hata mmoja wa askari jeshi alinambia kuwa anapopata likizo ya kuja kwa mkewe, basi akifika tu nyumbani, yule mwanamke hutokwa damu na inaendelea kipindi chote cha likizo na zaidi ya siku tano au kupungua kidogo. Anaporudi kazini kwake jeshini, damu haimjii. Bali damu hukatika baada yeye tu kutoka nyumbani. Na hali hii ni daima.

4. *Fundo la kizibo*:
Mwanamume anapotaka kumjamii mkewe, hupata kizuizi kigumu cha nyama asichoweza kukitoboa; hivyobasi shughuli ya kukutana kijinsia isifaulu.

5. *Fundo la kuongeza kina cha uke*:
Mwanamume atamuowa msichana bikira, anapomjamii anamkuta kama mke mkuu kabisa hata anamshuku. Lakini anapotibiwa, sihiri hubatilika na utando wa ubikira hurudi kama ulivyokuwa.

*****

NJIA NYINGI ZA KUTIBU MAFUNDO

Njia Ya Kwanza

Utamsomea zunguo lililotajwa katika mwanzo wa *Fasili ya Sita*. Jini aliyewakilishwa kwa sihiri, akizungumza utamwuliza mahali iliopo sihiri, utaenda kuitoa na utaibatilisha, utamwamuru jini atoke katika mwili wa mgonjwa. Jini akitoka, sihiri itakuwa imeshabatilika. Na utakapomsomea zunguo wala jini asizungumze, utamtumilia njia nyingine.

Njia Ya Pili

Utazisoma Aya hizi mara kadhaa katika maji, atakunywa na ataogea siku kadhaa. Sihiri itabatilika Inshâ-allâh. Aya zenyewe ni hizi:

﴿قَالَ مُوسَى مَا جِئْتُمْ بِهِ السِّحْرُ إِنَّ اللهَ سَيُبْطِلُهُ إِنَّ اللهَ لاَ يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ. وَيُحِقُّ اللهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ﴾

﴿وَأَوْحَيْنَا إِلَى مُوسَى أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ. فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ. فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَاغِرِينَ. وَأُلْقِيَ السَّحَرَةُ سَاجِدِينَ. قَالُوا آمَنَّا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ. رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ﴾.

﴿إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سَاحِرٍ وَلاَ يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَى﴾.

Njia Ya Tatu

Utachukua majani saba mabichi ya mkunazi na utayasaga vizuri, halafu utayaweka katika chombo chenye maji, kisha utaukaribisha mdomo wako katika chombo huku ukiyakoroga majani katika maji na ukisoma *Âyatul-Kursy* na *Mu‘awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a‘ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a‘ûdhu Birabbin-Nâs*), halafu utamwamuru mgonjwa anywe na aogee maji haya siku kadhaa, wala asizidishe maji juu yake wala asiyachemshe, iwapo atahitaji kuyachemsha, basi ayaweke katika uharara wa jua, wala asiyamwage mahala penye najisi. Sihiri na mafundo yatabatilika Inshâ-allâh, na huenda fundo likafunguka mwanzo wa kuoga.

Njia Ya Nne

Utasoma zunguo katika sikio la aliyefungwa, halafu utamsomea masikioni mwake Aya hii:

﴿وَقَدِمْنَا إِلَى مَا عَمِلُوا مِنْ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَنْثُورًا﴾.

Utaikariri mara mia (100) au zaidi mpaka mgonjwa ahisi kufa ganzi katika viungo vyake. Zunguo hili utamkariria mgonjwa siku kadhaa mpaka asihisi chochote, hapo ndipo utayakinisha kuwa sihiri imebatilika Inshâ-allâh.

Njia Ya Tano

al-Hâfidh (Ibnu Hajar) amesema katika *Fat-hul-Bârî:* "'Abdur-Razzâq amepokea kwa isnadi ya Sha'by amesema: "Hapana ubaya *nushra* ya Kiarabu, nayo ni: mtu aende penye '*idhâh* (aina ya mti wenye miba) achukue kuliani mwake na kushotoni mwake (mwa mti huo) halafu ayaponde, ayasomee na aogee." [*Fat-hul-Bârî*: 10/233].

Nami nasema: Atayasomea *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*) na *Âyatul-Kursy*.

Njia Ya Sita

Aliyesihiriwa atakusanya – katika majira ya kuchipua – kiasi awezavyo mawaridi ya jangwani na mawaridi ya kwenye mabustani, halafu atayaweka ndani ya chombo kisafi na atamimina humo maji tamu, halafu mawaridi hayo yachemke kidogo tu, kisha asubiri mpaka yapoe, atayasomea *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*) halafu atajimiminia, atapona kwa Idhini ya Allâh. [*Fat-hul-Bârî*:10/234].

Njia Ya Saba

Utachukua chombo chenye maji na ukisomee *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*) na dua hizi:

Allâhumma rabbannâs adh-hibilba-s washfi Antasshâfî lâ

﴿اللَّهُمَّ رَبَّ النَّاسِ أَذْهِبِ الْبَأْسَ وَ اشْفِ

shifâ-a illâ shifâ-uk, shifâ-allâyughâdiru saqamâ walâ alamâ.[(1)]	أَنْتَ الشَّافِي لاَ شِفَاءَ إِلاَّ شِفَاؤُكَ شِفَاءً لاَ يُغَادِرُ سَقَمًا وَلاَ أَلَمًا﴾.
Bismillâhi arqîk, Wallâhu yashfîka min kulli dâ-in yu'dhîk, wamin sharri kulli nafsin aw 'aini hâsid, Allâhu yashfîk.[(2)]	﴿بِسْمِ اللهِ أَرْقِيْكَ وَاللهُ يَشْفِيْكَ مِنْ كُلِّ دَاءٍ يُؤْذِيْكَ وَ مِنْ شَرِّ كُلِّ نَفْسٍ أَوْ عَيْنِ حَاسِدٍ اللهُ يَشْفِيْكَ﴾.
A'ûdhu bikalimâtillâhittâmmâti minsharri mâkhalaq.[(3)]	﴿أَعُوْذُ بِكَلِمَاتِ اللهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ﴾.
Bismillâhilladhî lâ yadhurru ma'asmihî shay-un fil-ardhi walâ fissamâ, wahuwassamî 'ul'alîm.[(4)]	﴿بِسْمِ اللهِ الَّذِي لاَ يَضُرُّ مَعَ اسْمِهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلاَ فِي السَّمَاءِ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ﴾.

Utazisoma dua hizi katika maji; atakunywa na kuogea siku kadhaa. Sihiri na mafundo yatabatilika kwa Idhni ya Allâh.

Njia Ya Nane

Utachukua chombo safi na utaandika kwa wino twahara (safi) Aya hizi:

---

(1) Ewe Mola, Mlezi wa watu, Ondosha huzuni, Ponya, Wewe Ndiwe Mponyaji, hakuna ponyo ispokuwa ponyo Lako, ponyo lisilobakisha ugonjwa wala maumivu.

(2) Kwa Jina la Allâh nakuzungua, Allâh Akuponye kutokana na kila maradhi yanayokudhuru, kutokana na shari ya kila nafsi au jicho la mwenye husuda, Allâh Akupe shifaa (ponyo).

(3) Najilinda kwa Maneno ya Allâh Yaliotimia dhidi ya shari ya Alivyoviumba.

(4) Kwa Jina la Allâh Ambalo hakidhuriki chochote pamoja na Jina Lake katika ardhi wala katika mbingu, Naye ni Msikizi, Mjuzi (wa yote).

﴿قَالَ مُوسَى مَا جِئْتُمْ بِهِ السِّحْرُ إِنَّ اللهَ سَيُبْطِلُهُ إِنَّ اللهَ لاَ يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ. وَيُحِقُّ اللهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ﴾.

Utazifuta kwa mafuta ya habalsoda, halafu aliyesihiriwa atakunywa na atajipaka kifuani na katika kipaji chake siku tatu; sihiri na mafundo yatabatilika Inshâ-allâh. Shaikhul-Islâm (Ibnu Taimiyyah) amefutu kujuzu kuandika Qur'âni au nyuradi na kuzifuta halafu kumpa mgonjwa anywe. [*Majmû'ul-Fatâwâ:* 19/64].

Njia Ya Tisa

Utaandika zunguo la sihiri kwa wino twahara – kama vile zafarani – katika chombo safi na utafuta kwa maji, na atakunywa na kuogea yule aliyefungwa kwa siku kadhaa, fundo litafunguka Inshâ-allâh.

Tafauti Baina Ya Fundo, Kutodisa (Uume Kutosimama) Na Udhaifu Wa Nguvu Za Kiume

*** *Kwanza*: *fundo*:**
Aliyefungwa huhisi nishati na uwezo kamili wa kumjamii mkewe, bali uume husimama maadamu yu mbali naye, lakini anapomkaribia na akataka kumkaribia, husinyaa na kutoweza kumjamii.

*** *Kutodisa*:**
Kutodisa maana yake ni mwanamume kutoweza tendo la kujamii, ima awe karibu au mbali na mkewe, bali uume hausimami aslan.

*** *Udhaifu wa nguvu za kiume*:**
Mwanamume huwa hawezi kumjamii mkewe ela katika nyakati mbalimbali, na kujamii kwenyewe humalizika katika muda mchache tu pamoja na uume kusinyaa baada ya kujimai.

Tiba

Ama kufungwa (kwa mafundo), tumetaja njia tisa za kutibu hapo mbele kidogo. Ama kutodisa, hutibiwa kwa madaktari (iwapo wataweza). Ama udhaifu wa nguvu za kiume, tiba yake ni hii:

1. Utachukua kilo moja ya asali safi ya nyuki na gramu 200 za mkate wa nyuki. [Bora iwe ni baada tu ya kutoka mzingani, na kila ikiketi sana ndipo ikosapo thamani nguvu zake].
2. Utaisomea *Sûratul-Fâtihah*, *Sûratu Alam Nashrah* na *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*).
3. Mgonjwa atakula kila siku vijiko vitatu vilivyojaa kabla ya kula, kijiko kimoja kabla ya chakula cha mchana na kijiko kimoja kabla ya chakula cha jioni kwa muda wa saa.
4. Ataendelea hivyo kwa muda wa mwezi mmoja au miwili kulingana na kiwango cha udhaifu. Na atapona kwa Idhini ya Allâh.

*****

KUTIBU BAADHI YA AINA ZA UTASA

**** Utasa kwa mwanamume*:**

Utasa upo aina mbili:

Kwanza: utasa wa kiungo, hutibiwa kwa madaktari kama wakiweza kuutibu.

Pili: Utasa kwa sababu ya mguso wa jini ndani ya mwili wa Mwanaadamu, utasa aina hii hutibiwa kwa Qur'âni, dua na nyuradi.

Yafahamika kuwa, utendaji wa kuzalisha – kwa Idhini ya Allâh – ni kiwango cha wadudu wa manii kwa mwanamume wawe ni zaidi ya milioni ishirini (20,000,000) katika sentimita mraba. Mara nyingine shetani huwa akiyabana mapumbu ya mwanamume yanayotoa wadudu wa manii, au huwa akitumia njia nyingine mapumbu hayo yakatoa kiwango kidogo chini zaidi ya itakiwavyo, ikawa ndio sababu ya kutozalisha. Wakati wadudu wa manii wanapogura kutoka katika mapumbu hadi katika kibofu cha manii, wadudu hawa huhitajia kiowevu cha ute kinachotolewa na tezi ya koubar na kuimimina katika kibofu cha manii wakati ambapo wadudu hawa waliohifadhiwa katika kibofu hiki huwa wakiila. Na hapa shetani huwa ana tabia nyingine katika tezi hiyo ya koubar, huwa akiizuwia kutoa kiowevu cha ute, hapobasi wale

wadudu waliohifadhiwa katika kibofu cha manii hawapati chakula, basi huwa wakifa na ikawa vigumu mtu kuzaa.

UTATOFAUTISHA VIPI BAINA YA UTASA WA KIMAUMBILE NA UTASA ULIOSABABISHWA NA JINI?

**** Utasa unaosababishwa na jini dalili zake ni hizi*:**
1. Kuhisi dhiki kifuani hasa baada ya alasiri, na pengine huendelea hadi katikati ya usiku.
2. Kutokuwepo kiakili na usahaulifu.
3. Kuhisi maumivu chini ya pingili la uti wa mgongo.
4. Wasiwasi na hamaniko usingizini.
5. Usingizini mwake huwa akiona ndoto za kutisha.

*****

**** Utasa kwa mwanamke*:**
Vilevile utasa kwa mwanamke upo aina mbili:
Kwanza: utasa wa kimaumbile, hivi ndivyo alivyoumbwa na Allâh awe tasa.

Pili: utasa uliosababishwa na jini aliyestakiri katika kizazi cha mwanamke, kwa namna ya kuyaharibu mayai, na hapo isiwezekane kuzaa.

Au atamwacha mpaka mimba ikamilike, lakini baada ya miezi kadhaa ya mimba, shetani huukanyaga mshipa katika kizazi cha mwanamke damu ikateremka na ikasababisha kuavya (kuharibu mimba). Mara nyingi kuavya kunakokaririwa huwa kumesababishwa na jini. Hali nyingi za aina hii zimetibiwa. Imethubutu katika *S̲ah̲îh̲ul-Bukhârî* na Muslim kuwa shetani hupita ndani ya Mwanaadamu mapitio ya damu. Bukhârî (4/282 *Fat-h̲i*) na Muslim (14/155 *Nawawy*)].

TIBA YA UTASA
1. Utamrekodia zunguo katika kanda awe akisikiliza mara tatu kila siku.
2. Asome *Sûratus-Sâffâti* asubuhi au aisikilize.

3. Asome *Sûratul-Ma'ârij* wakati wa kulala au aisikilize.

4. Utamsomea katika mafuta ya habalsoda: *Sûratul-Fâtihah* – *Âyatul-Kursy* – mwisho wa *Sûratul-Baqarah* – mwisho wa *Sûratu Âli 'Imrân* – *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*). Halafu atajipaka kifuani mwake, katika kipaji chake na katika pingili la uti wa mgongo kabla ya kulala.

5. Kisha utamsomea Aya zizo hizo katika asali safi, kila siku awe akinywa kijiko kimoja kilichojaa kabla ya kula.

Ataendelea hivyo miezi kadhaa pamoja na kufwata Amri za Allâh Mtukufu moyoni mwake ili awe miongoni mwa wakweli ambao Allâh Huwaponya kwa Qur'âni Tukufu. Allâh Anasema:

﴿وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ﴾.

"Tunateremsha katika Qur'âni ambayo ni ponyo na rehma kwa Waumini." [17: 82].

Allâh Akawahusisha Waumini mbali na wengine. Hali kama hizi zimewahi kutibiwa kwa Fadhila za Allâh Mtukufu.

*****

TIBA YA KUSHUSHA UPESI

Kushusha upesi huenda likawa ni jambo la kawaida kwa mwanamume. Madaktari huwa wakitibu kwa njia mbalimbali, ikiwemo:

1. Kutumia baadhi ya marahamu (krimu) zinazofanya hisia zisiwe kali.
2. Kufikiria jambo fulani wakati wa kujamii.
3. Kuyafumbua baadhi ya maswala magumu ya ki-hisabati wakati wa kujamii.

Na pia huenda ni kwa sababu ya kichocheo anachokifanya jini ndani ya tezikibofu (*prostate gland*), na hapo akashusha haraka. Hali hii hutibiwa hivi:

1. Kila baada ya Swala ya alfajiri utasoma mara mia (100):

﴿لاَ إِلـهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَ لَهُ الحَمْدُ وَ هُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ﴾.

Lâ ilâha illallâhu wahdahû lâ sharîka lah, lahulmulku walahulhamdu wahuwa 'alâ kulli shay-in qadîr.[1]

2. Utasoma *Sûratul-Mulk* kabla ya kulala au utaisikiliza.
3. Kila siku utaisoma *Âyatul-Kursy* mara nyingi.
4. Utasoma dua hizi kila asubuhi mara tatu:

﴿أَعُوْذُ بِكَلِمَاتِ اللهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ﴾.

A'ûdhu bikalimâtillâhittâmmâti minsharri mâkhalaq.[2]

﴿بِسْمِ اللهِ الَّذِي لاَ يَضُرُّ مَعَ اسْمِهِ شَيْءٌ فِي اْلأَرْضِ وَلاَ فِي السَّمَاءِ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ﴾.

Bismillâhilladhî lâ yadhurru ma'asmihî shay-un fil-ardhi walâ fissamâ, wahuwassamî 'ul'alîm.[3]

﴿أَعُوْذُ بِكَلِمَاتِ اللهِ التَّامَّةِ مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ وَ هَامَّةٍ وَ مِنْ كُلِّ عَيْنٍ لاَمَّةٍ﴾.

A'ûdhu bikalimâtillâhittâmmati minkulli shaytâniwwahâmmah, waminkulli 'aynillâmmah.[4]

Mara tatu, kwa muda wa miezi mitatu kwa uchache.

*****

KINGA DHIDI YA SIHIRI

Yaeleweka kuwa, sihiri na mafundo mara nyingi hutokea kwa barobaro wakati anapooa, hasa anapoishi katika jamii iliyo na wachawi waovu. Na hapa linakuja swali: "Je, yawezekana maarusi wakajikinga dhidi ya sihiri hata wakifanyiwa sihiri hawataweza kuathirika?"

---

[1] Hakuna mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allâh Peke Yake, Ufalme ni Wake na Himdi zote ni Zake, Naye ni Muweza juu ya kila kitu.

[2] Najilinda kwa Maneno ya Allâh Yaliotimia dhidi ya shari ya Alivyoviumba.

[3] Kwa Jina la Allâh Ambalo hakidhuriki chochote pamoja na Jina Lake katika ardhi wala katika mbingu, Naye ni Msikizi, Mjuzi (wa yote).

[4] Najilinda kwa Maneno ya Allâh Yaliotimia dhidi ya kila shetani, mdudu au mnyama anayedhuru, na dhidi ya kila jicho lenye husuda.

Jawabu ni: Ndio. Hilo lawezekana, na nitazitaja kinga hizi Inshâ-allâh. Lakini kabla ya hapo, napenda kuwatajia tukio hili:

Palikuwepo na barobaro mmoja akilingania katika Dini ya Allâh ndani ya kijiji chake na nje yake. Mara nyingi akiwahutubia watu na akiwalingania katika Tawhîd safi na Imani sahihi. Alikuwa akiwahadharisha kuenda kwa wachawi na akiwabainishia kuwa, sihiri ni ukafiri, na kwamba mchawi ni mtu khabithi anampiga vita Allâh na Mtume Wake. Kijijini mwao humo alikuwepo mchawi maarufu. Barobaro yeyote akitaka kuoa, humwendea mchawi huyo na akamweleza: “Mimi siku fulani nataka kuoa, kwa hivyo wataka nini?” Basi yule mchawi akitaka kiwango fulani cha mali, huyo barobaro humpa bila ya kusita. Bila hivyo, jaza yake huwa ni kufungiwa mkewe asiweze kumjamii, basi hapo atakuwa hana budi kumwendea mchawi huyu ili amfungulie sihiri. Lakini mara hii, kiwango kitapanda!

Basi yule barobaro mwenye msimamo, akawa akimpiga vita mchawi huyu waziwazi, akiyafedhehi mambo yake juu ya mimbari, katika mikusanyiko ya jumuia na makhsusi na akimtaja kwa jina hasa na huku akiwahadharisha watu wasimwendee. Barobaro huyu alikuwa hajaoa bado. Watu wakawa wakisubiri siku ya arusi yake ili waone kitakachotokea kwa mchawi dhidi yake, na je huyu barobaro mwenye msimamo aliyeshika Dini, ataweza kujihami dhidi ya mchawi huyu?!

Ikafika siku ya arusi. Kabla ya kuingia nyumbani, alinijia na akanihadithia kisa chote. Akanambia: “Mchawi yuwanitisha na watu wote kijijini wanasubiri ushindi ni wa nani. Basi nini rai yako? Je, waweza kunipa kinga dhidi ya mchawi yule? Pamoja na kufahamu kuwa mchawi atamaliza juhudi yake yote na atafanya sihiri kali zaidi anayoweza kuifanya, kwa sababu mimi mara nyingi nilikuwa nikimtweza mbele ya watu.”

Nikamwambia: “Ndio, naweza – Inshâ-allâh – lakini kwa sharti.” Akauliza: “Sharti gani hiyo?” Nikamwambia: “Utamtumia salamu mchawi umwambie: “Mimi nitaowa siku fulani, nami nakupa changamoto, kwa hivyo fanya unavyotaka, na kama huwezi njoo pamoja

na unayemtaka katika wachawi," mapambano haya uyafanye waziwazi mbele ya watu."

Yule barobaro akauliza kwa kusitasita: "U-n-a h-a-k-i-k-a uyasemayo?" Nikamwambia: "Ndio, nina hakika kuwa ushindi ni wa Waumini, udhalilifu na unyonge ni wa waovu."

Na kweli, barobaro huyu alimtumia ujumbe mchawi akimpa changamoto afanye analotaka, na akamjulisha siku ya arusi yake. Watu wakawa wanasuburi kwa hamu na shauku siku hii nzito ifike.

Yule barobaro nikampa baadhi ya kinga hizi – ambazo nitazitaja Inshâ-allâh. Matokeo yakawa ni kuwa yule barobaro alioa na akaingia kwa mkewe, wala hakuna sihiri ya mchawi yeyote wala vitimvi vya mchimvi yeyote vilivyomuathiri. Watu wakastaajabu na kushangaa. Jambo hili likawa ni ushindi kwa Imani sahihi, ni dalili wazi juu ya uthibiti wa watu wake na ni himaya ya Allâh kwao mbele ya watu wa ubatilifu. Ikatukuka shani ya barobaro huyu kwa jamaa, marafiki na watu wa kijiji chake, haiba na utisho wa yule mchawi ikaanguka machoni mwa watu.

Allâhu Akbar walillâhil-hamd. Nusura na ushindi unatoka kwa Allâh Pekee.

***Kinga zenyewe ni hizi*:**

Kinga Ya Kwanza

Utakula tende saba za '*ajwah* (aina ya tende nzuri mno) kabla ya kula chakula. Ukiweza ziwe ni tende za Madina itakuwa bora, usipoweza basi tende yoyote ya '*ajwah* utakayoipata ni sawa. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿مَنِ اصْطَبَحَ بِسَبْعِ تَمَرَاتِ عَجْوَةٍ، لَمْ يَضُرَّهُ ذَلِكَ اليَوْمَ سَمٌّ، وَلاَ سِحْرٌ﴾.

"Atakayekula asubuhi tende saba za '*ajwah*, katika siku hiyo hatodhurika na sumu wala sihiri." [Bukhârî (10/249)].

Kinga Ya *Pili*
Udhu

Sihiri haimuathiri Muislamu aliyetawadha. Muislamu aliyetawadha amehifadhiwa na Malaika watokao kwa Allâh.

‘Abdullâh bin ‘Abbâs رضي الله عنهما amesimulia: “Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

“Vitwahirisheni viwiliwili hivi, Allâh Atawatwahirisha. Hakuna mja anayelala ilihali yuko <u>twahara</u> ispokuwa Malaika hulala naye katika nguo yake ya ndani. Hatogeuka wakati wowote usiku ispokuwa huomba: “Ewe Mola, msamehe mja Wako; kwani <u>alilala akiwa twahara.</u>” [<u>T</u>abarâny, *isnadi* yake ni *jayyid* kama alivyosema al-Mundhiry katika *at-Targhîb:* 2/13].

﴿طَهِّرُوا هذِهِ الأَجْسَادَ طَهَّرَكُمُ الله فَإِنَّهُ لَيْسَ عَبْدٌ يَبِيتُ طَاهِراً إلاَّ بَاتَ مَعَهُ مَلَكٌ فِي شِعَارِهِ لاَيَنْقَلِبُ سَاعَةً مِنَ اللَّيْلِ إلاَّ قَالَ: اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِعَبْدِكَ فَإِنَّهُ بَاتَ طَاهِراً﴾.

Kinga Ya *Tatu*
Kuhifadhi Swala Ya Jamaa

Kuswali Swala ya jamaa, humfanya Muislamu kuwa katika amani na kumueka mbali na shetani, na kuidharau humfanya shetani akamteka Mwanaadamu, na atekwapo husibiwa na wazimu au sihiri au jambo lingine lolote analoweza shetani.

Abud-Dardâ ﷺ amesimulia: “Nilimsikia Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akisema:

“Hakupatikani watu watatu kijijini wala jangwani wasiosimamisha Swala, ispokuwa shetani huwa <u>amewateka</u>. Shikamana na jamaa; kwani mbwa mwitu humla aliye mbali (pekee).” [Bukhârî (3/34 *Fat-hi*) na

﴿مَا مِنْ ثَلَاثَةٍ فِي قَرْيَةٍ وَلَا بَدْو، لَا تُقَامُ فِيهِمُ الصَّلَاةُ إِلَّا قَدِ اسْتَحْوَذَ عَلَيْهِمُ الشَّيْطَانُ، فَعَلَيْكَ بِالجَمَاعَةِ، فَإِنَّمَا يَأْكُلُ الذِّئْبُ الْقَاصِيَةَ﴾.

Muslim (6/63 *Nawawy*)].

Kinga ya nne
Kuswali Usiku

Anayetaka kuikinga nafsi yake na sihiri, basi asimame (kuswali) sehemu katika usiku, wala asiache, kwa sababu kuacha kuswali usiku shetani humsaliti Mwanaadamu, na utakaposalitiwa na shetani, utakuwa ni udongo wa rutuba ya sihiri kukuathiri.

'Abdullâh bin Mas'ûd ﵁ amesimulia: "Kulitajwa mtu mbele ya Mtume صلى الله عليه وآله وسلم , akaambiwa: "Hajaacha kulala mpaka asubuhi," yaani ameamka asubuhi tu kwa ajili ya Swala, "hakusimama kuswali Swala ya usiku." Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akasema:

﴿بَالَ الشَّيْطَانُ فِي أُذُنَيْهِ﴾.

"shetani amemkojolea masikioni mwake." [Abû Dâwûd: 1/150].

Sa'îd bin Man<u>s</u>ûr amepokea kwa 'Abdullâh bin 'Umar رضي الله عنهما : "Hakupambazukiwa mtu bila kuswali witri, ispokuwa huamka na kichwani mwake muna kamba kiasi cha dhiraa sabiini." [Bukhârî (3/25 *Fat-<u>h</u>i*)].

Kinga Ya Tano
Kujilinda Wakati Wa Kuingia Chooni

shetani huwa akiotea fursa ya Muislamu kuwa chooni katika mahali hapa pachafu ambapo ndipo maskani ya mashetani na akimsaliti. Mmoja katika mashetani alinambia kuwa, yeye alimuingia mtu kwa sababu hakujilinda wakati wa kuingia chooni, basi akamsaliti na akamuingia. Lakini Allâh Alinisaidia dhidi yake, nikamwamuru atoke na akatoka *Al<u>h</u>amdulillâh*.

Mmoja katika majini alinambia: "Allâh Amewapa nyinyi silaha yenye nguvu mnayoweza kutumaliza nayo lakini hamuitumii." Nikamwuliza: "Ni silaha gani hiyo?" Akanambia: "Nyuradi za Mtume."

Imeswihi kutoka kwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alikuwa anapotaka kuingia chooni, husema:

“Mola wangu, najilinda Kwako dhidi ya mashetani wachafu waume na wake.” [Bukhârî (1/292 *Fat-hi*) na Muslim (4/70 *Nawawy*)].

﴿اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الخُبُثِ وَالخَبَائِثِ﴾.

Kinga Ya Sita
Kujilinda Wakati Wa Kuingia Katika Swala

Jubair bin Muṯ‘im رضي الله عنه alimuona Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akiswali, akasema:

“*Allâhu Akbaru kabîra walhamdu lillâhi kathirâ,*” mara tatu, ***“subhânallâhi bukratawwa-asîlâ,”*** mara tatu. ***“A‘ûdhu billâhi minash-shaitânirrajîm min nafkhihî wanafthihî wa hamzihî.”*** [(1)]

﴿اللهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا وَالحَمْدُ لله كَثِيرًا﴾. ثَلَاثًا

﴿سُبْحَانَ اللهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا﴾. ثَلَاثًا

﴿أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ مِنْ نَفْخِهِ وَنَفْثِهِ وَهَمْزِهِ﴾.

[Abû Dâwûd (1/203). al-Albâny ameisahihisha katika takhriji ya *al-Kalimut-Tayyib* (55).]

Kinga Ya Saba
Kumkinga Mwanamke Wakati Wa Kufunga Naye Ndoa

Baada ya kufunga ndoa na mkeo, weka mkono wako wa kulia juu ya kipaji chake na useme:

“Allâhumma innî as-aluka khairahâ, wakhaira mâ jabaltahâ ‘alaih, wa-a‘ûdhu bika min sharrihâ, washarri mâ jabaltahâ ‘alaih.”[(2)]

﴿اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَهَا وَخَيْرَ مَا جَبَلْتَهَا عَلَيْهِ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا وَشَرِّ مَا جَبَلْتَهَا عَلَيْهِ﴾.

---

(1) Najilindia kwa Allâh dhidi ya shetani aliyelaaniwa; kutokana na kunong’oneza kwake, kupuliza kwake katika nyoyo za Wanaaadamu na wasiwasi wake.

(2) Mola wangu, nakuomba kheri yake (mke) huyu na kheri ya maumbile Uliyomuumba nayo. Najilinda Kwako shari yake, na shari ya maumbile Uliyomuumba nayo.

Kinga Ya Nane
Kuyafungua Maisha Ya Unyumba Kwa Swala

‘Abdullâh bin Mas‘ûd ﵁ amesema: “Unapomwendea mkeo – yaani siku ya kuingia kwake – mwamuru aswali nyuma yako rakaa mbili,[1] na useme:

﴿اللَّهُمَّ بَارِكْ لِي فِي أَهْلِي وَبَارِكْ لَـهُمْ فِيَّ. اللَّهُمَّ اجْمَعْ بَيْنَنَا مَا جَمَعْتَ بِخَيْرٍ، وَفَرِّقْ بَيْنَنَا إِذَا فَرَّقْتَ إِلَى خَيْرٍ﴾.

Kinga Ya Tisa
Kujikinga Wakati Wa Kujimai

‘Abdullâh bin ‘Abbâs رضي الله عنهما amesimulia: “Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema: **“Lau mmoja wenu anapomjamii mkewe akasema:**

“Bismillâh, Allâhumma jannibnash-shaitân, wajannibish-shaitâna mâ razqtanâ.” [2]

﴿بِسْمِ اللهِ اللَّهُمَّ جَنِّبْنَا الشَّيطَانَ وَجنِّبِ الشَّيطانَ ما رزَقْتَنَا﴾.

wakajaaliwa mtoto baina yao, (shetani) hatoweza kumdhuru.” Bukhârî (1/291 *Fat-hi*)].

Mmoja katika majini alinambia baada ya kusilimu na kutubia kwa Allâh, kwamba yeye alikuwa akishirikiana na mtu huyu – mgonjwa – katika kumjamii mkewe, kwa sababu alikuwa haisomi dua hii!

Subhânallâh, tuna makanzi mangapi yenye thamani, lakini hatujui thamani yake!!

Kinga Ya Kumi

Utatawadha kabla ya kulala, utasoma *Âyatul-Kursy* na utamtaja Allâh Mtukufu mpaka upatwe na usingizi. Imethubutu kuwa, shetani alimwambia Abû Huraira ﵁ : “Atakayesoma *Âyatul-Kursy* kabla ya kulala; ataendelea kuwa katika Hifadhi ya Allâh, wala hakuna shetani

---

[1] Yaani umswalishe rakaa mbili, wewe uwe Imamu, yeye maamuma.

[2] Kwa Jina la Allâh, Mola wetu, Tuepushe na shetani na Umuepushe shetani katika Utakachoturuzuku.

atakayemkaribia mpaka apambazukiwe. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akathibitisha juu ya hilo na akasema:

﴿صَدَقَكَ وَهُوَ كَذُوبٌ﴾.

"Amekwambia kweli naye ni muongo." Bukhârî (4/487 *Fat-hi*)].

Kinga Ya Kumi Na Moja

Baada ya Swala ya alfajiri utasema mara mia (100):

﴿لاَ إِلـهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَ لَهُ الحَمْدُ وَ هُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ﴾.

Lâ ilâha illallâhu wahdahû lâ sharîka lah, lahulmulku walahulhamdu wahuwa 'alâ kulli shay-in qadîr. (1)

Imethubutu kuwa Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema – mwenye kusema hivyo – :

﴿كَانَتْ لَهُ عَدْلَ عَشْرِ رِقَابٍ، وَكُتِبَ لَهُ مِائَةُ حَسَنَةٍ، وَمُحِيَتْ عَنْهُ مِائَةُ سَيِّئَةٍ، وَكَانَتْ لَهُ حِرْزًا مِنَ الشَّيْطَانِ، يَوْمَهُ ذَلِكَ حَتَّى يُمْسِيَ، وَلَمْ يَأْتِ أَحَدٌ بِأَفْضَلَ مِمَّا جَاءَ إِلَّا رَجُلٌ عَمِلَ أَكْثَرَ مِنْهُ﴾.

"Itakuwa ni sawa na kutoa watumwa kumi, ataandikiwa hasanati mia, atafutiwa mabaya mia na itakuwa ni hifadhi kwake dhidi ya shetani mchana wake huo mpaka afike jioni. Wala hakuna yeyote aliyefanya jambo bora kuliko alilofanya yeye ispokuwa mtu aliyefanya kwa wingi zaidi yake." Bukhârî (6/338 *Fat-hi*) na Muslim (17/17 *Nawawy*)].

Kinga Ya Kumi Na Mbili

Unapoingia Msikitini utasema:

﴿أَعُوْذُ بِاللهِ الْعَظِيْمِ وَبِوَجْهِهِ الْكَرِيْمِ وَ

A'ûdhu billâhil 'adhwîm wabiwajhihilkarîm wasultânihilqadîm minash-

---

(1) Hakuna mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allâh Peke Yake, Ufalme ni Wake na Himdi zote ni Zake, Naye ni Muweza juu ya kila kitu.

shaytânirrajîm.[1] | سُلْطَانِهِ الْقَدِيْمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ﴾.

Imethubutu kuwa, Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

"Atakayesema hivyo, shetani husema: "Amehifadhiwa dhidi yangu siku nzima." [Abû Dâwûd: 1/127, Imâm Nawawy ameifanya ni *Hasan*].

﴿فَمَنْ قَالَ ذَلِكَ قَالَ الشَّيْطَانُ: حُفظ مِنِّي سَائِرَ الْيَوْمِ﴾.

Kinga Ya Kumi Na Tatu

Asubuhi na jioni utasema:

Bismillâhilladhî lâ yadhurru ma'asmihî shay-un fil-ardhi walâ fissamâ, wahuwassamî'ul'alîm.[2]

﴿بِسْمِ اللهِ الَّذِي لاَ يَضُرُّ مَعَ اسْمِهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلاَ فِي السَّمَاءِ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ﴾.

Mara tatu. [Tirmidhy 5/133, amesema Hadîth yake ni *Hasan Gharîb Sahîh*].

Kinga Ya Kumi Na Nne

Unapotoka nyumbani utasema:

Bismillâhi tawakkaltu 'alallâh, walâ hawla walâ quwwata illâ billâh [3]

﴿بِسْمِ اللهِ توكَّلْتُ عَلَى اللهِ، ولا حوْلَ ولا قُوةَ إلاَّ بِاللهِ﴾.

Utakavyosema hivyo, unaambiwa: "Umetoshelezwa, umekingwa na umeongozwa." shetani hukukimbia huku akimwambia mwenzie: "Vipi

---

[1] Najilinda kwa Allâh Mtukufu, na kwa Uso Wake Mtakatifu, na kwa Ufalme Wake wa kale, dhidi ya shetani aliyelaaniwa.

[2] Kwa Jina la Allâh Ambalo hakidhuriki chochote pamoja na Jina Lake katika ardhi wala katika mbingu, Naye ni Msikizi, Mjuzi (wa yote).

[3] Kwa Jina la Allâh, nimeegemea kwa Allâh, hakuna jinsi ya kuepuka maasia wala nguvu ya kufanyia ibada ela ni kwa Msaada wa Allâh.

utamwingia mtu aliyeongozwa, aliyekifiwa na aliyekingwa?" [Abû Dâwûd: 4/325 na Tirmidhy 5/154, na akasema ni Hasan Sahîh].

Kinga Ya Kumi Na Tano

Utasema asubuhi na jioni:

A'ûdhu bikalimâtillâhittâmmâti minsharri mâkhalaq.(1) ﴿أَعُوْذُ بِكَلِمَاتِ اللهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ﴾.

Hizi ni hifadhi zenye faida, zenye kinga ya sihiri na mafundo kwa ujumla, hasa zikitekelezwa kwa yakini na ikhlasi.

Sampuli Ya Kiutendaji Ya Kufungua Fundo

Hali ziko nyingi na sampuli pia ziko nyingi, lakini nitatoa sampuli moja kwa kuhofia kurefusha.

Nilijiwa na shababu pamoja na nduguye aliyeowa yapata wiki moja, lakini akashindwa kumjamii mkewe, akaenda kwa wapiga ramli na matapeli, lakini hakufanikiwa. Nilipofahamu kuwa aliwaendea watu hao, kwanza nilimtaka atubie toba ya kweli, na awakadhibishe matapeli hawa ili Imani yake iwe sahihi na tiba imfae. Akanambia: "Baada ya kuwaendea nilizidi yakini juu ya uwongo wao na udhaifu wao." Nikamsomea zunguo. Nikataka waniletee majani saba mabichi ya mkunazi, hawakupata. Nikachukua majani saba ya mti wa kafuri, halafu wakayaponda baina ya mawe mawili nami nikayatia katika maji, nikayasomea *Âyatul-Kursy* na *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu Ahad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*), kisha nikamwamuru anywe na akiogea, naye akafanya hivyo, sihiri ikabatilika na fundo likafunguka papo hapo. *Alhamdulillâh* mwanzo na mwisho.

Sihiri Ya Kufunga Inageuka Kuwa Wazimu

Alikuwepo barobaro aliyekuwa ana akili yake timamu. Lakini siku alipoingia kwa mkewe, hali yake ilibadilika, akatokezewa na hali ya kufungwa halafu ikabadilka na kuwa wazimu. Kugeuka hali za sihiri siku hizi hutokea sana kwa sababu ya ujinga wa wachawi kutozielewa

---

(1) Najilinda kwa Maneno ya Allâh Yaliotimia dhidi ya shari ya Alivyoviumba.

fani mbalimbali za sihiri. Kama kisa cha yule mwanamke aliyemwendea mchawi ili amfanyie mumewe sihiri itakayomfanya akiwachukia wanawake wote ela yeye. Na kweli alimfanyia sihiri na akamwekea mumewe katika chakula. Mara yule mumewe akawachukia wanawake wote mpaka mkewe pia. Bali ilifikia hali ya kumtaliki. Yule mke akamwendea mchawi mara ya pili ili amfungulie fundo, lakini alikuwa ameshakufa! Basi yule barobaro akawa anazurura mijini akipiga makelele kama mwendawazimu. Aliposomewa katika maji na majani ya mkunazi na akanywa pamoja na kuogea, alirudiwa na akili na akamwendea mkewe. *Alhamdulillâh*.

FASILI YA NANE
TIBA YA KIJICHO

1. Dalili za Qur'âni Tukufu juu ya taathira ya kijicho.
2. Dalili za Sunnah juu ya taathira ya kijicho.
3. Kauli za Ulamaa kuhusu uhakika wa kijicho.
4. Tofauti baina ya kijicho na husuda.
5. Majini wanawaonea kijicho Wanaadamu.
6. Tiba ya kijicho.
7. Sampuli ya kiutendaji ya kutibu kijicho.
8. Mkembe aliyekataa ziwa la mama yake.
9. Mtoto anasita kuzungumza.
10. Jambo la ajabu.

FASILI YA NANE
Tiba ya kijicho
Dalili za Qur'âni Tukufu juu ya taathira ya kijicho

1. Allâh Amesema:

"Akasema (Yaqubu): "Enyi wanangu! Msiingie Misri katika mlango mmoja, bali ingieni katika milango mbalimbali; wala sitowafaa chochote mbele ya Allâh. Hukumu haiko ela kwa Allâh tu. Kwake nimetegemea, na wategemeao wategemee Kwake." Walipoingia jinsi alivyowaamrisha baba yao, haikuwafaa kitu kwa Allâh, ispokuwa haja iliyokuwa katika nafsi ya Yaqubu aliitimiza (alikuwa akitaka asadifiane na Yûsuf). Bila shaka yeye (Yaqubu) alikuwa ni mwenye ilimu kwa sababu Tulimfundisha, lakini watu wengi hawajui." [12: 67,68].

﴿وَقَالَ يَا بَنِيَّ لاَ تَدْخُلُوا مِنْ بَابٍ وَاحِدٍ وَادْخُلُوا مِنْ أَبْوَابٍ مُتَفَرِّقَةٍ وَمَا أُغْنِي عَنْكُمْ مِنَ اللهِ مِنْ شَيْءٍ إِنِ الْحُكْمُ إِلاَّ للهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَعَلَيْهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ * وَلَـمَّا دَخَلُوا مِنْ حَيْثُ أَمَرَهُمْ أَبُوهُمْ مَا كَانَ يُغْنِي عَنْهُمْ مِنَ اللهِ مِنْ شَيْءٍ إِلاَّ حَاجَةً فِي نَفْسِ يَعْقُوبَ قَضَاهَا وَإِنَّهُ لَذُو عِلْمٍ لِمَا عَلَّمْنَاهُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لاَ يَعْلَمُونَ﴾.

al-Hâfidh Ibnu Kathîr رحمه الله تعالى amesema katika kutafsiri Aya hizi: "Allâh Yuwamzungumzia Yaqubu عليه السلام kwamba aliwaamuru wanawe – alipowaandaa pamoja na ndugu yao Benjamin kuelekea Misri – kuwa wote wasiingie katika mlango mmoja, bali waingie katika milango tofauti. Kwani ni kama alivyosema 'Abdullâh bin 'Abbâs, Muhammad bin Ka'bi, Mujâhid, adh-Dhahhâk, Qatâdah, as-Suddy na wengine wengi (wamesema): "Yeye aliwahofia wasije wakapatwa na kijicho; kwa sababu walikuwa ni wenye uzuri, jamali, hali nzuri na mandhari (ya kupendeza). Akawahofia watu wasije wakawaonea kijicho; kwani kijicho ni kweli, humteremsha shujaa juu ya farasi wake."

Kauli Yake: **"… wala sitowafaa chochote mbele ya Allâh."** Yaani: tahadhari hii haizuwii Qadari ya Allâh na Hukumu Yake; kwani Allâh Anapolitaka jambo hakhalifiwi wala hazuiwi.

﴿وَلَـمَّا دَخَلُوا مِنْ حَيْثُ أَمَرَهُمْ أَبُوهُمْ مَا كَانَ يُغْنِي عَنْهُمْ مِنَ اللهِ مِنْ شَيْءٍ إِلاَّ حَاجَةً فِي نَفْسِ يَعْقُوبَ قَضَاهَا﴾.

"Walipoingia jinsi alivyowaamrisha baba yao, haikuwafaa kitu kwa Allâh, ispokuwa haja iliokuwa katika nafsi ya Yaqubu aliitimiza (alikuwa akitaka asadifiane na Yûsuf)." [12: 67].

Ulamaa wamesema: "Huko ni kuwaepushia kijicho." – *kwa ufupi*. [*Tafsîr Ibnu Kathîr* (2/485)].

2. Allâh Amesema:

﴿وَإِنْ يَكَادُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَيُزْلِقُونَكَ بِأَبْصَارِهِمْ لَـمَّا سَمِعُوا الذِّكْرَ وَيَقُولُونَ إِنَّهُ لَمَجْنُونٌ﴾.

"Wale makafiri hukaribia <u>kukutelezesha</u> kwa <u>(udokozi wa) macho</u> yao wanaposikia mauidha (yako); na husema: "Yeye ni mwendawazimu."

al-<u>H</u>âfidh Ibnu Kathîr رحمه الله تعالى amesema: "'Abdullâh bin 'Abbâs, Mujâhid na wengineo wamesema: **<u>"Kukutelezesha"</u>** yaani: "Wanakuhusudu kwa macho yao, kwa maana wanakuhusudu kwa chuki zao juu yako, lau kama si kinga na himaya ya Allâh kwako dhidi yao, basi ungalidhurika."

Katika Aya hii, muna dalili kuwa kijicho kusibu kwake na taathira yake ni kweli kwa Amri ya Allâh kama zilivyopokewa – kuhusu jambo hilo – <u>H</u>adîth nyingi zilizopokewa kwa njia mbalimbali." [*Tafsîr Ibnu Kathîr* (4/410)].

DALILI ZA HADÎTH JUU YA TAATHIRA YA KIJICHO

1. Abû Huraira ﷺ amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

"Kijicho ni kweli." [Bukhârî (10/213) na Muslim (14/170 *Nawawy*)].

﴿العَيْنُ حَقٌّ﴾.

2. 'Âisha رضي الله عنها amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

"Jilindeni kwa Allâh dhidi ya kijicho; kwani kijicho ni kweli." [Ibnu Mâjah: 3508].

﴿استعيذوا بالله من العين، فإن العين حق﴾.

3. 'Abdullâh bin 'Abbâs رضي الله عنهما amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

"Kijicho ni kweli. Lau kama kuna kitu kingeweza kuitangulia *Qadar*, basi ingelitanguliwa na kijicho. Na mnapoombwa kuoga, basi ogeni." [Muslim (14/171 *Nawawy*)].

﴿الْعَيْنُ حَقّ، وَلَوْ كَانَ شَيْءٌ سَابِقَ الْقَدَرِ لَسَبَقَتْهُ الْعَيْنُ. وَإِذَا اسْتُغْسِلْتُمْ فَاغْسِلُوا﴾.

Yaani mmoja wenu anapotakiwa aoge kwa ajili ya nduguye Muislamu – kwa sababu yeye ndiye aliyemuonea kijicho – basi aitike mwito na amwogee.

4. Asmâ binti 'Umais رضي الله عنها amesema: "*Yâ Rasûlallâh*, hakika Banî Ja'far huwa wakipatwa na kijicho, je niwazungue?" Akamwambia:

"Ndio. Lau kama kuna kitu kingeweza kuitangulia *Qadar*, basi kingelitanguliwa na kijicho." [Ahmad (6/438), Tirmidhy (2059), Ibnu Mâjah (3510) na katika *Sahîhul-Jâmi'* ya al-Albâny (5286)].

﴿نَعَمْ، فَلَوْ كَانَ شَيْءٌ يَسْبِقُ القدرَ لَسَبَقَتْهُ الْعَيْنُ﴾.

5. Abû Dharri ﷺ amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿إِنَّ الْعَيْنَ لَتُولِعُ الرجلَ بِإِذْنِ اللهِ، فَيَتَصَاعَدُ حَالِقًا، ثُمَّ يَتَرَدَّى مِنْهُ﴾.

"Kijicho humsibu mtu – kwa Idhini ya Allâh – hata atakapopanda mahala pa juu, halafu huanguka kutoka juu kutokana na athari ya kijicho." [Ahmad na Abû Ya'lâ, imesahihishwa na al-Albâny katika *Sahîhul-Jâmi'* (1681) na katika *Sahîhah* (889)].

6. 'Abdullâh bin 'Abbâs رضي الله عنهما amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿الْعَيْنُ حَقٌّ تَسْتَنْزِلُ الحَالِقَ﴾.

"Kijicho ni kweli, humwangusha aliyekwea (aliyepanda juu ya jabali)." [Ahmad, Tabrâny na Hâkim. al-Albâny ameifanya ni *Hasan* katika *Silsilatus-Sahiha* 1250)].

7. Jâbir ﷺ amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿الْعَيْنُ تُدْخِلُ الرَّجُلَ الْقَبْرَ وَتُدْخِلُ الجَمَلَ الْقِدْرَ﴾.

"Kijicho humuingiza mtu kaburini, na humuingiza ngamia sufuriani." [Abû Nu'aim katika *Hilya*, al-Albâny ameifanya ni *Hasan* katika *Sahîhul-Jâmi'* (4144) na katika *Sahîha* (1249)].

Maana ya Hadîth hii ni kuwa, kijicho humsibu mtu kikamuuwa akafariki na akazikwa kaburini. Na humsibu ngamia akakaribia kufa, akachinjwa na akapikwa sufuriani.

8. Jâbir ﷺ amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

﴿أَكْثَرُ مَنْ يَمُوتُ مِنْ أُمَّتِي بعدَ قَضاءِ اللهِ وقَدَرِهِ بالعَيْنِ﴾.

"Wengi watakaokufa miongoni mwa Umma wangu – baada ya Hukmu ya Allâh na Qadari Yake – ni kutokana na kijicho." [Bukhârî katika *at-Târîkh* na al-

Albâny akaifanya ni *hasan* katika *Sah̲îh̲ul-Jâmi'* (1217)].

9. 'Âisha رضي الله عنها amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alikuwa akiniamuru nijizungue kujiepusha na kijicho." Bukhârî (10/170) na Muslim (2195)].

10. Anas bin Mâlik ﷺ amesema: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم ameruhusu katika kujizungua kujiepusha na kijicho, mchonoto[1] na vidonda vinavyotokezea ubavuni." [*an-Nihâyah:* 5/120].

11. Ummu Salamah رضي الله عنها amesimulia: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alimuona mjakazi usoni mwake ana baka. Akasema: **"(Mjakazi huyu) amepatwa na kijicho, mzungueni."** Bukhârî (10/171) na Muslim (2197)].

﴿بِهَا نَظْرَةٌ فَاسْتَرْقُوا لَهَا﴾.

12. Jâbir ﷺ amesema: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم aliwaruhusu kina Âlî H̲azmi katika zunguo la nyoka. Na akamwambia Asmâ binti 'Umais: **"Mbona naiyona miili ya wana wa ndugu zangu imekonda? Wanasibiwa na matatizo?"** (Asmâ binti 'Umais) akasema: "Hapana, lakini kijicho huwafikia upesi. Akasema: **"Wazungueni."** Nikamwendea (Mtume صلى الله عليه وآله وسلم) nikamwambia: "Mimi nitawazungua." Muslim (2198)].

﴿مَا لِي أَرَى أَجْسَامَ بَنِي أَخِي ضَارِعَةً ، أَتُصِيبُهُمُ الْحَاجَةُ؟﴾. قَالَتْ: لَا ، وَلَكِنَّ الْعَيْنَ تُسْرِعُ إِلَيْهِمْ، قَالَ: ﴿ارْقِيهِمْ﴾. قَالَ: فَعَرَضْتُ عَلَيْهِ، فَقَالَ: ﴿ارْقِيهِمْ﴾.

*****

[1] *Mchonoto*: ni kuumwa na kila chenye sumu kama vile nyoka, nge n.k.

KAULI ZA ULAMAA JUU YA SIHIRI

* al-<u>H</u>âfidh Ibnu Kathîr رحمه الله تعالى amesema: “Kusibu kwa kijicho na taathira yake, ni kweli kwa Amri ya Allâh.” [*Tafsîr Ibnu Kathîr* (4/410)].
* al-<u>H</u>âfidh Ibnu <u>H</u>ajar رحمه الله تعالى amesema: “Hakika ya kijicho ni kutazama kwa kupendezewa kulikochanganyika na husuda kutokana na uchafu wa maumbile kunakomletea madhara yule aliyetazamwa.” [*Fat-<u>h</u>ul-Bârî*: 10/200].
* Ibnul-Athîr رحمه الله تعالى amesema: “Husemwa: ‘fulani amesibiwa na kijicho’, atakapotazamwa na adui au hasidi na akamwathiri, akaugua kwa sababu yake.” [*an-Nihâyah*: 3/332].
* al-<u>H</u>âfidh Ibnul-Qayyim رحمه الله تعالى amesema: “Kikundi fulani kilicho na fungu dogo la usikizi na akili, kilikana suala la kijicho. Wakasema ni njozi tu za maoni zisizo na uhakika. Hawa ni katika watu wajinga zaidi kwa usikizi na akili, ni miongoni mwa wenye pazia nzito, tabia ngumu na walio mbali zaidi na maarifa kuhusu roho, nafsi, sifa zake, matendo yake na taathira zake. Umma wenye akili pamoja na tofauti ya mila na dini zao, hawapingi suala la <u>kijicho,</u> wala hawakani japo wanahitilafiana juu ya sababu zake na njia ya kuathiri <u>kijicho</u> …”

Kisha akasema: “Hapana shaka kuwa Allâh Ameumba katika viwiliwili na roho, nguvu na tabia mbalimbali, na Akajaalia katika tabia nyingi miongoni mwazo zina sifa maalumu na namna zinazoathiri. Wala haimkiniki kwa mwenye akili kupinga taathira ya roho katika viwiliwili, kwani ni jambo linaloonekana na kuhisiwa. Wewe utauwona uso (wa mtu) jinsi unavyokuwa mwekundu mno wakati anapotazamwa na mtu anayemuheshimu na kumstahi, na jinsi unavyokuwa rangi ya njano mno wakati anapomtazama anayemwogopa. Watu wameshuhudia anayeugua kutokana na kutazamwa na nguvu zake kudhoofika. Yote haya ni kwa kupitia taathira ya roho. Na kwa sababu ya kufungamana kwake sana na jicho, kitendo nacho kimenasibiwa kwake. Jicho sio lenye kufanya kitu, lakini taathira ni ya roho. Na roho zimetofautiana katika tabia, nguvu, namna na sifa zake makhsusi. Roho ya hasidi humdhuru aliyehusudiwa madhara ya wazi kabisa. Na kwa ajili hii, Allâh Amemwamuru Mtume Wake ajilinde Kwake dhidi ya shari yake (hasidi).

Taathira ya hasidi kwa kumletea adha aliyehusudiwa, ni jambo ambalo hakuna anayepinga ela ambaye yuko mbali na hakika ya Binadamu. Naye ndiye asili ya kusibiwa na kijicho. Nafsi chafu yenye husuda, hubadilika kwa namna chafu na humkabili aliyehusudiwa, basi ikamwathiri kwa sifa hiyo. Kitu mshabaha zaidi na jambo hili, ni nyoka. Sumu huwa imejificha ndani yake, anapomkabili adui yake, ndani yake hutoka nguvu za hasira na hubadilika kwa namna chafu inayoleta madhara.

Kuna ambao namna yao huwa na nguvu mpaka huathiri katika kuavya kiinitete (mimba changa), muna na wanaoathiri katika kuyapofusha macho kama alivyosema Mtume صلى الله عليه وآله وسلم kuhusu *al-Abtar* (aina ya nyoka mwenye mkia mfupi) na *dhittufyatain* (aina ya nyoka mwenye mistari myeusi):

﴿إِنَّهُمَا يَلْتَمِسَانِ الْبَصَرَ وَيُسْقِطَانِ الْحَبَلَ﴾.

"Hao wanatafuta macho na wanaavya mimba." Bukhârî (6/248) na Muslim (2233)].

Taathira mara huwa ni kwa kuwasiliana, kukabiliana, kwa kuona, roho kuelekea kwa anayemwathiri, kwa dua, zunguo na kujikinga na mara huwa ni kwa njozi za maono na kusawiri. Nafsi ya mwenye kijicho taathira yake haikomei katika kuona pekee, bali huenda akawa ni kipofu, akasifiwa jambo na nafsi yake ikaliathiri jambo hilo hata kama hajalionapo. Na wengi miongoni mwa wenye kijicho, huwaathiri wanaoonewa kijicho kwa wasifu bila ya kuona, nayo ni mishale inayotoka katika nafsi ya mwenye kijicho ikampata aliyeonewa kijicho, na mara nyingine humkosa. Ikimpata yuko wazi hana kinga, hapana budi humwathiri. Na ikimkuta ana tahadhari ameshika silaha isiyopenyeza mshale, haimwathiri, na pengine mishale ile humrudia mwenyewe.

Asili yake hutokana na mwenye kijicho kukiajabia kitu, halafu yakafwatia mabadiliko ya nafsi yake khabithi, halafu akijisaidia kupeleka sumu yake kwa kumtazama aliyeonewa kijicho. Na mtu huenda akajionea kijicho yeye mwenyewe, na huenda akaona kijicho bila ya kukusudia." – *kwa mukhtasari*. [*Zâdul-ma'âd:* 4/165].

*****

TOFAUTI BAINA YA KIJICHO NA HUSUDA

1. Hasidi (maana yake) imeenea zaidi kuliko mwenye kijicho. Mwenye kijicho ni hasidi makhsusi. Kwa hivyo, kila mwenye kijicho ni hasidi, lakini si kila hasidi ni mwenye kijicho. Kwa ajili hiyo, katika Qur'âni kumetajwa – katika *Sûratul-Falaq* – kujikinga na hasidi. Muislamu atapojikinga dhidi ya shari ya hasidi, na mwenye kijicho pia ameingia humo. Hii yatokana na ukubwa wa Qur'âni, kuajizisha na ufasaha wake.
2. Husuda yatokana na chuki, bughudha na kutamani mtu aondokewe na neema. Ama kijicho sababu yake ni kuajabia, kuona jambo ni kubwa na kupendezewa nalo.
3. Husuda na kijicho hushirikiana katika kuathiri kwa namna inavyosababisha madhara kwa aliyeonewa kijicho na aliyehusudiwa, na hukhitilafiana katika chanzo. Chanzo cha husuda ni moyo kuchomeka na kuiona neema ni kubwa kwa aliyehusudiwa na kutamani iondoke. Ama mwenye kijicho, chanzo chake ni mchocheo wa mtazamo wa jicho. Kwa hivyo, huenda likamsibu asiyemhusudu katika vitu visivyo na roho, wanyama, mazao au mali. Na pengine jicho lake huisibu nafsi yake mwenyewe. Kutazama kwake kitu kwa mtazamo wa kuajabia na kukodolea jicho pamoja na nafsi yake kubadilika, kwa mabadiliko hayo, humwathiri aliyeonewa kijicho.
4. Hasidi aweza kulihusudu jambo linalotarajiwa kutokea kabla ya kutokea kwake, wakati ambapo mwenye kijicho hawezi kuona kijicho ela katika jambo ambalo lipo hasa.
5. Mtu hawezi kuihusudu nafsi yake wala mali yake, lakini yuwaweza kuionea kijicho.
6. Hasadi haitokani ela katika nafsi khabithi yenye chuki. Lakini kijicho huenda kikatoka hata kwa mtu mwema kwa sababu ya kuajabia kwake jambo bila ya kupenda liondoke; kama ilivyotokea kwa 'Âmir bin Rabî'a alipomsibu Sahli bin Hunaif kwa kijicho, pamoja na kuwa 'Âmir رضي الله عنه ni miongoni mwa waliotangulia katika Uislamu, bali ni katika *Ahlu Badri* (Mashujaa wa Vita vya Badri).

Katika waliotafautisha baina ya husuda na kijicho, ni Ibnul-Jawzy, Ibnul-Qayyim, Ibnu Hajar, an-Nawawy na wengineo رحمهم الله تعالى.

Yapendeza Muislamu akionapo kitu kilichompendezea, akibarikie; yaani akiombee baraka; kitu hicho kiwe ni chake au ni cha mwingine; kwa kauli ya Mtume صلى الله عليه وآله وسلم katika Hadîth ya Sahli bin Hunaif: **"Si ungelimbarikia!"** (Bukhârî *Kitâbuttibb*)]. Yaani ungalimwombea baraka, kwa sababu dua hii huzuwia taathira ya kijicho.

MAJINI WANAWAONEA KIJICHO WANAADAMU

1. Abû Sa'îd al-Khudry ﷺ amesema: "Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alikuwa akijilinda dhidi ya kijicho cha majini kisha cha Wanaadamu. Zilipoteremka *Mu'awwidhâti* mbili (*Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*), alizitumia na akaziacha zisizokuwa hizo." [Tirmidhy (2059) na Ibnu Mâjah (3511)].
2. *Ummul-Mu'minîn* (Mama wa Waumini), Ummu Salamah رضي الله عنها amesimulia kuwa, Mtume صلى الله عليه وآله وسلم alimuona – nyumbani mwake – mjakazi aliye na baka leusi usoni mwake akasema:

﴿اسْتَرْقُوا لَهَا، فَإِنَّ بِهَا النَّظْرَةَ﴾.

"Mzungueni kwani amepatwa na kijicho." Bukhârî (10/171) na Muslim (97)].

al-Farrâ amesema: "Aliposema **baka**, yaani ni kijicho cha jini."

Kutokana na Hadîth hizi mbili, twaona kuwa kijicho hutokana na majini pia kama kinavyotokana na Binadamu. Kwa hivyo, yampasa Muislamu ataje Jina la Allâh anapovua nguo zake, au kujitazama katika kioo, au anapofanya jambo lolote ili ajiondolee madhara ya majini kutokana na kijicho au jambo lolote liwalo.

*****

TIBA YA KIJICHO

Muna njia nyingi za kutibu kijicho, nitazitaja baadhi yake:

Njia Ya Kwanza
Kuoga Mwenye Kijicho

Atakapojulikana mwenye kijicho, ataamriwa aoge halafu yachukuliwe maji yale (aliyoogea) na amiminiwe aliyeonewa kijicho kwa nyuma yake; atapona kwa Idhini ya Allâh.

Abû Umâmah bin Sahli bin Hunaif amesema: "Baba yangu Sahli bin Hunaif alioga huko Kharrâr (katika jangwa la Madina). Akalivua juba alilokuwa amelivaa, huku 'Âmir bin Rabi'a anamtazama. Sahli alikuwa mweupe mno ana ngozi nzuri. `'Âmir akasema: "Sijaonapo kama leo wala ngozi ya msichana bikira aliyefichwa (katika sitara yake)!" Sahli akaugua sana. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akaelezewa kuugua kwake. Akaambiwa: "Hainui kichwa." Akauliza:

"Mnamtuhumu yeyote?" ﴿هَلْ تَتَّهِمُونَ لَهُ أَحَدًا﴾.

Wakajibu: "Ndio, 'Âmir bin Rabî'a." Mtume صلى الله عليه وآله وسلم akamwita na akawa mkali juu yake, akasema:

"Ni kwa nini mmoja wenu anataka kumuua nduguye. Si ungalimbarikia. Mwogee!" ﴿عَلَامَ يَقْتُلُ أَحَدُكُمْ أَخَاهُ، هَلَّا إِذَا رَأَيْتَ مَا يُعْجِبُكَ بَركت؟ اغْتَسِلْ لَهُ﴾.

'Âmir akaosha uso wake, mikono yake, viwiko vyake, magoti yake, vidole vyake vya miguuni na ndani ya kikoi chake katika chombo; halafu akammiminia kwa nyuma yake. Sahli akapona papo hapo." [Ahmad, Nasâ-i na Ibnu Mâjah].

Kuna ikhtilafu katika neno '*ndani ya kikoi*'. Kumesemwa kuwa makusudio ni mahali pake katika mwili. Na kumesemwa kuwa ni dhakari yake. Pia kumesemwa kuwa ni nyonga yake; kwani ndipo mahali pa kufunga kikoi.

al-Qâdhî Ibnul-'Araby amesema: "Dalili ya wazi yenye nguvu, bali yenye haki ni: sehemu inayofwatia mwili katika kikoi." ['*Âridhatul-Ahwadhy*: 8/217].

Sifa Ya Kuoga

Ibnu Shihâb az-Zuhry رحمه الله تعالى amesema: "Josho tulilokuta Ulamaa wetu wakilisifu ni hili: Mwenye kijicho ataletewa chombo, ataingiza kiganja chake humo na atasukutua, halafu atatema chomboni, halafu ataosha uso wake katika chombo, kisha ataingiza mkono wake wa kushoto; atamiminia juu ya kiganja chake cha kulia katika chombo, Ataingiza mkono wake wa kulia, atamimina kwayo juu ya kiganja chake cha kushoto mara moja, kisha ataingiza mkono wake wa kushoto na atamimina juu ya kiwiko chake cha kulia, kisha ataingiza mkono wake wa kulia, atamimina juu ya kiwiko chake cha kushoto, kisha ataingiza mkono wake wa kushoto, atamimina kwayo juu ya mguu wake wa kulia, kisha ataingiza mkono wake wa kulia, atamimina juu ya mguu wake wa kushoto, kisha ataingiza mkono wake wa kushoto, atamimina kwayo juu ya goti lake la kulia, kisha ataingiza mkono wake wa kulia na atamimina kwayo juu ya goti lake la kushoto; yote hayo atayafanya kwenye chombo. Halafu ataingiza ndani ya kikoi chake kwenye chombo na chombo kile hakiwekwi chini, na yatamiminwa juu ya kichwa cha aliyesibiwa na kijicho kwa nyuma yake mmimino mmoja." [*as-Sunan* ya al-Bayhaqy: 9/252].

*****

Kuwekwa Sharia Ya Kuoga Mwenye Kijicho

1. Mtume صلى الله عليه وآله وسلم amesema:

"Kijicho ni kweli. Lau kama kuna kitu kingeweza kuitangulia *Qadar*, basi kingelitanguliwa na kijicho. Na mnapoombwa kuoga, basi ogeni." [Muslim (14/171 *Nawawy*)].

﴿الْعَيْنُ حَقٌّ، وَلَوْ كَانَ شَيْءٌ سَابِقَ الْقَدَرِ لَسَبَقَتْهُ الْعَيْنُ. وَإِذَا اسْتُغْسِلْتُمْ فَاغْسِلُوا﴾.

2. 'Âisha رضي الله عنها amesema: "Mwenye kijicho alikuwa akiamriwa atawadhe kisha maji yale aogee aliyesibiwa na kijicho." [Abû Dâwûd 3880].

Kutokana na Hadîth hizi mbili na nyinginezo, muna Sharia ya kutawadha au kuoga kwa mwenye kijicho kwa aliyemuonea kijicho.

Njia Ya Pili

Utauweka mkono wako juu ya kichwa cha aliyesibiwa na kijicho na utasoma:

Bismillâhi arqîk, Wallâhu yashfîka min kulli dâ-in yu'dhîk, wamin sharri kulli nafsin aw 'aini hâsid, Allâhu yashfîk.[(1)]

﴿بِسْمِ اللهِ أَرْقِيْكَ وَاللهُ يَشْفِيْكَ مِنْ كُلِّ دَاءٍ يُؤْذِيْكَ وَ مِنْ شَرِّ كُلِّ نَفْسٍ أَوْ عَيْنِ حَاسِدٍ اللهُ يَشْفِيْكَ﴾.

Njia Ya Tatu

Utauweka mkono wako juu ya kichwa cha aliyesibiwa na kijicho na utasoma:

Bismillâhi yubrîk, wamin kulli dâ-in yashfîk, wamin sharri hâsidin idhâ hasad, waminsharri kulli dhî 'ayn.[(2)]

﴿بِسْمِ اللهِ يُبْرِيْكَ وَ مِنْ كُلِّ دَاءٍ يَشْفِيْكَ وَ مِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ وَ مِنْ شَرِّ كُلِّ ذِي عَيْنٍ﴾.

Njia Ya Nne

Utauweka mkono wako juu ya kichwa cha aliyesibiwa na kijicho na utasoma:

Allâhumma rabbannâs, adh-hibilba-s, washfi Antasshâfî, lâ shifâ-a illâ shifâ-uk, shifâ-allâyughâdiru saqamâ walâ alamâ.[(3)]

﴿اللَّهُمَّ رَبَّ النَّاسِ أَذْهِبِ الْبَأْسَ وَ اشْفِ أَنْتَ الشَّافِي لاَ شِفَاءَ إِلاَّ شِفَاؤُكَ شِفَاءً لاَ

[(1)] Kwa Jina la Allâh nakuzungua, Allâh Akuponye kutokana na kila maradhi yanayokudhuru, kutokana na shari ya kila nafsi au jicho la mwenye husuda, Allâh Akupe shifaa (ponyo).

[(2)] Kwa Jina la Allâh, Allâh Akupe nafuu, Akuponye kila maradhi na Akuondoshee shari ya hasidi anapohusudu na kutokana na shari ya kila kijicho.

[(3)] Ewe Mola, Mlezi wa watu, Ondosha huzuni, Ponya, Wewe Ndiwe Mponyaji, hakuna ponyo ispokuwa ponyo Lako, ponyo lisilobakisha ugonjwa wala maumivu.

يُغَادِرُ سَقَمًا وَلاَ أَلَمًا﴾.

Njia Ya Tano

Utauweka mkono wako mahali unapoumwa, na utamzungua kwa *Sûratul-Ikhlâs*, *Al-Falaq* na *An-Nâs*.

*****

SAMPULI ZA KIUTENDAJI YA KUTIBU KIJICHO

Sampuli Ya Kwanza
Mtoto Yuwakataa Ziwa La Mama Yake

Nilikuwa nikiwatembelea baadhi ya jamaa. Wakanambia kuwa, mtoto wao amekataa ziwa la mama yake yapata siku nyingi baada ya kuwa akinyonya kama kawaida. Nikawaambia: "Mleteni mtoto." Wakamleta. Nikamzungua kwa *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu A<u>h</u>ad, Qul-a'ûdhu Birabbil-Falaq* na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*) na baadhi ya dua zilizopokewa. Halafu nikawaambia: "Mpelekeni kwa mama yake." Papo hapo wakaja wakinipa habari njema kuwa mtoto amelishika ziwa la mama yake. Fadhila ni za Allâh Pekee!

Sampuli Ya Pili
Kijana Asita Kuzungumza

Alikuwa ni mtoto fasaha, hodari na aliyewashinda wenzake, katika umri wa wastani. Alikuwa akizungumza kwa niaba yao katika minasaba mbalimbali, na akiwazungumzia watu katika sherehe za kila aina. Siku moja, mmoja katika vijana wa kijijini mwao alifariki. Kijana huyu yeye na watu wa kabila lake wakaenda kuwataazi. Akamhimidi Allâh na akamsifu. Halafu akawaidhi watu mawaidha fasaha kabisa. Haikufika usiku, akawa bubu hasemi. Baba yake akababaika na akampeleka hospitali. Madaktari wakafanya kila uchunguzi na picha za *x-ray* za lazima, lakini wapi, bila mafanikio! Akaniletea. Nilipomuona nilikaribia kulia – kwa sababu nafahamu nishati zake za Kiislamu akiwa Madrasa – lau kama nisingejizuia. Nikamwuliza. Baba yake akanitolea kisa chote, na mtoto amenyamaa. Nikafahamu kuwa mtoto amesibiwa na kijicho. Nikamzungua kwa *Mu'awwidhâti* (*Qul-Huwallâhu A<u>h</u>ad, Qul-a'ûdhu*

Birabbil-Falaq na *Qul-a'ûdhu Birabbin-Nâs*). Halafu nikamsomea zunguo la kijicho katika maji. Nikamwambia baba yake kuwa, atakunywa na ataogea maji haya siku saba kisha aje. Baada ya siku saba alinijia na amepona. Na akarudia hali yake ile ya ufasaha kama kawaida yake. Nikamfundisha kinga awe akizisoma asubuhi na jioni ili zimlinde dhidi ya kijicho. *Alhamdulillâh!*

Sampuli Ya Tatu
Jambo La Ajabu

Jambo hili lilitokea nyumbani kwetu. Kwa ufupi ni kuwa, nilijiwa na mwanamume na ajuza. Yule mwanamume akaketi nami sebuleni akinihadithia kisa cha mama yake. Na yule ajuza aliingia kwa mke wangu. Baadaye nikamwita. Nikamsomea kisha wakaondoka. Nilipotazama nyumbani, niliona mabuu weupe wengi mno! Nikastaajabu kwa hali hiyo. Mke wangu akaisafisha nyumba kwa ufagio. Lakini kwa haraka sana mabuu yakarudi tena katika vyumba vyote.

Lo! Nikamwambia mke wangu hebu njoo tutafakari juu ya swala hili (*mmakubwa haya!*). Yule ajuza alikwambia nini?

Akasema: "Alikuwa akiitazama nyumba na akiikodolea macho wala hazungumzi chochote." Nikafahamu kuwa alikuwa ana kijicho pamoja na kuwa nyumba yetu ilikuwa ni ya kawaida sana. Lakini pengine ajuza yule alikuwa akiishi jangwani na hajawahi kabisa kuona miji.

Muhimu ni kuwa, nilichukua maji nikayasomea zunguo la kijicho, nikayanyunyiza maji yale kando kando ya nyumba, yale mabuu yakatoweka kwa haraka mno, na nyumba ikarudia hali yake ya kawaida.

Twamhimidi Allâh Aliye Mmoja Mwenye kulipa.

﴿سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُوبُ إِلَيْكَ﴾.

Subhânakallâhumma wabihamdika ash-hadu allâ-ilâha illâ anta astaghfiruka wa atûbu ilayk. [1]

MWISHO

---

(1) Ewe Mola, Umetakasika, Himdi ni Zako. Nashuhudia kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki ispokuwa ni Wewe, nakuomba msamaha na natubia Kwako.

VITABU VINGINE VILIVYOTAFSIRIWA

TAFSIRI YA *AL-ADHKÂR*

Mtungaji: al-Imâm Abû Zakariyyâ; Yahyâ bin Sharaf an-Nawawy
Mfasiri: 'Uthmân Muhammad 'Alî

Kitabu hiki:
Kitabu cha *al-Adhkâr* ni miongoni mwa vitabu mashuhuri mno alivyoandika Imâm Nawawy رحمه الله تعالى; ni kitabu muhimu na kilichoenea kwa wingi, kimekusanya *Adhkâr* za mchana na usiku. Kimejumuisha mambo anayohitajia mtu katika hali zake zote, ikiwemo *Adhkâr* na dua za mchana na usiku kwa muda wa mwaka mzima, bali katika umri wake wote.

Imâm Nawawy رحمه الله تعالى amesema katika *ar-Rawdha*: "Kitabu hicho (*al-Adhkâr*), mtu aliyeshikamana na Dini, hafai kukikosa."

Kitabu hiki ni akiba ya waliokatikia kufanya ibada na wanaomtaja Allâh, ni kiongozi kwa Waislamu.

Mwanachuoni hawezi kuwa mbali nacho ili kurudia rudia maudhui yaliomo ndani yake, khatibu ni lazima akitegemee, anayemtaja Allâh hachoki nacho, anayekisoma atapata Hukmu za kifiqhi (Sharia) na faida kubwa za kiilimu.

Wanazuoni waliopita walinena: "Uza nyumba ununue *al-Adhkâr*." Mwingine akasema: "Asiyeisoma *al-Adhkâr*, huyo hafanyi Dhikri."

Hadîth zilizotajwa humu, zimeandikwa pamoja na nambari zake kama zinavyopatikana katika vitabu vya Hadîth.

Hadîth ambazo ni *Dha'îf* lakini mtungaji hakuzibainisha, zimeelezwa udhaifu wake, kwa kutegemea vitabu vilivyobainisha Hadîth hizo.

al-Adhkâr ni kitabu kilicho na faida adhimu, yatakiwa kila Muislamu akisome na awe akikirudia mara kwa mara. Yatosha kuwa kimejazwa tahakiki na maelezo ya Imâm Nawawy, kwani maelezo yake yana ladha yake maalumu, msomaji huwa akihisi jinsi anavyofaidika na kukihitaji kile akisomacho.

Imâm Nawawy رحمه الله, kitabu chake hiki amekipangilia kwa uzuri mno, Allâh Amewanufaisha Waislamu kwa kitabu hiki. Nasi hatuna la kumlipa ela ni kumuombea dua, Allâh Amrehemu na Amlipe majazi mema. *Âmîn*.

TAFSIRI YA *MUKHTASAR SAHÎHIL-BUKHÂRY*

Mwandishi: Ibnu Abî Jamrah al-Andalusy
Mfasiri: 'Uthmân Muhammad 'Alî

Mbali na kutafsiri, kazi nyingine ya ziada ni:

1. Hadîth zilizomo humu, zimehakikiwa katika *Sahîhul-Bukhâry*.
2. Kuitaja Hadîth kwa ukamilifu bila ya kuifupisha, ambapo mwandishi wa asili (Ibnu Abî Jamrah), alikuwa akichagua sehemu fulani.
3. Wakati mwingine, huwa akitajwa mpokezi muhimu ambaye huenda akawa ni taabii au aliyekuja baada ya taabii ili ipatikane asili ya kisa chenyewe kuanzia mwanzo, au sababu ya kutajwa Hadîth hiyo ili ifahamike kwa uwazi zaidi.
4. Hadîth zimewekewa milango ili kurahisisha kufahamika, ambapo Ibnu Abî Jamrah alikusudia kutofanya hivyo.
5. Wasifu wa Imâm Bukhâry umeelezwa kwa urefu kiasi.

TAFSIRI YA *BULÛGH AL-MARÂM* (Kuyafikia makusudio kutoka katika mkusanyiko wa dalili za Hukumu za Sharia)

Mtungaji: al-Hâfidh Ibnu Hajar al-'Asqalâny
Mfasiri: 'Uthmân Muhammad 'Alî

- Kitabu hiki kimekusanya misingi ya dalili za ki-Hadîth juu ya Hukumu za Sharia.
- Fiqhi (Sharia) ni lazima iwe na dalili ya Qur'ân au Hadîth. Kitabu hiki kimejumuisha mambo mengi kutoka katika Hadîth kwa ibara fupi. Kwa ajili hii Ulamaa wengi walikitumia kitabu hiki kwa kuhifadhi, kusomesha na kukisherehesha. Anayesoma wasifu wa mwanachuoni yeyote, aghlabu atakuta kuwa jumla ya vitabu alivyohifadhi ni *Bulûgh al-Marâm* kama ambavyo kitabu hiki husomeshwa katika vikao vya kiilimu. Huwezi kuingia mji wowote ukakosa darasa ya kitabu hiki.
- Mwandishi alikipangilia kulingana na milango ya Fiqhi, akianzia katika Mlango wa Twahara mpaka mwisho wa mambo ya ibada. Kisha akaingilia muamalati: biashara, Nikaha hadi mwisho. Amekhatimisha kitabu chake kwa kuandika Kitabu kilichojumuisha Adabu, Wema, Kuunga kizazi, Kuipa mgongo dunia, Uchamungu na kuhadharisha tabia mbaya, akakhatimisha kitabu kwa Mlango wa Dhikri na Dua, akataja dalili kutoka katika Hadîth pamoja na kufanya umuhimu wa kumtaja aliyeipokea Hadîth hiyo.
- Ameweka umuhimu wa kuwataja walioipokea Hadîth, kuzungumza juu ya isnadi ya Hadîth, kuwataja wapokezi wake, kubainisha udhaifu wa Hadîth na kumtaja aliyeitaja Hadîth hiyo mbali ya vile Vitabu Sita vya Hadîth.
- Kuwataja Maimamu walioisahihisha Hadîth au kuifanya ni *Hasan* au *Dha'îf*, ambapo jambo hili ndio roho ya ilimu ya Hadîth, na Sharia inategemea hapo.
- Kuzifwatilia njia za Hadîth pamoja na kubainisha *Sahîh* na *Dha'îf*.
- Kutaja ziada zilizothibiti katika matini ya Hadîth ambazo hazimo katika Vitabu Sita vya Hadîth.
- Kufupisha katika *al-Jarh* na *Ta'dîl* (kasoro au sifa nzuri aliyonayo mpokezi) kwa ibara fupi, jambo ambalo ladhihirisha umahiri wa mwandishi wa kitabu hiki.
- Kuzitaja Hadîth zinazotegemewa na madhehebu mingine bila kubagua madhehebu fulani.

KITABU CHA SAUMU Kutoka katika *Bulûghul-Marâm* pamoja na maelezo
Mtungaji: al-Hâfidh Ibnu Hajar al-‘Asqalâny
Mfasiri: ‘Uthmân Muhammad ‘Alî

Kitabu hiki, kimetolewa katika Tafsiri ya *Bulûghul-Marâm*, Hadîth ni zile zile, ispokuwa humu yameongezwa maelezo marefu kiasi kwa ajili ya kumfafanulia msomaji. Kazi yenyewe ilifuata utaratibu huu:

- Maelezo yaliyokuwamo katika *Bulûghul-Marâm*, hayakuondolewa.
- Fauka ya Hadîth zilizomo katika *Bulûghul-Marâm*, muna Hadîth nyingine zimeongezwa, zikianza na ibara: **Nyongeza ya Hadîth.**
- Tarakimu za Hadîth, ni zile zile kwa mtiririko ule ule wa *Bulûghul-Marâm*.
- Kizuri zaidi, ni kuongezwa anwani ndogo ndogo zinazotoa mwongozo wa kila Hadîth takriban, anwani hizo utazitambua kwa kuwa zimewekewa mabano kama [hivi] kwa upande wa maandishi ya Kiarabu.
- Asili ya kitabu kimewekwa ndani ya fremu, na maelezo yake yako nje, na kama kuna cha zaidi, basi kimewekwa chini ya ukurasa huo huo.
- Mengine mazuri, atajionea mwenyewe msomaji.
- Mwisho muna *Kiambatisho Cha Dua* tulizofundishwa na Mtume صلى الله عليه وآله وسلم.

TAFSIRI YA *‘UMDATUL- AHKÂM*
Mtungaji: al-Hâfidh Taqiyyuddîn ‘Abdul-Ghaniy al-Maqdisy
Mfasiri: ‘Uthmân Muhammad ‘Alî

- Ni kitabu cha Hadîth kwa mpangilio wa milango ya Fiqhi (Sharia).
- Jumla ya Hadîth zake ni: 428, zimedondolewa kutoka katika *Sahîhul-Bukhârî* na *Sahîh Muslim* pekee.

- Kitabu hiki, ni mojawapo ya hazina kuu ya Hadîth iliyowekwa na Mwanachuoni mkubwa katika fani ya Hadîth na Sharia.
- Ulamaa wengi wamekisherehesha, kila mmoja kwa namna yake.
- Ufafanuzi wa Hadîth, umetolewa katika *Sherehe ya Sahîh Muslim* ya Imâm Nawawy, *Fat-hul-Bârî* ya al-Hâfidh Ibnu Hajar al-'Asqalâny رحمة الله عليهما, *Taisîrul-'Allâm, Sharhu 'Umdatil-Ahkâm*, ya Sheikh 'Abdullâh bin 'Abdirrahmân bin Sâleh Âl Bassâm, na vitabu vinginevyo kama atakavyoona msomaji.
- Maneno magumu yamefafanuliwa katika ukurasa huo huo, na yakaorodheshwa tena mwisho wa kitabu pamoja na maana yake.
- Kina maelezo wastani ya kila Hadîth na tafiti mbali mbali kwa mujibu wa Hadîth hiyo.

TAFSIRI YA *HISNUL-MUSLIM* (Ngome ya Muislamu Kutoka katika Qur'ân na Sunnah)
Mkusanyaji:
Sheikh Sa'îd Bin 'Alî Bin Wahf al-Qahtânî
Mfasiri: 'Uthmân Muhammad 'Alî

- Kitabu hiki kimetafsiriwa kwa lugha nyingi; ikiwemo Kiswahili.
- Katika chapa hii, muna maendelezo ya Dua kwa Kiswahili pamoja na irabu zake.
- Dua zilizoandikwa humu, asili yake zinatokana na Hadîth *Sahih* au *Hasan*, wala si *Dha'îf*.
- Aya zilizotajwa kwa mukhtasari, zimewekwa kwa ukamilifu ili msomaji asilazimike kuacha uradi na kupekua Msahafuni.
- Chapa hii mpya, imeshughulikiwa ipasavyo.

VITABU VINGINE VYA MWANDISHI

1. Adabu za Kusoma Qur'âni
2. Jitibu kwa Qur'âni
3. Furaha ya ndoa na siri ya unyumba
4. Kamusi ya mwanafunzi – ndogo
5. Kamusi ya mwanafunzi – kubwa
6. Kujitibu pasipo tabibu
7. Maafa ya ulimi yalogawanyika sehemu ishirini
8. Majina ya wanyama
9. Maombi arubaini ya *Allâhumma*
10. Miujiza ya tiba (Tafsiri ya *Mu'jizâtush-shifâ*)
11. Msingi imara wa kujifunza kusoma Qur'âni
12. Mwongozo wa twahara na Swala
13. Tafsiri ya *al-Adhkâr* ya Imâm Nawawy
14. Tafsiri ya *al-'Aqîdatul-Islâmiyyah*
15. Tafsiri ya *Bulûghul-Marâm*.
16. Tafsiri ya *Khulâsatu Nuril-Yaqîn* (1 - 3)
17. Tafsiri ya *al-Mabâdi-Ulfiqhiyyah* (1 - 4)
18. Tafsiri ya *Mukhtasar Sahîhil-Bukhârî*
19. Tafsiri ya Qur'âni inayoitwa: **Ufunguo wa Imani na Utamu wa Qur'âni** (juzuu ya kwanza).
20. Tafsiri ya *Riyâdhussâlihîn* iliyokamilishwa.
21. Tafsiri ya *as-Sârimul-Battâr* (Upanga mkali wa kupambana na wachawi waovu)
22. Tafsiri ya *Shamâ-ilul-Muhammadiyyah* (ya Imam Tirmidhy)
23. Tafsiri ya *Sharh Mukhtasar Arkânil-Islâm*
24. Tafsiri ya '*Umdatul-Ahkâm*
25. Tafsiri ya *al-Usûluth-thalâthah* misingi mitatu na dalili zake
26. Tafsiri ya *Wiqayatul-Insân* (Kinga ya mwanaadamu dhidi ya jini na shetani)
27. Tumaini maishani kwa dua za Qur'âni

YALIYOMO